# Nipashe

Jumanne Novemba 12, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580073

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Mdee arejea bungeni kwa kishindo, Ndugai amuonya

UKURASA 3




UKURASA 13

# MNYUKANO

**SERIKALI**, wapinzani wavutana uchaguzi mitaa, ACT-Wazalendo yatoa masharti mazito, Dovutwa aibuka, wanaharakati watoa neno...*Endelea ukurasa wa 2*



## MBARONI KUKUTWA NA MENO YA TEMBO

UKURASA 3

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, akionyesha kwa waandishi wa habari jana meno ya tembo na nyama ya twiga, zilizokamatwa katika wilaya za Arumeru na Ngorongoro juzi. PICHA NDOGO: Nyama ya twiga na nyaya zinazotumika kumtega mnyama huyo. **PICHA: DANIEL SABUNI**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## JKCI yaweka mshipa bandia moyo wa mtoto

UKURASA 2




## HABARI KITAIFA

# Mnyukano uchaguzi wa serikali za mitaa

**Na Waandishi wetu**

NI mnyukano! Ndivyo mtu anavyoweza kuelezea kutokana na vuta nikuvute kati ya serikali na vyama vya upinzani kuhusu mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa unaoendelea sasa.

Kutokana na hali ilivyo, kila upande unavutia kwake kama msemo wa 'mwamba ngoma huvutia kwake'. Hakuna anayekubali yaishe hasa baada ya kutokea 'figisu' wakati wa uchukuaji, urejeshaji fomu na kuenguliwa kwa baadhi ya wagombea wa vyama vya upinzani.

Hatua hiyo ilisababisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani jafo, kuwaruhusu wagombea wa vyama vyote waliochukua na kurejesha fomu washiriki uchaguzi huo.

Ikiwa siku moja baada ya Jafo kutoa agizo hilo, jana wabunge wa upinzani waliibuka na hoja mpya.

Hoja hiyo ni kwamba kuna idadi kubwa ya wagombea wao ambao hawakurudisha fomu kutokana na ofisi za wasimamizi wa uchaguzi kukuta zimefungwa, wengine kuzuiwa kuchukua fomu. Lakini serikali kupitia Jafo jana ndani ya Bunge iliwajibu wapinzani hao kuwa wanajaribu kuhamisha goli.

Mbunge wa Mtwara Mjini (CUF), Maftah Nachuma, katika hoja yake alisema katika Wilaya ya Liwale mkoani Mtwara, asilimia 97 ya wagombea wa chama hicho walishindwa kurudisha fomu baada ya kukuta ofisi za wasimamizi zimefungwa.

Pia alisema wako wagombea ambao walizuiwa kuchukua fomu, hivyo Waziri Jafo anapaswa kulitolea ufafanuzi suala hilo.

"Spika naomba hoja ya kuahirisha mjadala ili tujadili suala la hatari ambalo linaendelea. Uliagiza kwamba tukuletee ushahidi kwenye meza yako kuhusu wagombea kukuta ofisi zimefungwa na tumeshakuletea. Jana (juzi) Waziri Jafo alitoa ufafanuzi lakini bado kuna mambo hajayafafanua," alisema.

"Mfano wa mambo hayo ni baadhi ya maeneo mfano Liwale wagombea wote wa upinzani hawakupewa fomu pia walifungiwa ofisi, hivyo hawakujesha kwa sababu wasimamizi waliwakimbia. Mheshimiwa Spika naomba busara yako itumike ili tutumie dakika 30 kujadili kwa sababu huko kuna mambo ya hatari, hili jambo ni nyeti," alisisitiza.

Nachuma alisema Waziri Jafo alitoa maelekezo kwamba wagombea walioondolewa wote

INAENDELEA UK 8



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara katika mitaa ya Tandale, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mfumo ununuzi kumaliza rushwa

**Na Enock Charles**

SERIKALI imeanzisha mfumo mpya wa manunuzi wa kielektroniki ujulikanao kama Taneps, ambao utamaliza rushwa na urasimu katika ununuzi wa umma.

Aidha, taasisi zote za umma zimetakiwa kujiunga na mfumo huo ambao utaongeza na kupunguza gharama za ununuzi na kuimarisha mfumo wa utunzaji kumbukumbu za serikali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, alisema ili kuongeza kiwango cha uwajibikaji na kurahisisha michakato ya zabuni katika taasisi za serikali ni muhimu kwa taasisi hizo kubadili mfumo wa ununuzi na kuanza kutumia mfumo huo mpya.

"Kwa kuzingatia kuwa fedha zitumikazo katika utekelezaji wa miradi ya serikali kwa kiasi kikubwa hutumika kupitia mifumo ya ununuzi wa umma, jitihada mbalimbali zimekuwa zikitumika kuimarisha eneo hilo, hivyo naziagiza na nimeshaziandikia waraka taasisi zote 540 za ununuzi za serikali kujiunga na mfumo huu kufikia mwisho wa mwezi ujao," alisema James.

Alisema kulingana na upembuzi uliofanyika kabla ya kuanzishwa, mfumo huo umekadiriwa kuokoa wastani wa Sh. bilioni 34 kwa kipindi cha miaka

INAENDELEA UK 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
06 – 11 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **alhamisi tarehe 14 – 11 – 2019** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam kuelekea Mafinga,** gari hizo zenye namba za usajili:

| | |
|---|---|
| T 660 BZU / ZD 8121 | T 316 CZS / T 249 AGZ |
| T 628 DFA / ZD 8113 | T 210 BYM / T 146 CHN |
| T 641 DFA / T 137 CHN | T 324 CZS / T 777 AQR |
| T 245 BXH / T 380 DHQ | T 553 BKC / T 385 DHQ |
| T 645 DFA / T 377 DHQ | |

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 33**
**Upana - mita 4.70**
**Kimo - mita 5.4**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port hadi Mafinga Kupitia Iringa,** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215511102


# JKCI yaweka mshipa bandia kwenye moyo

**Na Joseph Mwendapole**

KWA mara ya kwanza madaktari bingwa wa upasuaji wa moyo kwa watoto katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), wamefanya upasuaji wa kutenganisha mshipa wa kusambaza damu kwenye mwili na kuweka mshipa bandia wa kusambaza damu kwenye mapafu.

Upasuaji huo uliochukua muda wa saa nne na nusu, ulifanyika kwa mtoto mwenye umri wa miezi mitano ambaye alikuwa na tatizo la damu safi na chafu kutokea kwenye mshipa mmoja wa damu badala ya mishipa miwili tofauti.

Mtoto huyo alizaliwa na tatizo la kuwa na mshipa mmoja wa damu ambao ulikuwa unapeleka damu kwenye mwili na mapafu kutoka kwenye moyo badala ya mishipa miwili ya 'Aorta' ambao unapeleka damu kwenye mwili na 'Pulmonary Artery' ambao unapeleka damu kwenye mapafu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, daktari bingwa wa upasuaji wa moyo kwa watoto wa taasisi hiyo, Godwin Sharau, alisema wametengeneza mshipa wa damu bandia ambao unabeba damu chafu kutoka kwenye chumba cha chini cha kulia cha moyo na kupeleka kwenye mapafu ili kutenganisha damu chafu na safi.

"Katika upasuaji huo tumefanikiwa pia kuziba tundu la moyo na kulitenganisha kutoka kulia na kushoto ili kusaidia mzunguko wa damu kuwa katika hali ya kawaida. Mshipa huu bandia utadumu kwa muda wa miaka 10 hadi 15 baada ya hapo utabadilishwa na kuwekwa mkubwa zaidi tofauti na wa sasa ambao ni mdogo," alisema.

"Aina hii ya magonjwa ya moyo ni nadra sana kutokea lakini katika mazingira yetu tumekuwa tukiwaona watoto wenye matatizo kama haya na watoto kama hawa wasipopata matibabu ndani ya miezi sita tangu kuzaliwa kwao, wanaweza kupoteza maisha", alibainisha.

Dk. Sharau alisema kwa mwaka

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Mdee arejea bungeni kwa kishindo, Ndugai amuonya

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

MBUNGE wa Kawe (Chadema), Halima Mdee, jana, alirejea bungeni kuendelea kushiriki vikao, huku akisababisha kishindo cha shangwe kutoka kwa wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

Hali hiyo ilimsababisha Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuwaonya wabunge wenzake wa upinzani waliokuwa wakimshangilia mbunge huyo.

Mdee amerejea bungeni baada ya kumaliza kutumikia adhabu aliyopewa ya kutoshiriki mikutano miwili kwa kosa la kuunga mkono kauli iliyotolewa na aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prod. Mussa Assad, kwamba Bunge ni dhaifu.

Aprili 2, mwaka huu Bunge liliridhia mapendekezo ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuwa Mdee asimamishwe kushiriki mikutano miwili ya Bunge ukiwamo Mkutano wa Bajeti wa 15 na Mkutano wa 16 uliofanyika Septemba, mwaka huu.

Jana, Mdee aliingia ndani ya mhimili huo wa kutunga sheria majira ya saa tatu asubuhi wakati wa kipindi cha maswali na majibu na kuwasalimia baadhi ya wabunge, huku akishangiliwa na baadhi ya wabunge wenzake wa upinzani.

Hali hiyo, ilimlazimu Spika wa Ndugai kuwaonya wabunge waliokuwa wanashamshangilia Mdee kwa kuwaambia: "Mnaweza kumponza tena, nadhani mnanijua huwa sitanii. Nakuomba Mheshimiwa Mdee ukae tafadhari."

Baada ya muda kidogo, Spika Ndugai alimpa nafasi Mdee kuuliza swali, ambaye alitaka kupata majibu ya serikali kuhusu fidia kwa wakati wa maeneo ya Chuo Kikuu cha Ardhi (Aru), Makongo Juu na Goba wilayani Kinondoni waliopisha ujenzi wa barabara.

"Barabara ya Chuo Kikuu cha Ardhi-Makongo Juu-Goba iko katika mkakati wa ujenzi baada ya kero ya muda mrefu, sasa naomba kujua fidia ya Sh. bilioni tatu kwa wakazi wa maeneo hayo waliopisha ujenzi italipwa lini?" Alihoji Mdee.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, alisema suala la fidia kwa wakazi wa maeneo hayo lipo kwa mujibu wa sheria na siyo la makubaliano.



Mkurugenzi Mtendaji wa Precision Air, Patrick Mwanri (kushoto), akifanyiwa mahojiano na Mtangazaji wa East Africa Radio, Ian Dialo, ikiwa ni mwendelezo wa Kampeni ya Kibiashara zaidi inayoendeshwa na East Africa Television na East Africa Radio, ofisini kwake, jijini Dar es Salaam jana, yenye lengo la kuchochea ukuaji wa shughuli za kibiashara nchini. **PICHA: EATV/RADIO**

# Mbaroni kwa kunaswa na meno ya tembo

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

JESHI la Polisi mkoani Arusha linawashikilia watu saba kwa tuhuma za kukutwa na meno mawili ya tembo na nyama ya twiga ambaye anadaiwa kuuawa na watuhumiwa hao wa ujangili.

Watuhumiwa wawili kati ya hao, Nyamhanga Mwanga Mwita (19) na Chacha Marwa Mtocho (20) wote wakazi wa Serengeti mkoani Mara, walikamatwa na nyama ya twiga baada ya kumuua.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema watuhumiwa hao walikamatwa na nyama hiyo wakiwa wanaanika porini ili waisafirishe.

Mbali na kukamatwa na nyama hiyo, pia alisema walikutwa na panga, sime, tochi, kisu na nyaya za kutegea wanyama zikiwa katika mafungu saba.

Shana aliwataja watuhumiwa wengine waliokamatwa na meno ya tembo kuwa ni Thomas Kiteo (29), Edward Mollel (30), Emmanuel Sengeu (40) na Lembris Meyan (45) wote wakazi wa Simanjiro mkoani Manyara na mwenzao Samweli Nassari (53) mkazi wa King'ori wilayani Arumeru.

Alisema meno hayo yalipatikana juzi majira ya saa 11:40 jioni maeneo ya Mbuyuni wilayani Arumeru baada ya polisi kupata taarifa za kiintelijensia kuwa meno hayo yaliyofichwa wilayani Simanjiro, yameletwa Arusha kwa ajili ya kuuza na watuhumiwa wapo kwenye pikipiki.

"Tuliweka mtego na tulikamata pikipiki mbili aina ya Kinglion yenye namba za usajili T.917 BUA na Sunlag yenye namba za usajili MC 819 ACD ambazo zilibeba meno hayo," alisema.

Shana alisema hayo ni mafanikio ya jeshi hilo kwa kushirikiana na Kikosi

INAENDELEA UK 8

# Vyakula vyapaisha mfumuko wa bei

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

BEI ya bidhaa za vyakula kwa kipindi kilichoishia Oktoba 2019 imesababisha mfumuko wa bei kuongezeka kutoka asilimia 3.4 hadi 3.6.

Baadhi ya bidhaa hizo ni mchele, unga wa mahindi, unga wa muhogo, nyama, samaki, maziwa ya ng'ombe, mafuta ya kupikia, maharage, mihogo na viazi vitamu.

Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii, Ruth Davison, alisema jana kuwa mfumuko wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia Oktoba 2019, umeongezeka hadi kufikia asilimia 3.6 kutoka asilimia 3.4 kwa mwaka ulioishia Septemba 2019.

"Hii inamaanisha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa ulioishia Oktoba 2019 imeongezeka ukilinganisha na kasi iliokuwapo kwa mwaka ulioishia Septemba 2019," alisema Davison.

Alisema kuongezeka kwa mfumuko wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia Oktoba 2019 kumechangiwa hasa na kuongezeka kwa bei ya baadhi ya bidhaa za vyakula kwa kipindi kilichoishia Oktoba 2019 ikilinganishwa na mwaka 2018.

Aliainisha baadhi ya bidhaa za vyakula zilizoongezeka bei kwa Oktoba zikilinganishwa na bei za mwezi Oktoba 2018 ni pamoja na mchele kwa asilimia 6.1, unga wa mahindi kwa asilimia 20.5, unga wa muhogo kwa asilimia 10.9.

Kwa upande we nyama imeongezeka kwa asilimia 2.2, samaki kwa asilimia 16.4, maziwa ya ng'ombe kwa asilimia 3.6, mafuta ya kupitia kwa asilimia 7.0, maharage kwa asilimia 4.9, mihogo kwa asilimia 17.0 na viazi vitamu kwa asilimia 8.7.

Alifafanua zaidi kuwa mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia Oktoba 2019 umeongezeka kwa asilimia 5.1 kutoka asilimia 4.0 kwa mwaka ulioishia Septemba 2019.

Kuhusu mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki, alisema Kenya kwa mwaka ulioishia Oktoba 2019 umeongezeka hadi asilimia 4.95 kutoka asilimia 3.83 kwa mwaka ulioishia Septemba 2019.

Uganda mfumuko wa bei ulioishia Oktoba 2019 umeongezeka hadi asilimia 2.5 kutoka asilimia 1.9 kwa mwaka ulioishia Septemba 2019.




## HABARI KITAIFA

# Mamlaka za maji 36 zafutwa

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SERIKALI imezifuta mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 36 na maeneo yake yatahudumiwa na mamlaka za makao makuu ya mikoa 25, zilizoundwa na kuongezewa majukumu ya utoaji huduma.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kilila Mkumbo, alipokuwa akitoa taarifa ya wizara juu ya maboresho hayo kwa waandishi wa habari jijini Dodoma.

Prof. Mkumbo alisema katika kiimarisha uendeshaji wa sekta ya usambazaji maji na usafi wa mazingira mijini, Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, kwa mamalaka aliyonayo kwa mujibu wa sheria, ameongeza maeneo ya huduma za maji.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5, ya mwaka 2019, ameongeza maeneo ya huduma kwa baaadhi ya mamlaka za maji na usafi wa mazingira nchini. Aidha, Waziri wa Maji ameanzisha na kufuta baadhi ya mamlaka za maji na usafi wa mazingira nchini," alisema.

Alisema katika mabadiliko hayo kutakuwa na mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 25, katika ngazi ya makao makuu au miji mikuu ya mikoa.

Pia alisema mamlaka hizo zitahudumia halmashauri zilizopo katika miji mikuu, makao na makuu ya mikoa husika.

"Aidha baadhi ya mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira katika ngazi hii zimeongezewa maeneo ya huduma na kuunganishwa na baadhi ya miji midogo katika mikoa husika au mikoa ya jirani," alisema.

Alizitaja baadhi ya mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira za mikoa zilizoongezewa majukumu ni Mamlaka ya Maji na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) ambayo itahudumia hadi maeneo ya Bagamoyo, Kibaha, Kisarawe na Mkuranga.

"Mamlaka nyingine ambayo imeongezewa majukumu ni Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA), ambayo nayo pia itahudumia eneo lake la jiji pamoja na miji ya Kongwa, Bahi na Chamwino," alisema.

Nyingine ni Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) ambayo imeongezewa miji ya Kilosa na Mikumi.

"Pia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) ambayo itahudumia Halmashauri ya Jiji la Mwanza na manispaa zake na mji wa Magu, Nansio na Ngudu," alisema.

Vilevile, alisema mamlaka za maji na usafi wa mazingira za miji midogo ya wilaya 40, zitasimamiwa na mamlaka ya maji vijijini (RUWASA) katika wilaya husika.

Alizitaja baadhi ya mamlaka za maji na usafi wa mazingira za miji midogo ya wilaya zitakazo kuwa chini ya Ruwasa ni Halmashauri ya Chemba na Kondoa.

Baadhi ya mamlaka za maji na usafi wa mazingira zilizofutwa kati ya 36, ni Kibaha WSSA, Kongwa WSSA, Chamwino WSSA, Kilosa, Kyela WSSA, Mikumi WSSA, Pangani WSSA, Magugu WSSA.

Kwa mujibu wa Prof. Mkumbo, lengo ni kuongeza ufanisi na kupunguza matumizi ya fedha ili kiasi chote kiende katika utekelezaji wa miradi katika maeneo ya wananchi.

Distributed via




Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Salome Kitomari (kushoto), akifurahia jambo na mhitimu mwenzake, Zulfa Nyangasa, wakati wa mahafali ya 13 ya Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (TUDARCo), yaliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**






# Bil. 43/- kulipa wakulima pamba mwisho wa mwezi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema kiasi cha Sh. bilioni 43 kinachodaiwa na wakulima wa pamba kitalipwa mwisho wa mwezi huu.

Aidha, hadi sasa kiasi cha Sh. bilioni 437 kimelipwa kwa wakulima wa zao la pamba.

Bashe alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Busega (CCM), Raphael Chegeni, ambaye alihoji serikali ina mkakati gani kutatua changamoto za wakulima wa mazao ili wapewe bei za kuwakomboa hususani zao la pamba.

Bashe alisema kuwa tatizo la pamba lililojitokeza mwaka huu ni kama ilivyojitokeza kwenye korosho mwaka jana na kwamba mwaka huu wameruhusu soko na minada ili wakulima wapate fedha kwa wakati.

"Tatizo la pamba lililojitokeza katika msimu uliopita halitajitokeza katika msimu ujao na serikali itakachofanya kwa wakulima wa pamba ili wasipate hasara ni kudhibiti gharama za viuatilifu, mbegu na mambo mengine lakini siku ya mwisho sokoni tutaruhusu bei ili wafanyabiashara wakutane na wakulima masokoni wanunue bidhaa hiyo na wahusika wapate pesa kwa wakati,"alisema.

Aidha, alisema bei ya pamba duniani ilianguka kutokana na mgogoro uliopo kati ya China na Marekani.

"Matokeo yake pamba ikakosa bei hivyo serikali ikaamua kutangaza bei kwa Sh. 1,200 ili wafanyabiashara wasipate hasara tukaamua kufanya mazungumzo na baadhi ya taasisi za fedha ili wanunue kwa bei hiyo mpaka ijumaa iliyopita wakulima wamelipwa kiasi cha Sh. bilioni 437,"alisema.

Hata hivyo, alisema kiasi cha Sh. bilioni 43 ambacho hakijalipwa serikali itahakikisha mwisho wa mwezi huu wakulima wa pamba wanalipwa.

Vile vile, aliwataka katika msimu unaoanza Novemba 15 wasambazaji wa mbegu wasambaze bila kuwadai wakulima chochote na kwamba watalipwa gharama zao msimu ujao.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji maana ya dhana ya uchumi kukua ukilinganisha na maisha ya wananchi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alisema dhana ya uchumi kukua ukilinganisha na maisha ya wananchi inaweza kutafsiriwa katika dhana kuu mbili.

Alibainisha kuwa dhana hizo ni pamoja na kuangalia upatikanaji, ubora na gharama za huduma za jamii zinazotolewa na serikali.

## HABARI KITAIFA

# Mabweni yapaisha elimu, yamaliza mimba shuleni

**Na Elizabeth Zaya, MAKAMBAKO**

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Sekondari Mlowa, katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, Raymond Kyando, amesema ujenzi wa mabweni katika shule hiyo umesaidia kuongeza kiwango cha elimu na kumaliza mimba kwa wanafunzi wa shule hiyo.

Akizungumza na wanahabari shuleni hapo, Kyando alisema mabweni hayo yamejengwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) kupitia miradi inayofadhiliwa na umoja wa nchi zinazozalisha na kusambaza mafuta duniani (OPEC).

Alisema miongoni mwa sababu zilizokuwa zikichangia wanafunzi hao kupata mimba katika shule hiyo ni kutokana na kutembea umbali mrefu kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

"Tunaishukuru sana Tasaf kupitia miradi yake ya OPEC, wametujengea mabweni ya wasichana yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 72, huu umekuwa mkombozi mkubwa kwetu, kwa maana kwamba mimba katika shule yetu itabaki kuwa historia, na hata sasa hivi hali ya wanafunzi kitaaluma imepanda," alisema Kyando.

Aliongeza: "Kabla ya wanafunzi kuhamia hosteli mwaka 2017, mimba zilikuwa nne na hawa walikokuwa wanashawishiwa huko mtaani walikokuwa wanaishi, lakini kwa sasa hali ni nzuri hatujapata kesi za namna hiyo, na wanafunzi wanasoma vizuri."

Mwalimu wa masomo ya Kiswahili na Kiingereza wa shule hiyo, Nzangwa Mtimagulache, alisema kabla ya kujengwa kwa mabweni hayo, alikuwa anatumia pikipiki yake kuwachukua wanafunzi njiani kuwapeleka shuleni.

"Wakati mwingine tulikuwa tunachelewa kuanza vipindi darasani kwa kuwasubiri wanafunzi wafike, mimi mwenyewe nilikuwa naishi mtaani umbali wa kilomita 12... kwa hiyo kwa sababu nilikuwa na pikipiki, nilikuwa nalazimika kupakia wanafunzi kwa mtindo wa 'mishikaki' na kuwapeleka shuleni," alisema Mtimagulache.

Mwanafunzi wa kidato cha nne wa shule hiyo, Uleliya Msemwa, alisema miongoni mwa changamoto walizokuwa wanakabiliana nazo kabla ya kuhamia kwenye mabweni ni pamoja na kusumbuliwa na wanaume.

Ofisa Ufuatiliaji wa Tasaf katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, Edwin Mlowe, alisema miradi iliyojengwa na Tasaf kwa ufadhili wa OPEC katika shule hiyo mbali na mabweni, ni nyumba za walimu za kuishi walimu wanne na ofisi ya utawala.

Alisema majengo yote hayo kwa pamoja yametumia gharama ya zaidi ya Sh. milioni 287.8.

# Balozi India afichua mgogoro wa ardhi kwao ulivyomalizwa

**Na Romana Mallya**

BALOZI wa India Tanzania, Sanjiv Kohli, amesema Mahakama Kuu ya India, imetoa hukumu ya mgogoro wa kihistoria wa umiliki ardhi ya Badri baina ya Mabaniani na Waislamu nchini humo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Balozi Kohli alisema kuwa, katika hukumu hiyo, Mabaniani (Wahindi) wamekabidhiwa ardhi hiyo ili wajenge kanisa lao.

"Ujumbe wetu siyo kwa Wahindi wa Tanzania pekee bali kwa watu wote duniani waendelee kuimarisha amani, upendo, mshikamano na kufanya kazi pamoja kuendeleza amani katika nchi zao," alisema.

Balozi Kohli alisema hukumu hiyo ilitolewa Jumamosi chini ya jopo la majaji watano waliopitisha uamuzi huo wakiongozwa na Jaji Mkuu, Ranjan Gogoi.

Alisema katika hukumu hiyo, iliamuliwa kuwapatia Mabaniani eneo hilo la ardhi iliyopo kwenye mji wa Ayodhya katika Jimbo la Uttar Pradesh Kaskazini mwa India ambapo awali ulikuwapo msikiti.

Balozi Kohli alisema serikali ya India bila kuingilia tatizo hilo, iliiachia Mahakama ya India kutoa uamuzi.

"Hukumu imefuata sheria na masuala ya kiufundi na siyo kwa imani. Hukumu ilitilia maanani ushahidi wa kimazingira uliokusanywa na mawakala wataalamu," alisema na kuongeza:

"Kwa mujibu wa hukumu, mali hii itakabidhiwa kwa mfuko wao ili wajenge kanisa na sehemu nyingine itakabidhiwa kwa Sunni Waqf Board kwa ajili ya ujenzi wa msikiti."




Meneja Huduma kwa Wateja wa Benki ya NMB, tawi la Oyster Plaza, Zuhura Mkumba (kulia), akikabidhi sehemu ya msaada wa fulana 350 kwa Mjumbe wa Umoja wa Wake wa Viongozi 'New Millennium Women Group', Germina Lukuvi, kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 10 ya umoja huo, yaliyofanyika jijini Mwanza juzi. Kushoto ni Mjumbe wa Umoja huo, Rahma Othman. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kortini tuhuma za utakatishaji fedha

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA George Mapalala (47), amefikishwa mahakamani akikabiliwa na tuhuma za uhujumu uchumi ikiwamo kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha zaidi ya Sh. milioni 33 kutoka kwa Sista wa Shirika la Ekaristi Takatifu na Uinjilishaji Mpya wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha.

Mapalala alisomewa mashtaka yake jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Saada Mohammed, alidai kuwa Machi 15, mwaka huu eneo la Mbezi Luis kwa Yusufu Wilaya ya Ubungo jijini Dar es Salaam kwa njia ya udanganyifu, mfanyabiashara huyo alijipatia Sh. 33,175,000 kutoka kwa mtawa (Sista) huyo kwa lengo la kusajili taasisi mpya, huku akijua si kweli.

Ilidaiwa kuwa Mapalala alitakatisha Sh. 33,175,000, huku akijua kuwa fedha hizo ni mazalia ya kosa tangulizi la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Hakimu Shaidi alisema mshtakiwa hatakiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Hata hivyo, upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa shauri hilo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Shaidi aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 25, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na mshtakiwa alirudishwa rumande kwa sababu mashtaka hayo hayana dhamana.

**Ilidaiwa kuwa Mapalala alitakatisha Sh. 33,175,000, huku akijua kuwa fedha hizo ni mazalia ya kosa tangulizi la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.**

absa
Maelfu ya maeneo
kukurahisishia huduma za kibenki
Zaidi ya matawi 1 000 na ATM karibu 10 000 zinatufanya kuwa benki ya Kiafrika inayoongoza. Tembelea absa.africa
BARCLAYS

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Serikali ikomeshe udhalilishaji huu

**KATIKA** moja ya taarifa zetu za leo tumeripoti kuhusu baadhi ya kinamama wanaojifungua katika zahanati za wilayani Same mkoani Kilimanjaro, kurudi nyumbani na taka za uzazi.

Kama wadau wa uzazi salama taarifa hizi zimetuchoma na kutuumiza. Hili jambo ambalo kwa namna yoyote linaleta fedheha na halikubaliki kwa taifa na jamii inayojua thamani ya uzazi na jukumu la mwanamke katika uzazi wa watoto.

Tunaona kuwa hatua hiyo ni kinyume na haki za binadamu na utu wa mwanamke ambao unaweza kufananishwa na udhalilishaji usio na kifani. Kama taifa haipendezi mama kujifungua na kurudi nyumbani akiwa amefungashiwa mfuko au nyumba ya mtoto (kondo la nyuma), lakini pia bila kuoga wala kufua nguo zilizotumika wakati wa kumpata mtoto, kisa hakuna maji.

Suala hili lililoripotiwa na vituo vya Taarifa na Maarifa vya Kata za Lugulu linadokeza kuwa tatizo la maji katika hospitali hizo limekuwa sugu.

Aidha, inasemekana kuwa kinamama wanaojifungua katika zahanati hiyo wanatakiwa kwenda na majini wodini. Hii ni ajabu na jambo la kizamani.

Lakini, taarifa zetu zinaeleza kuwa hakuna tanuru la kuchomea taka hizo, wala shimo la kutupa taka mbichi za uzazi hasa nyumba ya mtoto pindi mjamzito anapojifungua.

Inasikitisha zaidi inapoelezwa kuwa huwalazimu kinamama hao kufungashiwa taka hizo na kurudi nazo nyumbani wakatupe wenyewe.

Habari hizi ni za kusikitisha mno na kukatisha tamaa kinamama na wadau wa uzazi salama. Tunaomba juhudi za lazima zifanywe ili kuwasaidia kinamama hawa ambao ndiyo wanaozaa wapigakura, walipa kodi na taifa letu.

Tunaona kuwa si jambo jema kwa sababu kuna mambo mengi mengine yanayoelezwa ambayo nayo hushusha heshima ya mwanamke. Inashuka zaidi kwani kuna habari zinazosema katika zahanati hizo hakuna eneo la kujifungulia na wanawake hao hulazimika kujifungulia kwenye chumba cha sindano ama eneo la kufunga vidonda.

Tunaiomba serikali ifanye utafiti na kuchukua hatua. Haitoshi kusema kuwa kinamama wanajifungua bure na kuhudumiwa bila gharama wakati wanapokwenda kujifungua, huku tena kuna madai kuwa baadhi ya zahanati za nchi yetu hazina wodi za wazazi wala maji ya kuoga baada ya kujifungua.

Tunaomba suala hilo lipewe uzito maalumu kwa kuwa pengine si Wilaya ya Same pekee, inawezekana sehemu nyingine za nchi yetu kuna tatizo hilo na pengine kubwa zaidi.

Inawezekana shida hiyo haipo vijijini hata mijini pia. Ndiyo maana tunaomba utafiti wa kina na wa haraka ufanyike ili kupata ufumbuzi.

Tunashukuru kuwa serikali inafanya jitihada nyingi za kusaidia uzazi salama, kutoa chanjo kwa watoto na kupunguza idadi ya vifo vya wanawake na watoto, lakini bila kujali huduma muhimu kama maji kwenye chumba cha uzazi juhudi hizo zinaweza kukwama. Tunapenda kusisitiza kuwa jitihada hizo zinapata doa iwapo wanawake wataachwa kurudi nyumbani na taka mbichi za uzazi kutokana na ukosefu wa maji.

Hali hiyo inaongeza mashaka kwa sababu ni rahisi kuwa na maji kuliko kuwa na wataalamu wa kushughulikia dharura za wajawazito. Aidha, kama ni vigumu kujenga tanuru la kuchoma taka za uzazi itawezekana kuwa na wabobezi wa kuwasaidia matatizo yakitokea?

Tunapenda kukumbusha wanawake wanaweza kususia kujifungulia hospitalini ikiwa wanakutana na changamoto kama hizo.

Tunarudia tena kuiomba serikali ifanye juu chini kuchunguza na kufahamu ukubwa wa tatizo hilo kitaifa na kurekebisha kasoro hiyo ili kuwanusuru kinamama na aibu hiyo na kurejesha heshima na utu wa mwanamke.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Raphael Kibiriti

# Serikali isikilize kilio cha wakulima hawa wanaodai

**NIMEVUTIKA** kuendelea kuzungumzia kadhia ya baadhi ya wakulima wa pamba ambao hawajalipwa fedha zao hadi sasa, wengi wakiwa kwenye maeneo ya Kanda ya Ziwa, wakati msimu mpya wa kilimo ukiwa tayari umeshaanza.

Zipo sababu zilizonivutia, mojawapo ikiwa ni hatua ya Mbunge wa Busega, Raphael Chegeni, kuuliza swali la nyongeza bungeni wiki iliyopita, akitaka kujua mkakati wa serikali kuwalipa wakulima hao madeni wanayodai hadi sasa.

Hatua ya Chegeni imenifanya nijue kwamba kumbe suala la kilio cha wakulima hawa linafahamika hata kwa wabunge ambao kimsingi ni wawakilishi wa wananchi, likiwamo kundi hili maskini.

Kwamba hatua hiyo ya kuhoji mkakati uliopo, kumemwonyesha Muungwana ukweli kuwa bado wapo wawakilishi wa wananchi ambao wanaumia.

Wanaumia kwa jinsi wakulima wanavyohangaikia malipo yao hadi sasa, huku wakipigwa danadana na kampuni zilizochukua pamba yao kutoka kwenye maghala ya Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS).

Wakulima hawa wamepaza kilio chao kwa muda mrefu kwa viongozi wao wakiwamo wakuu wa mikoa na wilaya wenye jukumu la moja kwa moja kushughulikia changamoto za wananchi katika maeneo yao ili walipwe, bila mafanikio.

Na ndiyo maana Muungwana anaungana na Chegeni kuwasemea wakulima hawa kwani ndiyo hasa kazi ya mwakilishi wa wananchi, na kwa hiyo hapaswi kukaa kimya, ila kuendelea kusema hadi pale wakapolipwa fedha zao.

Kingine kilichonivutia ni takwimu zilizotolewa na serikali kupitia kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, zilizobainisha kwamba hadi sasa tayari serikali imeshalipa Sh. bilioni 417 kwa wakulima wa zao hilo nchi nzima.

Aidha, Bashe akakiri hilo la baadhi ya wakulima wa pamba ambao hawajalipwa fedha zao kiasi cha Sh. bilioni 50!

Kimsingi, kiasi hicho cha fedha wanachodai wakulima hawa ni kikubwa kwao na kwamba iwapo zingelipwa mapema yumkini zingechangia tija na maendeleo yao kwa ujumla.

Wengi wa wakulima hawa ni wale wadogo wadogo ambao kwao pamba ni chanzo kikubwa cha mapato ya kujenga ustawi wao wa kiuchumi, kijamii, kitamaduni na hata kisiasa wakati mwingine.

**Kimsingi, kiasi hicho cha fedha wanachodai wakulima hawa ni kikubwa kwao na kwamba iwapo zingelipwa mapema yumkini zingechangia tija na maendeleo yao kwa ujumla.**

Muungwana ana taarifa kwa mfano wa baadhi ya AMCOS katika Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, kudai hadi sasa mamilioni ya fedha kama ilivyo katika maeneo mengine.

Kwamba kuna AMCOS, zinadai Sh. milioni 60, Sh. milioni 100 na zingine zaidi ya Sh. milioni 100 kutoka kwa kampuni za ununuzi.

Na kwa bahati mbaya ziko kampuni za ununuzi ambazo hazijapeleka fedha kwenye AMCOS kutoka mwezi Agosti hadi leo hii Novemba, na kila zinapoulizwa lini zitapeleka fedha za wakulima, zimekuwa na majibu ya kupiga chenga.

Hayo ni pamoja na kuwa zimepeleka mahesabu ya kilo zilizokusanya kutoka AMCOS benki, hivyo zinasubiri sasa zipewe fedha na benki za kuja kuwalipa wakulima na lugha zingine ambazo zinachosha.

Kuna taarifa vilevile kutoka kwa viongozi wa AMCOS kwamba baadhi ya kampuni za ununuzi wa zao hilo sasa hazipokei tena hata simu za wenyeviti wa vyama vya ushirika wanaoulizia fedha za wakulima na hivyo kuwaacha wakulima wasijue la kufanya.

Kwa wanaojua maisha ya vijijini, mzunguko wa Sh. milioni 60 ama 100 zinazodaiwa na AMCOS kutoka kwa wanunuzi, una maana gani kwa maendeleo ya wanakijiji na kijiji kwa ujumla wake.


Wakati msimu wa kilimo umeshaanza, tayari mbegu za pamba zimeshapelekwa vijijini katika baadhi ya maeneo na mkulima anatakiwa anunue mbegu hizi kwa fedha taslimu na si vinginevyo.

Sasa mkulima huyu anayedai fedha zake, lakini anatakiwa anunue mbegu na mahitaji mengine ya kilimo kama mbolea kwa fedha taslimu, afanyaje?

Ni rai ya Muungwana kwa serikali ichukue hatua stahiki ili wakulima wa pamba wanaodai walipwe na hivyo kuwezesha ustawi wao na tija katika kilimo chao.

Distributed via ippmedia

## BARUA / MJADALA




# *Naomba msaada wa JPM*

***Mhariri habari,***

*NINAOMBA nafasi kwenye gazeti lako katika ukurasa wa barua kwa Mhariri, ili niweze kueleza tatizo linalonikabili na hatimaye niweze kupata msaada kutoka kwa Rais wetu mpendwa.*

*Mimi Atupele Mtafya mkazi wa Igurusi, mkoani Mbeya, namwomba Rais mtetezi wa wanyonge, Dk. John Magufuli, aingilie kati anisaidie kupata eneo langu la ekari 30 baada ya Jeshi la Polisi Wilaya ya Vwawa, mkoani Songwe kunipiga danadana.*

*Nilipeleka malalamiko kwa mkuu wa kituo hicho tangu Mei 6, mwaka huu na malalamiko yangu yakaandikishwa katika kituo hicho, halafu nikaambiwa nirejee siku inayofuata yaani Mei 7, kituoni hapo kwa ajili ya hatua zaidi. Nilipofika mapokezi nikaambiwa malalamiko yangu yamefutwa, hivyo niwaone wakubwa kwa ufafanuzi zaidi.*

*Nikahangaika kuingia ofisi ya mkuu wa kituo hicho, lakini sikufanikiwa kumuona na sikupata msaada wala ufafanuzi wowote hadi sasa.*

*Nilifungua malalamiko dhidi ya watu wanne akiwamo Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Isangu ambao wameingia bila idhini katika shamba letu la urithi na kuvunja nyumba kisha kung'oa bati, milango na kuvihamisha sehemu nyingine pamoja na makochi.*

*Pia wameharibu kwa kukata miti ya miembe, na mingine ya asili na kisha wanalima eneo hilo lililo ndani ya ekari 30 za urithi unaonihusu mimi na dada zangu wawili Tupokigwe na Tusubisiwe.*

*Eneo hilo baba yangu mzazi Lwitiko Mtafya alimnunulia mama Sikomene Msokwa na kumjengea nyumba, baada ya kufariki mimi nilikuwa msimamizi wa mirathi na ikaamriwa kuwa ni letu mimi na dada zangu lakini ndugu zetu watano ambao tumezaliwa tumbo moja wanaingia kwa nguvu na kuharibu mali kwa madai kuwa nao ni wahusika.*

*Kupitia barua hii ndiyo maana sasa naomba msaada wa Rais Magufuli ili haki yangu na dada zangu tuliorithishwa shamba hilo tulitumie kwa nafasi na uhuru bila ya bughuda tunayopata sasa.*

***Atupele Mtafya mkazi wa Igurusi!***



Ajira kama hii inapaswa kupigwa vita na jamii yote. **PICHA: MTANDAO**

# Kwa watoto iwe ni elimu kwanza, ajira baadaye

**Na Sabato Kasika**

MAADHIMISHO ya Siku ya Kupinga Ajira kwa Watoto Duniani ya mwaka huu wa 2019, yalikuwa na ujumbe usemao: "Watoto wasifanye kazi mashambani, bali wafanyie kazi ndoto zao."

Ujumbe huo ulilenga kuiasa jamii kuwaacha watoto wakue, na kukuza ndoto zao kupitia njia mbalimbali ikiwamo elimu, badala ya kuwaingiza katika ajira na kujikuta wakikosa haki ya kupata elimu.

Siku hii huadhimishwa Juni 12 ya kila mwaka, na katika maadhimisho ya mwaka huu ilielezwa kuwa kuna jumla ya watoto milioni 150 wanaofanyishwa kazi duniani kote na hawapati nafasi ya kuhudhuria shule.

Ingawa ni miezi kadhaa imepita tangu maadhimisho hayo yafanyike, bado kuna haja ya kuendelea kujadili tatizo la ajira kwa watoto, kwa kuzingatia kwamba bado lipo katika jamii.

Katika maadhimisho ya mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Anna Henga alisema wengi wa watoto wanatumikishwa katika sekta mbalimbali.

Mkurugenzi huyo alikaririwa na vyombo vya habari akisema, kuna aina nyingi za ajira kwa watoto zikiwamo za kufanya kazi shambani, viwandani na kutumikishwa katika vita na kulazimishwa kuwa ombaomba.

Watoto wanaofanya kazi ya kuomba fedha mitaani hasa maeneo ya mijini, kama katika Jiji la Dar es Salaam, wanafanya hivyo kwa maslahi ya watu wengine wakiwamo hata wazazi wao.

"Wengine huhusishwa katika aina mbaya zaidi za ajira kwa watoto kama kufanyishwa biashara za ngono, kushirikishwa katika biashara ya dawa za kulevya na kazi nyingine zisizofaa," anasema Henga.

Anasema hapa nchini, ajira nyingi za watoto ziko katika mifumo ya wafanyakazi wa ndani, wafanyakazi shambani, ombaomba na wanaofanyishwa biashara za ngono.

Kwa mujibu wa Henga, ajira hizo zinaathiri watoto kwa vile wanashindwa kukua kiakili pia wanashindwa kuhudhuria masomo na kwamba Sheria ya Mtoto, Namba 21 ya mwaka 2009, inatoa maana ya mtoto kuwa ni mtu yeyote mwenye umri wa miaka chini ya 18.

Aidha, inatoa ufafanuzi kuwa ukatili kwa watoto unajumuisha ajira kwao ikiwamo ajira zinazowanyonya, hivyo ni muhimu zikomeshwe.

Pamoja na yote hayo, mkazo wa mkurugenzi huyo ni kutaka watoto waachwe watimize ndoto zao kupitia elimu na wawe na muda wa kucheza na kushiriki na wenzao kwa ajili ya ukuaji wao.

Kwa maana hiyo, jamii ina wajibu wa kushiriki kikamilifu katika kukomesha ajira kwa watoto, ambazo zinachangia kuwafanya wakose haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Kimsingi siyo jambo jema jamii ikiacha watoto wakiajiriwa kama wafanyakazi wa ndani, shambani, viwandani au kufanyishwa biashara za ngono na kukosa elimu, ambayo ni muhimu katika maisha.

Mojawapo ya sababu ambazo zimekuwa zikitajwa kuchangia hali hiyo ni mifarakano katika ndoa na kwamba ikikoma inaweza kuokoa watoto katika janga hilo, ambalo halijapatiwa ufumbuzi.

Mifarakano hiyo ya ndoa ikikoma, inawezekana wazazi wakawa na nafasi nzuri ya kulea na kuwalinda watoto wao, ili watimize ndoto, kwani itakuwa ni rahisi kushirikiana katika kuwatimizia mahitaji na watahudhuria masomo shuleni.


Kwa maeneo ya mijini hasa Dar es Salaam, kama nilivyosema, ninaamini wakazi wake watakuwa wameshuhudia watoto wadogo wenye umri wa kwenda shule wakiwa mitaani wakiomba fedha kwa wapita njia.

Siyo wapita njia tu bali na madereva wa magari ndio, ambao wamekuwa wakizongwa na ombaomba ili angalau wapate chochote kutoka kwao, lakini ajira za aina hii zinatakiwa kukomeshwa.

Njia mojawapo ya kuzikomesha ni ushirikiano wa jamii, siyo kuiachia serikali tu na taasisi zisizo za kiserikali, hivyo jamii isikwepe wajibu kwenye jambo hili, ambalo linaharibu maisha ya baadaye ya watoto.

Hivyo jamii ishtuke na kuchukua hatua kwa kuzingatia malezi bora ili kusaidia kupunguza kama siyo kumaliza kabisa tatizo la kuwapo kwa ajira za watoto, ambazo zimeshamiri duniani.

Ajira au kazi hazitakiwi kuathiri mahudhurio ya mtoto shuleni na haki nyingine ingawa baadhi ya watoto wamekuwa wakijiingiza kwenye ajira na kusababisha wasihudhurie shule, hali inayowafanya wakose haki ya kupata elimu.




HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

# Mnyukano uchaguzi serikali za mitaa

INATOKA UK 2

warejeshwe na washiriki lakini kuna baadhi ya maeneo hawakurejesha fomu.

"Nilichokuwa nikikihitaji haya manyanga ambayo yamefanyika kwa makusudi ya kuwanyima wapinzani fomu. Kuna wagombea wetu fomu zimekataliwa naomba Jafo azungumze na serikali inatoa kauli gani," alisema Nchua.

Naye Mbunge wa Iringa Mjini (Chadema), Peter Msigwa, alisema hata jimboni kwake eneo la Gangilonga wagombea wa chama chake wote hawakurejesha fomu baada ya kukuta ofisi za wasimamizi zimefungwa.

Kutokana na hoja hizo, Spika Ndugai alimpa nafasi Waziri Jafo kutolea ufafanuzi kuwa: "Sisi wote ni Watanzania na inawezekana tunatofautiana kwa ufafanuzi nilioutoa jana (juzi) kuhusu watu wote waliochukua na kurudisha fomu. Sasa watu wote wakacheze, demokrasia uwanjani ikafanye kazi."

Jafo alisema wapinzani wanataka kuhamisha goli na kwamba hana maelezo zaidi kuhusu suala hilo mbali na alichokizungumza jana (juzi).

"Mheshimiwa Spika sina maelezo zaidi ya hayo na kwa kumwogopa Mwenyezi Mungu iko siku wataenda kujibu haki mbele ya Mwenyezi Mungu. Nadhani kwa hekima iliyofanyika... Kama kweli watu wana hofu ya Mungu, walikuwa wanasema watu wamekatwa bado leo wanahamisha goli. Mheshimiwa Spika sina maelezo zaidi," alisema.

**MSIMAMO ACT**

Wakati hoja zikiendelea hivyo, Chama cha ACT Wazalendo Kimetoa msimamo wake na kutangaza masharti saba ili kuwa na uchaguzi huru na haki.

Katika taarifa kwa vyombo vya habari, imeyataja masharti hayo kuwa ni pamoja na kuitishwa kikao cha pamoja cha vyama vyote vya siasa ili kukubaliana namna ya kusonga mbele katika uchaguzi huo.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Kampeni na Uchaguzi Taifa, Joram Bashange, chama hicho kimesema kama hakuna tume huru, hakuna uchaguzi utakaokubalika nchini na kumtaka Jafo awajibike kwa kuharibu uchaguzi huo.

"Waziri Jafo aitishe kikao cha pamoja cha vyama vyote vya siasa ili kukubaliana kuhusu namna ya kusonga mbele kwa utekelezaji wa mapendekezo yetu. Kinyume cha hayo, ACT Wazalendo hatutashiriki uchaguzi huu," alisema Bashange huku akipendekeza mchakato wote wa uchaguzi uanze upya.

ACT Wazalendo pia imependekeza wasimamizi wa uchaguzi walioharibu mchakato huo wawajibishwe ili kukomesha tabia hiyo na pia ziundwe kanuni mpya za uchaguzi kwa maridhiano na makubaliano na wadau wote hususani vyama vya siasa.

Sambamba na hilo, ACT Wazalendo imemwomba aikirie upya kuiondoa Tamiseni chini ya ofisi yake na kuirejesha Ofisi ya Waziri Mkuu ili taasisi ya urais iepukane na kashfa za uharibifu wa demokrasia nchini.

" Bila tume huru ya uchaguzi pasiwe na uchaguzi wowote nchini. Viongozi wa kitaifa wa vyama watoke na tamko la pamoja kutaka tume huru ya uchaguzi.

"Tunaendelea kusisitiza msimamo wetu wa kujitoa kwenye uchaguzi na kuwataka wanachama wetu nchi nzima kuendelea kutekeleza agizo la chama la kuandika barua za kujitoa kwenye uchaguzi," ilieleza taarifa hiyo.

**WANAHARAKATI WANENA**

Taasisi isiyo ya kiserikali ya Aliance for Development Organization (ADO), imeelezea kusitikishwa kwake na hatua ya vyama vya upinzani kujitoa katika uchaguzi huo na kusema uamuzi huo umekiuka Katiba na demokrasia.

ADO imesema viongozi wa vyama vya upinzani wanapaswa kutafakari upya kwa wagombea wao kufuata kanuni na taratibu na uchaguzi wa serikali za mtaa.

Mwanaharakati wa Mambo ya Kijamii kutoka ADO, Mackdeo Shilinde, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa mambo yanayotakiwa yafanyike na chama pamoja na wagombea yafanyike kwa haki na kwa amani kwa kuwa kujitoa ni kuwanyima haki wananchi kuchagua viongozi wanaowataka.

"Viongozi wa vyama vya upinzani warudi tena wakatafakari na wagombea wao wakawashirikishe waseme je, ni kweli wagombea wao hawataki kushiriki kwenye uchaguzi wa serikali za mtaa? Lakini pia vyama vya upinzani vifuate taratibu katika kufikia uamuzi wao," alisema.

Naye Ally mwinyi kutoka taasisi hiyo, alisema wagombea wa vyama vya upinzani wanaojiondoa katika uchaguzi wa serikali za mtaa wanadhoofisha afya ya demokrasia na kuwanyima wananchi demokrasia.

"Jambo hili la kujitoa kwenye uchaguzi wa serikali za mtaa si jambo zuri kwa afya ya demokrasia na ni kuwanyima wananchi demokrasia ndani ya demokrasia," alisema.

**UPDP WAJITOA**

Mwenyekiti wa Chama cha UPDP, Fahmi Dovutwa, ameibuka na kutangaza kutoshiriki uchaguzi huo, hivyo kuungana na Chaumma, NCCR Mageuzi, ACT Wazalendo, Chadema na NCCR-Mageuzi.

**OFISI YACHOMWA MOTO**

Siku moja baada ya Ofisi ya Kata ya Soweto, Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro kuchomwa moto, watu wasiojulikana wamechoma moto wa ofisi ya kijiji cha Mlali wilayani Mvomero.

Moto huo umeteketeza nyaraka mbalimbali ikiwamo samani za viti na meza.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo na kwamba watu watatu akiwamo Diwani wa Mlali, Frank Mwananjinje, wanashikiliwa na polisi.

Tukio hilo lililotokea usiku wa kuamkia jana majira ya saa 9 usiku.

Kabla ya tukio hilo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mlali, ambaye pia ni msimamizi wa uchaguzi katika eneo hilo, Anusiata Mpina, alisema hivi karibuni alipokea vitisho kutoka kwa mmoja wa wagombea wa uchaguzi wa serikali za mitaa akimtuhumu kutotenda haki katika mchakato wa uchaguzi.

Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Morogoro ilifika jana katika eneo hilo na kushuhudia uharibifu uliojitokeza katika eneo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, alisema kilichofanyika ni uvunjifu wa amani na kwamba hawatakubali kuvumilia hali hiyo kuagiza polisi kuwasaka watu wote waliohusika na tukio hilo na kuchukuliwa hatua kali.

*Imeandikwa na Gwamaka Alipipi (Dodoma), Mary Geofrey na Romana Malya (Dar) na Idda Mushi, MOROGORO.*

Distributed via ippmedia



Wasamaria wema wakisaidia kusukuma gari lililozima barabarani katika eneo la njia panda Kawe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JKCI yaweka mshipa bandia kwenye moyo

INATOKA UK 2

huu, wamefanya upasuaji wa aina hiyo kwa wagonjwa watatu. Alisema wawili walifanyiwa upasuaji katika kambi maalum ya matibabu ya moyo ya wataalamu kutoka Italia na Ujerumani na huyu wa sasa amefanyiwa na madaktari wazawa wa taasisi hiyo.

Neema Amani, mama wa mtoto aliyefanyiwa upasuaji huo, alishukuru kwa huduma ambayo mtoto wake alipatiwa na kuwaomba wazazi wengine ambao wataona watoto wao wana matatizo ya afya, wasikae nao nyumbani wawapeleke hospitalini kwa ya matibabu.

Alisema Septemba, mwaka huu, alipewa rufani kwenda kutibiwa JKCI kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kinondoni ya Mwananyamala baada ya kugundulika kuwa na tatizo la moyo.

Kwa mujibu wa mama huyo, mtoto alikuwa na shida ya kubanwa na kifua, kukohoa na kutokwa na jasho jingi hasa wakati wa kunyonya.

"Naishukuru sana taasisi hii kwani mwanangu hana bima ya afya na sikuwa na pesa ya kulipia matibabu ya moyo. Lakini mwanangu amepatiwa matibabu na sasa anaendelea vizuri na ameruhusiwa kutoka katika chumba cha uangalizi maalum", alisema.

JKCI imekuwa ikifanya kambi maalum za matibabu ya moyo kwa kushirikiana na wataalamu kutoka nje ya nchi na miongoni mwa manufaa yliyopatikana katika kambi hizo ni kubadilishana ujuzi wa kazi na mafunzo ambayo yamewasaidia wataalamu wa taasisi hiyo kupata elimu na utaalamu wa kisasa na wa hali ya juu.

## Mfumo ununuzi kumaliza rushwa

INATOKA UK 2

mitano.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, serikali itapunguza mzigo unaotokana na matumizi yasiyo na tija yatokanayo na mfumo wa sasa.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), Mhandisi Leonard Kapongo, alisema taasisi 200 zimeshaanza kutumia mfumo huo na kuwasilisha mipango yao ya mwaka yenye jumla ya zabuni 11,343 zenye thamani ya takribani Sh. trilioni 11.3.

Ofisa huyo alizitaka taasisi ambazo bado hazijaunganishwa katika mfumo wa Taneps kuwaruhusu na kuwagharamia watumishi wa ununuzi wa Tehama kuhudhuria mafunzo maalum ya namna ya kutumia mfumo huo yanayotolewa na mamlaka hiyo.

## Mbaroni kwa kunaswa na meno ya tembo

INATOKA UK 3

Kazi cha Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Kikosi dhidi ya Ujangili (KDU) Kanda ya Kaskazini na kikosi cha kupambana na ujangili Kanda ya Ziwa.

Alisema kwa pamoja wanaendelea na operesheni Loliondo wilayani Ngorongoro na watuhumiwa hao walikamatwa Novemba 10 mwaka huu, majira ya saa 8:00 asubuhi katika kijiji cha Oleng'usa, Kata ya Oloipiri ndani ya pori Tengefu la Loliondo.

Alisema watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani wakati wowote kujibu tuhuma zinazowakabili.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Tanapa, NCAA, KDU, kikosi kazi cha kupambana na ujangili Kanda ya Ziwa, walikamata bunduki mbili za kivita zikiwa na risasi 15.

Bunduki hizo zilizokamatwa ni aina ya AK 47 yenye namba 174364 ikiwa na risasi sita ndani ya magazine na G3 yenye namba A36011858 ikiwa na risasi tisa. Bunduki zote hizo zilikamatwa karibu na mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Naani, Tarafa ya Loliondo.

Kamanda Shana alisema bunduki hizo zilipatikana baada ya majibizano ya risasi baina ya kikosi kazi hicho na majangili ka walipoona mashambulizi yamekuwa makali, majangili hao yalikimbilia nchini Kenya na kuteleza silaha hizo.

HABARI KITAIFA

## Wanaokwamisha uwekezaji sasa kupelekwa kwa JPM

**Na Gideon Mwakanosya, RUVUMA**

UMOJA wa Vijana wa CCM (UVCCM), mkoani Ruvuma unatarajia kumpelekea Rais John Magufuli majina ya watumishi wanaodaiwa kukwamisha shughuli za maendeleo na uwekezaji kutokana na kukithiri kwa vitendo vya rushwa mkoani humo, mapema mwezi Desemba, mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Umoja huo wa Mkoa wa Ruvuma, Raymond Mhenga, wakati alipokuwa akizungumza kwenye mahafali ya 10 ya Chuo cha Ufundi cha Top One Inn (TOP ONE INN VTC), kilichopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma.

Alidai Mkoa wa Ruvuma upo nyuma kimaendeleo kwa madai ya baadhi ya watumishi kuwa kikwazo cha kuweka urasimu na kuwakatisha tamaa watu wenye nia ya kutaka kuwekeza mkoani humo kwa sababu ya kutaka kupewa rushwa.

Alidai kuwa kuna watu wengi ambao wameonyesha nia ya kutaka kuwekeza kwa ajili ya kutaka kukomboa uchumi wa mkoa wa Ruvuma, lakini kutokana na tabia ya baadhi ya watumishi wasiokuwa waadilifu, wanakwamisha jitihada za Rais Magufuli za kulifikisha taifa katika uchumi wa kati kutokana na tabia ya kutaka rushwa.

"Nimesema kwamba nipo tayari kumpelekea Rais John Magufuli orodha ya baadhi ya watumishi wa serikali hususan wa Manispaa ya Songea ambao wanawakwamisha wawekezaji na jitihada za mkuu wa nchi za kulifikisha taifa kwenye uchumi wa kati kwa sababu ya kutaka rushwa," alisema Mhenga.

Hali hiyo imejitokeza baada ya Mkurugenzi wa Chuo hicho, Pascal Msigwa, kumwelezea changamoto ya ufinyu wa eneo la chuo hicho kwa madai kwamba anashindwa kupanua huduma zake kutokana na kuyumbishwa na baadhi ya watumishi na viongozi wa serikali kupata eneo kwa ajili ya kuendeshea shughuli zake.

Msigwa alimwelezea mwenyekiti huyo wa UVCCM, kuwa kuna tabia ya baadhi ya watumishi na viongozi wa serikali kuwathamini wawekezaji wa nje na kuwadharau wa ndani ambao wengine ni wazawa.

**"Nimesema kwamba nipo tayari kumpelekea Rais John Magufuli orodha ya baadhi ya watumishi wa serikali hususan wa Manispaa ya Songea ambao wanawakwamisha wawekezaji na jitihada za mkuu wa nchi za kulifikisha taifa kwenye uchumi wa kati kwa sababu ya kutaka rushwa," alisema Mhenga.**

# Ujenzi meli ya kisasa Ziwa Victoria wafikia asilimia 35

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

UJENZI wa meli mpya ya kisasa Ziwa Victoria umefikia asilimia 35, ambao unatarajia kugharimu Sh. bilioni 86 hadi kukamilika kwake.

Hayo yameelezwa juzi jijini Mwanza na Kaimu Mhandisi Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (Mscl) Mwanza, Abel Gwanafyo, kwa niaba ya ofisa mtendaji mkuu wa huduma hizo.

"Meli hiyo ina uwezo wa tani 400 yakiwamo magari madogo 20 na makubwa matatu na kubeba abiria 1,200, ambayo itakuwa ya kisasa zaidi kuliko meli zingine katika Ziwa Victoria," alisema Gwanafyo.

Akizungumza katika kongamano la wasaa wa marafiki wa habari mkoani Mwanza, Gwanafyo alisema ujenzi huo ulianza mwaka 2018 na unatarajia kukamilika 2021.

Gwanafyo alisema meli hiyo inajengwa na Kampuni ya Ujenzi ya GAS EntecCO Ltd kwa kuungana na Kang Nam Cooperation ya Korea Kusini pamoja na SUMA JKT ya Tanzania.

Aidha, alisema itakuwa na viti vya kisasa zaidi vya kukaa mtu mmoja mmoja kama kwenye ndege, ambayo itafanya safari zake Mwanza kwenda maeneo ya Kemondo, Bukoba, Musoma pamoja na Uganda kupitia Bandari ya Portbell. Pia inaweza kukodiwa na watalii.

Alisema itatumia saa chache kukimbia kutoka Bandari ya Mwanza kwenda bandari zingine kuliko meli ya zamani Mv. Victoria inayofanyiwa ukarabatiwa.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (katikati), mke wa Waziri Mkuu, Mary Majaliwa (kulia) na mke wa Waziri Mkuu mstaafu, Tunu Pinda, wakigawa chakula kwa watoto wenye ulemavu mbalimbali wakiwamo wanaolelewa kwenye kituo cha Buhangija, Shinyanga Mjini juzi, baada ya kukabidhi majengo ya vyumba vinne vya madarasa na vyoo kumi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Ofisa serikalini adaiwa kumfanyia mtoto ukatili

**Na Mwandishi Wetu, Pemba**

OFISA wa Serikali ya Zanzibar Wilaya ya Mkoani (jina linahifadhiwa kwa sasa), anatuhumiwa kumfanyia udhalilishaji mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 13 ambaye ni mwanafunzi wa darasa la sita, katika moja ya shule za wilayani humo Mkoa wa Kusini Pemba.

Jeshi la Polisi limethibitisha kupokea taarifa za tuhuma hizo na kuwa linazifanyia kazi.

Wakizungumza mjini Chakechake, wazazi wa mtoto huyo walisema kuwa, awali mtoto wao walimkuta na Sh. 3,000 na ndipo walipoanza kuingia wasiwasi, kwani hajawahi kumpa kiasi hicho cha fedha.

Walisema walimwita na kumuuliza alipozipata fedha hizo, ingawa hakusema, jambo ambalo liliwasababishia hofu zaidi na kuamua kumpeleka katika Ofisi za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi bandarini Mkoani, ili kumuhoji na kupata ukweli.

Walieleza kuwa, baada ya mtoto kusema hivyo, alichukuliwa na askari mwanamke na kumwangalia, ambapo aliwaambia kuwa sehemu zake za siri za mbele zimetanuka, ndipo walipoamua kwenda Hospitani ya Mkoani kwa ajili ya uchunguzi.

"Tulipofika hospitali tuliambiawa kwanza twende polisi, tukaenda kutoa maelezo na tukarudi tena hospitali, baada ya uchunguzi wa daktari, tulirudi tena Polisi na tukaambiwa hakuingiliwa bali alifanyiwa udhalilishaji kwa kuusugunisha uume wake katika sehemu za siri za mtoto wetu," alisema shangazi wa mtoto.

Alisema baada ya maelezo hayo walitakiwa kurudi, ingawa walikaa muda mrefu bila kupata mrejesho kutoka kituo cha Polisi, jambo ambalo lilianza kuwatia wasiwasi kwa vile kuna mtu alikwenda kuwaambia mtoto wao hakuingiliwa, na mtuhumiwa yuko tayari kuomba msamaha.

"Tulipoona kimya nilikwenda kuulizia kituo cha Polisi Mkoani, nikaambiwa kesi hiyo imefikishwa kituoni Chakechake, hivyo tuendelee kusubiri," alieleza.

Alieleza walipoona kimya kimeendelea, waliamua kumpeleka tena Hospitali ya Chakechake kwa ajili ya uchunguzi zaidi, ambapo majibu ya kituo cha Mkono kwa Mkono ni tofauti na majibu ya Mkoani.

"Tulihisi kuna mchezo hapa unachezwa, kwa nini majibu ya Hospitali ya Chakechake yawe yanafanana na yale ya askari wa kituo cha Zimamoto, lakini majibu ya Hospitali ya Mkoani yawe ni tofauti?

Mwalimu wa mtoto huyo ambaye pia ni msaidizi wa sheria Hidaya Bilali Hassan, huku wakiwa katika harakati za kulishughulikia tatizo hilo, ilikuja kamati ya Baraza la Wawakilishi Mkoani na kutakiwa awaite wazazi wa mtoto huyo, ambapo alimpigia simu shangazi yake na kwenda kuelezea tukio hilo.

"Baada ya maelezo aliyoyatoa hapo, siku ya pili alipigiwa simu na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed Suleiman Abdalla, twende kwa ajili ya kutoa maelezo zaidi," alisema mwalimu huyo.

Mama mzazi wa mtoto huyo, aliviomba vyombo vya sheria kuchukua hatua zinazostahiki na kuacha kuangalia aliyetenda udhalilishaji huo ni nani.

"Hata kama ni mkuu kwa vile amefanya kitendo cha kumdhalilisha mtoto anatakiwa ahukumiwe kisheria, kwani tunaona kwamba matendo haya yakiwafika wakubwa yananyamazwa," alisema.

Mtuhumiwa alipopigiwa simu, alikataa kumfanyia mtoto huyo kitendo cha udhalilishaji na kusema ni maneno ya kupangwa tu.

Alisema yeye ni muungwana, hivyo hawezi hata siku mmoja kumfanya mtoto kitendo chochote, na anaamini ni mchezo uliopangwa wenye lengo la kumchafulia jina.

Alisema, mtoto huyo inawezekana ameshapangwa na baadhi ya wazazi wake, kwa lengo la kumshushia hadhi, huku akikanusha kuwa aliwahi kumpa fedha mtoto huyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Hassan Nassir Ali, alisema jeshi hilo limepokea tuhuma hizo, na wanaendelea na upelelezi na kuwa jalada litafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

"Ni kweli tuhuma za mtuhumiwa zimeshafikishwa juu ya meza yetu, lakini kwa sasa hatujamkamata, maana tunakamilisha ushahidi kisha sheria itafutwa," alifafanua.

# Serikali yajiweka kando wanaotelekeza wazazi

BUNGE limeelezwa kuwa serikali haina mpango wa kuleta bungeni sheria ya kuwawajibisha watoto wenye uwezo wanaotelekeza wazazi wao.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Jasmine Tiisekwa.

Katika swali lake, Dk. Tiisekwa alieleza kuwa baadhi ya watoto wakubwa wenye uwezo wameamua kuwatelekeza wazazi wao pasipo kuwapa matunzo wanayostahili.

"Je, serikali ina mpango gani kuwawajibisha watoto waliotelekeza wazazi na kuhakikisha wanatoa matunzo stahiki," alihoji.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji serikali ipo tayari kuanzisha dawati la wazee ili wasikilizwe pindi wanapokuwa na malalamiko ya kutelekezwa na watoto wao.

Akijibu swali hilo, Dk. Ndugulile alisema kwa sasa hakuna mpango huo isipokuwa serikali itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha jamii kutambua jukumu lao la malezi na matunzo kwa wazazi ambao ni hazina na tunu muhimu ya Taifa.

Alisema serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa wazee katika ustawi wa Taifa.

"Tunatambua wazazi walitumia rasilimali walizokuwa nazo kuhakikisha watoto wanapata huduma za matunzo na malezi ili kukua na kufikia ndoto zao, hivyo kutokana na mifumo ya hifadhi ya jamii ya asili, jukumu la kuwalea wazazi au wazee lilikuwa ni la wanafamilia hususani watoto," alisema.

Alibainisha kutokana na kudhoofika kwa mifumo hiyo ya asili mmomonyoko wa maadili na utandawazi, jukumu hilo limekuwa na changamoto nyingi na kusababisha wazazi kutekelezwa.

"Katika kuhakikisha maslahi ya wazee yanalindwa na wanapata haki zao ikiwamo matunzo, serikali iliandaa sera ya wazee mwaka 2003 ambayo inaelekeza jamii kuwajibika kutoa matunzo kwa wazee," alisema.

Alitoa rai kwa watoto na jamii kuhakikisha wazazi wanapatiwa malezi na matunzo yanayostahili.

Kadhalika, Dk. Ndugulile alisema kuwa wazee wanaoona hawapati haki za msingi wafike kwa maofisa ustawi wa jamii ili changamoto zao zifanyiwe kazi.

Aidha, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Suzan Lyimo, alihoji mpango wa serikali wa kupeleka bungeni sera itakayobana watoto wasiotunza wazazi kwa kuwa suala hilo limekuwa changamoto ya muda mrefu.

Dk. Ndugulile akijibu swali hilo, alisema baada ya sera ya afya kukamilika wataangalia namna ya kuja na sheria ya kutambua haki za wazee.

Katika hatua nyingine, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliwaasa wabunge kuhakikisha wanakula na kuweka badala ya kutegemea watoto wao kuwatunza.

# Mbunge ataka tamko tume ajali Moro

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Viti Maalum (Chadema), Devotha Minja, amehoji sababu za kutotolewa tamko lolote kuhusu tume iliyoundwa kuchunguza ajali ya moto mkoani Morogoro.

Akiuliza maswali ya nyongeza jana bungeni, Minja alisema wakati wa mazishi ya watu waliofariki kwa ajali hiyo, Waziri Mkuu aliagiza kuundwa kwa tume hiyo, lakini hadi sasa ofisi yake haijatoa tamko lolote.

"Waziri Mkuu wakati wa mazishi pale Msamvu aliagiza kuundwa tume ya kuchunguza ajali ya msamvu. Je, ni kwanini mpaka sasa Ofisi ya Waziri Mkuu haijatoa tamko lolote juu ya tume iliyoundwa kuchunguza ajali ya moto Msamvu?"Alihoji.

Alisema ajali za moto wa malori ya mafuta zimeendelea kugharimu maisha ya Watanzania kwa kusababisha vifo na vilema vya kudumu.

Mbunge huyo aliliambia Bunge kuwa tukio la Agosti 10 mwaka huu, katika eneo hilo lilisababisha vifo vya watu zaidi ya 100, lakini umbali wa ofisi za Zimamoto hadi Msamvu haufiki kilomita moja.

"Je, serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwalipa fidia wapendwa waliopoteza maisha yao pale, kwa sababu fire (Zimamoto) ilifika pale kuzima moto wakati watu wameteketea na kuwa majivu na kuni," alihoji. Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema kwa kuwa kamati iliyoundwa ilikuwa ya Waziri Mkuu hana mamlaka ya kuitolea kauli.

"Nina hakika Waziri Mkuu kupitia ofisi yake kuna utaratibu ambao umewekwa wa kuweza kuitolea taarifa pale ambapo ataona inafaa kwa utaratibu unaofaa, Mbunge avute subira wakati serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hili," alisema.

Masauni alisema anaimani na kamati hiyo kuwa inafanya kazi vizuri na lengo la Waziri Mkuu ni kuhakikisha taarifa ya ripoti hiyo inatoa mapendekezo ambayo hatua zitachukuliwa, lakini kuhakikisha matukio ya aina hiyo hayajitokezi siku za mbele.

Aidha, katika swali la nyongeza la Mbunge wa Vunjo (NCCR-Mageuzi), James Mbatia, alisema asilimia 96 ya majanga yote yanasababishwa na binadamu.

"Serikali haioni kuna haja ya kuwa na mfumo rasmi wa kujilinda, kujikinga na kujiokoa na majanga hapa nchini?"Alihoji.

Masauni akijibu swali hilo, alisema ushauri uliotolewa na Mbunge huyo mamlaka husika zimesikia na serikali italichukua na kutafakari kama kuna haja ya kufanya hivyo.

Katika swali la msingi, Minja alihoji serikali ina mpango gani wa kukiwezesha kikosi cha Zimamoto kufanya kazi ipasavyo kwenye miji na nje ya miji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Masauni alisema seikali kupitia jeshi hilo inashirikiana na Shirika la Nyumbu (TATC) katika utengenezaji wa magari mapya ya kuzima moto na uokoaji.

Aidha, alisema Zimamoto imesaini hati ya makubaliano na kampuni ya ROM Solution Ltd ili kupata mkopo wenye masharti nafuu utakaowezesha kupata vitendea kazi kwa nchi nzima.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akizungumza na wakazi wa Nzunguni, jijini Dodoma jana, kuhusiana na mgogoro wa ardhi kati yao na halmashauri ya Jiji hilo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Rita kutoa vyeti mtandaoni

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Augutine Mahiga, amesema Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) utaanza kutoa kwa njia ya mtandao huduma ya usajili wa mpango wa kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa Watanzania wenye umri zaidi ya miaka mitano.


Dk. Mahiga alitoa kauli hiyo jana, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq, ambaye alisema serikali imeanza kampeni ya kusajili watoto chini ya miaka mitano ili kupata vyeti vya kuzaliwa lakini bado Watanzania wenye zaidi ya umri wa miaka mitano na kuendelea hawana vyeti.

Alihoji serikali imejipangaje kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa Watanzania wenye zaidi ya miaka mitano na kuendelea.

Akijibu swali hilo, Waziri Mahiga alisema Rita inaanzisha utaratibu huo ili kuwafikia wananchi wengi kwa urahisi.

"Mwananchi atafanya maombi ya cheti cha kuzaliwa kupitia mtandao na baadaye kufika ofisi ya Rita iliyo karibu kwa ajili ya kukamilisha taratibu za usajili," alisema.

Hata hivyo, alisema Rita imejipanga kusajili na kutoa vyeti kwa wananchi 15,917,602 ifikapo mwaka 2025 na hivyo idadi ya wasio na vyeti itapungua hadi kufikia 21,508,277 ambao ni chini ya asilimia 50 ya wote wenye umri zaidi ya miaka mitano.




Waziri huyo aliwataka wananchi ambao hawana vyeti vya kuzaliwa kufika kwenye ofisi za Rita kwa ajili ya kusajiliwa na kupewa vyeti hivyo.

Aliwaomba wabunge kushirikiana na serikali kuwaelimisha wananchi katika majimbo yao kuhusu umuhimu wa kusajili matukio muhimu ya binadamu ikiwamo vyeti hivyo.

"Serikali kupitia Rita imekuwa ikitekeleza mkakati wa usajili wa matukio muhimu na takwimu ili kuboresha hali ya usajili nchini," alisema.

Alitaja mikakati hiyo ni kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wote waliopo kwenye mfumo rasmi wa kufanya kampeni za uhamasishaji kwa kuwafuata wananchi katika maeneo yao ya makazi.

# Atishia kushusha vyeo watumishi

**Na Allan Isack, MANYARA**

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, ametishia kuwashusha vyeo wakuu wa idara wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati endapo wataendelea na tabia yao ya usimamizi mbaya wa miradi ya maendeleo.

Mnyeti alisema kama changamoto hiyo, ya usimamizi wa miradi ya maendeleo itaendelea basi ataagiza nafasi za wakuu wa idara katika halmashauri hiyo, zichukuliwe na maofisa watendaji wa kata.

Mnyeti alitoa onyo hilo, juzi baada ya kukataa kuzindua mradi wa vyumba vinne vya madarasa katika Sekondari Maganjwa Kata ya Dabil.

Alisema tatizo kubwa aliloliona ni usimamizi mbovu wa fedha zilizoletwa na serikali, licha ya wananchi kuonyesha moyo wa kizalendo wa kujitolea mawe na matofali ili kukamilisha ujenzi huo.

"Wakuu wa idara badilikeni, acheni kukaa maofisini nendeni kwa wananchi nitawachukulia hatua kwani nitaagiza mshushwe vyeo endapo mtaendelea na tabia hii ya kushindwa kusimamia kazi," alisema Mnyeti.

"Hapa gharama zilizotumika hazijanifurahisha, mimi siyo Mkuu wa Wilaya ya Babati bali ni Mkuu wa Mkoa wa Manyara nimetembea wilaya zote za mkoa huu, kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa mengi, Mkuu wa Wilaya ya Babati nadiriki kusema hapa kuna uchakachuaji umefanyika," alisema.

Mnyeti alisema atawatuma wakaguzi kutoka ngazi ya mkoani kukagua ujenzi huo, ili ukweli ufahamike kuwa kazi imegharimu fedha kiasi gani.

Alisema endapo viongozi watakaa kimya na kufumbia macho masuala ya uchakachuaji kwenye miradi, wananchi hawatakuwa na moyo wa kuchangia maendeleo.

Aliwataka wananchi wa eneo hilo, kuwa watulivu na wafanye shughuli zao na waendelee kuchangia mradi huo, wakati serikali ikitengeneza utaratibu wa kuuchunguza mradi huo.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema serikali imetoa Sh. milioni 50, kukamilisha ujenzi huo, huku akisisitiza kuwapo kwa matumizi mazuri ya fedha.

"Fedha zikibaki anzisheni mradi mwingine huwezi kusema kwa sababu zilipangwa kwa ajili ya ujenzi huu basi fedha zote Sh. milioni 50, ziishie hapa mradi ni mdogo na pesa ni nyingi kamilisha mradi huu halafu fedha zinazobaki anzisha mradi mwingine," alisema Mnyeti.

Awali, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Dabil, Raphael Baghayo, alisema shule hiyo ilianzishwa Februari 2019, kutokana na wanafunzi wa eneo hilo kutembea umbali mrefu hadi Shule ya Dabil.

Baghayo alisema jumla ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya mradi huo ni Sh. milioni 53 kutoka Serikali Kuu na nyingine 3,000,000 zimetokana na mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Babati.

# Tanesco yaahidi kasi mpya vijijini

**Na Allan Isack, MIRERANI**

SHIRIKA la Umeme nchini (Tanesco), limeendelea na kusambaza umeme kwa wateja wapya ili huduma hiyo iwafikie wananchi wanaoishi maeneo ya vijijini kwa wakati na kutimiza azma ya serikali ya kuwasha umeme Tanzania nzima.

Akizungumza na Nipashe wakati wa kuwapokea wafanyakazi wapya 19, Meneja wa Tanesco Wilaya ya Mirerani, Zakaria Masatu, alisema kazi hiyo inafanywa kwa kasi na kwa jitihada zote.

Masatu alisema wilaya hiyo ya Kitanesco ya Mirerani imefikisha nishati kwenye nyumba mbalimbali za Mirerani kwa gharama ya Sh. 27,000 kwa kila mwananchi aliyekuwa na uhitaji wa huduma hiyo.

Alitaja baadhi ya maeneo mapya yaliyofikishiwa umeme kuwa ni Naepo Kata ya Naisinyai, Sekondari ya Kata ya Shambarai na Shule ya Blue Tanzanite iliyopo Kata ya Endiamtu.

Alitoa wito kwa watu wanaohitaji kufungiwa umeme nyumbani kwao, kupeleka maombi ofisini Tanesco ili kazi ifanyike baada ya kukamilisha kanuni na taratibu.

Aidha, aliwakaribisha wafanyakazi 19 waliojiunga na shirika hilo, na aliahidi kuwapa ushirikiano katika utendaji kazi wao.

"Tumechagua kufanya kazi kwenye shirika letu, hivyo hatuna budi kutimiza wajibu wetu ipasavyo kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu," alisema Masatu.

Meneja wa Tanesco wa Mkoa wa Arusha, Mhandisi Herin Mhina, aliwataka wafanyakazi hao, kufanya kazi kwa bidii, kuwa na mshikamano na upendo ili kufikia malengo waliyojiwekea.

"Ili tuweze kufanikiwa zaidi tujitahidi kufuata hayo ili kuepuka lawama na malalamiko yasiyo ya msingi kutoka kwa wananchi angalau yapungue kama siyo kumalizika kabisa," alisema Mhina.

Aliwaambia kuwa sasa malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu utoaji wa huduma kwenye shirika hilo, yamepungua na hiyo imetokana na uwajibikaji makini wa wafanyakazi.

Mkuu wa Kituo cha Polisi Mirerani, Mratibu Msaidizi wa Polisi (ASP), Christina Mkonongo, aliwapongeza wafanyakazi wa Tanesco kwa namna wanavyowatumikia wananchi kwenye sekta hiyo ya nishati.

"Shughuli zetu za ulinzi na usalama wa raia na mali zao, tunazifanya kwa wepesi kwani maeneo mengi yana umeme, hivyo imetusaidia kuwapo kwa usalama na kuimarika ulinzi wa raia na mali," alisema Mkonongo.


Distributed via ippmedia

Mjasiriamali Tausi Swalehe akiwafundisha kinamama wa Kimaasai jinsi ya kutengeneza batiki ili nao waweze kujiajiri katika Kata ya Engalenaibo, wilayani Longido, mkoani Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Chama chaahidi kujenga ofisi 40

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

CHAMA cha Walimu (CWT), kinatarajia kukamilisha ujenzi wa ofisi za chama hicho, kwenye wilaya 40, lengo likiwa kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa walimu ambao ni wanachama wake.

Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, aliyasema hayo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Walimu yaliyofanyika wilayani Simanjiro mkoani Manyara.

Alisema hadi kufikia Aprili mwakani, ofisi 40, zitakuwa zimejengwa ikiwamo ya Simanjiro ili kupunguza gharama za kupanga ofisi.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, alisema kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kimepanda wilayani humo kutokana na utendaji kazi mzuri wa walimu.

Kiwango hicho kwa shule za msingi mwaka 2017 kilikuwa asilimia 49.96 na mwaka jana kimefikia asilimia 69.01 kwa mujibu wa maelezo yake.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, alisema kwa kipindi cha miaka mitatu wilayani humo, wameanzisha shule mbili za sekondari za kidato cha tano na sita.


"Tunatarajia kuanzisha shule nyingine ya tatu ya kidato cha tano kwenye Tarafa ya Moipo pia tumeanzisha Chuo cha Veta kilichopo Emboreet kupitia ufadhili wa mdau wa maendeleo Peter Toima," alisema Myenzi.

Mwanachama wa heshima wa chama hicho, Peter Toima, alisema kupitia Shirika lake lisilo la kiserikali la ECLAT Foundation, amejitolea matofali 3,000 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya CWT Simanjiro.

Toima ambaye kitaaluma ni mwalimu alisema ni mdau wa elimu ndiyo sababu anashirikiana na serikali kuunga mkono ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule mbalimbali wilayani humo.

Katibu wa chama hicho Wilaya ya Simanjiro, Nazama Tarimo, alisema Simanjiro ina walimu 892 kati ya hao 622 ni wa shule za msingi na 270 ni wa sekondari. Tarimo alisema katika awamu ya tano serikali imewapandisha madaraja walimu 249 wakati matarajio yao yalikuwa ni walimu 355.

Aidha, walimu 222 tayari wamebadilishiwa mishahara tangu Oktoba mwaka huu na wengine 106 wanasubiri ili kukamilisha idadi hiyo.





# Warudi nyumbani na taka za uzazi

**Na Paul William, SAME**

WAJAWAZITO wanaojifungua katika Zahanati ya Lugulu wilayani Same, wamedai kuwa tatizo la ukosefu wa maji linawalazamisha kinamama au jamaa zao kubeba ndoo za maji wanayotumia baada ya kujifungua wodini.

Hayo yalibainishwa jana na Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha kata hiyo, Happiness Mhina, wakati wa mafunzo maalum yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Mtandao wa Jinsia- TGNP Mtandao wilayani Same na kwamba kata hiyo ina vijiji viwili vyenye zahanati ya Lugulu na Kanza.

Mhina alisema kuwa, katika zananati ya Lugulu lipo tatizo sugu la maji na wazazi inawalazimu kurudi nyumbani na taka za uzazi endapo ndugu hawajapeleka maji ya kuogeshwa.

Alisema zahanati hiyo inakabiliwa na uhaba wa chumba cha leba hali inayosababisha kujifungulia katika chumba cha kusafishia vidonda pamoja na kuchomea sindano.

Katika Zahanati ya Kanza, mwenyekiti huyo alidai kuwa nayo inakabiliwa na ukosefu wa shimo maalum kwa ajili ya kutupa taka mbichi za uzazi hasa 'nyumba ya mtoto'.

Alisema hali hiyo inawalazimisha kinamama kufungashiwa taka hizo kwenye nguo kwa ajili ya kwenda nazo nyumbani na kuzitupa.

"Katika kata yetu ya Lugulu huduma ya afya ni changamoto sana hasa kwa kinamama wanateseka hakuna shimo la kutupa taka wala maji ya kuoga," anasema Mhina.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kata ya Kalemawe, Betty Malikula, alisema changamoto ni kivuko hali ambayo imekuwa ikiwaumiza wajawazito na wengine kufia njiani wakati wakipelekwa katika zahanati ya Kalemawe.

Betty alisema kuwa, katika kijiji cha Makokani kilichopo katika kata hiyo majisafi ni tatizo na kinamama na wanafunzi kutembea 20 kufuata maji.

Aidha, Ofisa Programu Mwandamizi wa TGNP, Deogratius Temba, alisema kwa kushirikiana na Asasi ya Ongawa wanatekeleza mradi wa uwezeshaji wa wananchi majisafi pamoja na utunzaji wa mazingira.

Aliongeza kuwa, kwa kushirikiana na Ongawa wanatarajia kujenga vyumba maalum katika shule zote kwa ajili ya wanafunzi wa kike kuweza kujisitiri wanapokuwa katika siku zao ili wasikatishe masomo.

# 'Wanaohitimu ufundi waanzishe viwanda'

**Na Paul William, HAI**

ILI kutimiza lengo la kuwa na uchumi wa viwanda, wanafunzi waliohitimu katika vyuo mbalimbali vya elimu ya ufundi, wametakiwa kutumia taaluma waliyoipata kuanzisha viwanda vidogo kwa vikubwa. Lengo likiwa ni kutoa mchango wao kwa maendeleo nchi na kuongeza ajira.

Mwenyekiti wa Umoja wa Machifu Tanzania (UMT), Chifu Frank Marealle, aliyasema hayo katika mahafali ya 25 ya Chuo cha Ufundi Hai, kinachomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Alitoa ushauri huo kwenye hotuba yake iliyosomwa na mjumbe wa UMT Rose Marealle.

Rose alisema katika kuelekea uchumi wa viwanda wahitimu hao wana wajibu mkubwa katika kuonyesha taaluma zao kwa vitendo kwa kuanzisha viwanda vidogo na vikubwa, ili kuchochea upatikanaji wa ajira sanjari na kuchangia pato la taifa kwa ujumla.

"Nyie mnaohitimu leo hapa mnatakiwa kwenda kuunga mkono jitihada za serikali katika kuanzisha viwanda vidogo hata vikubwa kwani kukaa bila kutumia taaluma mlizozisomea ni sawasawa na kupoteza muda," alisema Rose.

Mkuu wa Chuo hicho, Reiner Kammleiter, alisema chuo hicho kimeweza kutoa wahitimu zaidi ya 1,600 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1987 ambapo wengi wameajiriwa sehemu mbalimbali kutokana na taaluma zi izoambatana na vitendo wanavyotoa chuoni hapo.

Alisema licha ya chuo kuwa na vifaa vya kisasa bado idadi ya wanafunzi ni ndogo iki inganishwa na uhitaji kwani wananchi wengi wamejengewa dhana potofu kuwa elimu ya ufundi ni kwa waliofeli elimu ya kawaida darasani.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa chuo ni kuwa elimu wanayoitoa chuoni hapo inamwezesha mhitimu kujiajiri au kuajiriwa sehemu yoyote kutokana na kuwapo na vitendea kazi vya kujifunzia hivyo hupata muda mwingi wa kujifunza kwa vitendo kuliko nadharia.

Deonis Lyimo, mmoja wa wahitimu alisema chuo, kinakabiliwa na ukosefu wa nishati mbadala kwa ajili ya kupikia vyakula pamoja na kutokamilika kwa bweni la wavulana.

Ili kuunga mkono mgeni rasmi alitoa mifuko 100 ya saruji ili kuharakisha ujenzi wake.



Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa Hospitali ya Rufani ya KCMC, Stephen Kolimba (wa pili kushoto), akiteta jambo na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fedrick Shoo (kushoto), nje ya jengo la utawala la hospitali hiyo, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wafugaji walalamika gharama za mitamba

**Na Mary Mosha, MOSHI**

BAADHI ya wafugaji mkoani Kilimanjaro, wameiomba serikali kuwasaidia kupata ng'ombe bora wa maziwa kwa bei nafuu kutoka kwenye mashamba darasa ya serikali.

Lengo likiwa ni kuongeza upatikanaji na unywaji wa maziwa lakini pia nao kujiongezea kipato.

Wakizungumza na Nipashe, Elisa Mkoni mkazi wa Machame wilayani Hai, alisema wamekuwa wakikwamishwa na bei kubwa ya mitamba ya ng'ombe kutoka mashirika na watu binafsi.

Alisema hali hiyo inawakwamisha wananchi wa kipato cha chini ambao wanashindwa kununua na badala yake kuendelea kufuga ng'ombe wa kienyeji wanaotoa maziwa kidogo kwa gharama kubwa.

"Zipo aina mbalimbali za ng'ombe bora wa maziwa yaani 'Friesian, Ayrshire na Jersey' wana uwezo mkubwa wa kutoa maziwa, lakini wanauzwa kwa gharama kubwa. Wanaanzia Sh. milioni 1.6 hadi Sh. milioni 2 katika mashirika yasiyo ya kiserikali na watu binafsi hali ambayo inatufanya tushindwe kumudu kuwahudumia kwa faida katika kujiingizia kipato na kuongeza maziwa katika soko," alisema Moni.

"Tunaiomba serikali kuangalia mashamba darasa ili yaweze kuwasaidia wakulima wa mifugo kwa bei nafuu ili wanayoimudu nao wapate ng'ombe bora wenye tija kwa jamii," alisema Sabasitian Nkini.

Kwa mpande wake mtaalamu wa maziwa kutoka Shirika la Uholanzi SNV, Benovila Balama, alisema licha ya wafugaji kuiomba serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza bei ng'ombe wa maziwa lakini utafiti unaonyesha ng'ombe waliopo mkoani hapa wana uwezo mkubwa wa kutoa maziwa lakini wanakabiliwa na changamoto ya malisho.

Alisema bado wafugaji hawana elimu ya kutosha juu na namna bora ya kuwalisha ng'ombe na mazingira bora ya kuishi ili kuleta tija katika sekta ya maziwa.

"Serikali ya mkoa ihakikishe inatoa elimu kwa wafugaji kuhusu ya utengenezaji wa mabanda bora ya kulishia ng'ombe, lishe sahihi ili waweze kupata maziwa wengi na kujikwamua kiuchumi kwani maziwa ni chakula na pesa," alisema Balama.

Mapema mwanzoni mwa mwezi Oktoba Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alizindua jukwaa la maziwa mkoani hapo, alinukuliwa akiwataka wafugaji kuongeza kufuga ng'ombe bora wa maziwa ili kuongeza tija katika biashara hiyo.

Alisema, ikiwa wataalamu wa mifugo watawaelimisha wafugaji namna ya kufuga kwa tija, na unywaji wa maziwa ulio sahihi kwa afya tatizo la utapia mlo kwa watoto litageuka historia mkoani humo.

"Maziwa ni chakula na pesa nawaagiza wataalamu wa mifugo ofisini kwangu, hakikisheni mnatoa elimu ya kutosha kwa wafugali ili waweze kufuga kwa tija na kuleta mabadiliko katika jamii yetu," alisema Dk. Mghwira.

Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 12, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 15


**Ni elimu sekondari bure kwa wote; si Mahakama itazuia ndoa za utotoni**



Ukurasa 18

**UTAFITI**

Binadamu wa kale nchini Israel walivyohifadhi nyama pangoni



Ukurasa 18

## Kwa nini kupoteza ujauzito bado ni mwiko kuzungumzia?



# Mbeya, shule iliyoanza kwa nyasi yaonyesha inawezekana

Ukurasa 16

# ELIMU KUTOKA POLISI

KAMISHNA wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi (CP) Liberatus Sabas alifanya ziara hivi karibuni mkoani Kigoma, ambako pamoja na mengine alizungumza na Watendaji Kata pamoja na Maofisa Tarafa wa wilaya ya Kasulu.

Yafuatayo ni baadhi ya matukio ya ziara hiyo katika picha.




Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi (CP) Liberatus Sabas, (wa pili kulia) akiongea na Askari wa kutuliza Ghasia katika Kituo cha Polisi cha Kasulu.



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi, (CP) Liberatus Sabas (wa tano kutoka kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na Maofisa wa Jeshi la Polisi, Watendaji Kata na Maofisa Tarafa, baada ya kumalizika kwa kikao kazi kilichofanyika kwenye ukumbi uliopo kituo cha Polisi Kasulu, mkoani Kigoma.



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi (CP) Liberatus Sabas (katikati), akikagua kitabu cha kufungulia mashtaka kwenye kituo cha Polisi cha Nyarugusu, baada ya kutembelea kambi hiyo na kuongea na askari wa kituo hicho.

**PICHA ZOTE: JESHI LA POLISI**



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# 'Yajimwambafai' ni lugha ya nchi gani?

NIMEANDIKA mara nyingi kuwa 'lugha' ni: 1) mpangilio wa maneno yanayotumiwa na watu wa jamii fulani katika mawasiliano. 2) mtindo anaotumia mtu katika kujieleza.

Lughawiya ni taaluma inayoshughulikia uchambuzi wa lugha katika nyanja mbalimbali kama vile sarufi, maana, matamshi na matumizi.

Nikiwa najiandaa kuandika makala yangu ya 'Tujifunze Kiswahili,' nilipokea ujumbe ufuatao kutoka kwa msomaji aitwae Kissiwa Z.K. wa Zanzibar aliyeandika:

"Bado uchafuzi wa lugha (Kiswahili) unaendelea. Gazeti nilipendalo (Nipashe – Mwanga wa Jamii), lichapishalo makala maalum kila Jumanne, kuhusu matumizi sahihi ya Kiswahili, limeandika: "YANGA YAJIMWAMBAFAI, PYRAMIDS WACHEKELEA."

"Bila kusoma maelezo yaliyofuata, nisingeelewa kabisa kile kilichokusudiwa kwa neno 'mwambafai.' Kuna haja gani mwandishi kutumia neno lisiloeleweka wakati neno rahisi analifahamu?

"Nina wasiwasi sasa tunaweza kukuta maneno kama 'goliraiz,' 'shindafai,' n.k. Je, lengo la kukuza Kiswahili Kimataifa litafikiwa?"

Kongole (shukrani; asante) Bw. Kissiwa wa Zanzibar kwa kuona ujinga (hali ya mtu kutojua jambo fulani) huo!

Kichwa cha habari katika gazeti maarufu linaloandika mambo ya siasa, kiliandikwa: "Ni kufuru Jangwani." Aya ya kwanza chini ya kichwa hicho ilisomeka:

"NI kufuru! Unaweza kueleza hivyo, kutokana na mipango ya mdhamini wa Yanga SC, Kampuni ya GSM katika kuleta mabadiliko makubwa yatakayowashangaza wengi ndani ya makao makuu ya klabu hiyo kongwe."

Nawanukuu wahenga waliosema "Sikio la kufa halisikii dawa." Maana yake mtu ambaye siku yake imefika kufa (sikio la kufa) hana budi kufa hata kama akifanyiwa dawa za aina gani.

Methali hii hutumiwa kutueleza kuwa jambo lililoandikiwa kuharibika halina budi kuharibika hata kama zitafanywa juhudi nyingi.

Katika miaka ya karibuni, neno 'kufuru' limekuwa likitumiwa kila uchao, tofauti kabisa na maana yake, yaani kitendo cha kusema au kutenda jambo lililo kinyume na dini. Kitendo cha kumkana Mungu. Tamko au tendo lililo kinyume na dini au kumkanusha Mungu.

Tujiulize: Kama kampuni ya GSM italeta mabadiliko makubwa Yanga na kuwashangaza wengi, hiyo 'kufuru' inatokea wapi? Iweje kuleta maendeleo iwe kufuru badala ya kupokewa kwa mikono miwili na kushangiliwa na viongozi, wanachama na mashabiki wa timu husika?

Upotoshwaji mwingine wa magazeti ya michezo ni huu: "KRC Genk anayocheza nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', Mbwana Samatta imeambulia kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Standard Liege ikijiandaa kuivaa Liverpool katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa itakayochezwa Jumatano."

Je, neno 'ambulia' limetumiwa ipasavyo? Hapana. Maana ya 'ambulia' ni kitendo cha kupata kitu kidogo kinyume na matarajio; fanikiwa kupata kiasi fulani ya kile kilichotajwa.

Kwa kuwa timu ya KRC Genk ilifungwa na timu ya Standard Liege bao1-0, timu iliyoambulia si KRC Genk anayocheza Samatta, bali iliyoambulia ni wapinzani wake, Standard Liege.

Labda ilitarajia kupata ushindi mzuri zaidi lakini ilichoambulia ni bao 1-0 tu. Sijui siku hizi mafunzo ya uandishi wa habari yakoje. Tuliofunzwa zamani tuliambiwa sepetu liitwe sepetu na si 'kijiko kikubwa' kwa kuwa limefanana na kijiko cha mezani!

Jina lingine la sepetu ni 'pauro' yaani chombo kipana cha bati chenye umbo la kijiko na mpini mrefu kinachotumika kuchimbia na kutekea udongo. Pia huitwa beleshi, shepeu/chepeu au chepe.

"Zahera arudi na mzuka Yanga" ni kichwa cha habari kilichofuatiwa na maelezo: "kukwea pipa na kikosi Jumapili kwenda Mwanza."

Nimeeleza mara nyingi kuwa 'mzuka' ni kiumbe kisichoonekana ila hudhaniwa kuwa kinaishi na huweza kumtokea mtu; pepo, jini. Timu ya Yanga ilipopambana na Pyramids FC ya Misri ilifungwa 2-1 jijini Mwanza. Je! Ndio 'mzuka' aliorudi nao Zahera kutoka kwao ili Yanga ifungwe?

'Kukwea pipa' maana yake nini? Tuchambue maana ya neno moja moja tukianzia na 'kukwea.' Neno hili latokana na 'kwea'(kitenzi) na maana yake ni kitendo cha kupanda juu ya kitu kama vile mnazi. Kwenda kwa kuelekea sehemu ya juu ya kitu kama vile mti au mlima.

'Pipa' ni chombo aghalabu kirefu na duara chenye ujazo wa zaidi ya lita 200 ambacho kiowevu/kirowevu (kitu cha majimaji kinachoweza kumiminika kwa mfano maji, maziwa n.k. hutiwa humo);tangi. Je, 'pipa' hukwewaje na huwa hivyo kwa minajili gani? Jamani ndege/eropleni si 'pipa' asilani!

**Methali: Yai haliatamii kuku.**
**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

UCHAMBUZI

NA MICHAEL ENEZA

# Ni elimu sekondari bure kwa wote; si Mahakama Kuu itazuia ndoa za utotoni

Yapo matazamio kuwa serikali itapeleka muswada bungeni wa kubadili Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, kufuatia kupitisha hukumu ya Mahakama ya Rufani ambayo ilikazia hukumu ya Mahakama Kuu ya mwaka 2016, kuwa vipengele vya sheria ya mwaka 1971, vinavyoruhusu ndoa za watoto wa miaka 15 ni kinyume cha Katiba.

Matazamio hayo yalielezwa wakati wa sherehe na nderemo miongoni mwa wanaharakati jijini Dar es Salaam, wakafikia hisia au tamati kuwa sasa suala la kubadili Sheria ya Ndoa halina mjadala.

Kuna wasiwasi kama nderemo hizo zinawakilisha hali halisi ilivyo, au ushindi huo ni upi.

Jambo ambalo walioshereheka uamuzi huo wa Mahakama ya Rufani hawakulitilia maanani au kuliangalia machoni ni kuwa hapakuwa na kesi halisi ya ndoa ya mtoto mdogo iliyopelekwa halafu ikabatilishwa na Mahakama Kuu, na Mahakama ya Rufani ikakazia hukumu hiyo.

Kilichotokea ni kuwa mwanaharakati Rebecca Gyumi alitafuta mwanasheria na kundi la wanasheria wakapeleka ombi la kisheria Mahakama Kuu kutaka vipengele vinavyoruhusu ndoa za utotoni kufutwa kwa sababu viko kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Inakiuka pia sheria ya mwaka 2016, ambayo inatoa adhabu ya kifungo cha miaka 30 kwa mtu anayemtia mimba mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari.

Ingekuwa kuna ndoa halisi iliyofungwa kwa msingi wa sheria ya mwaka 1971 ambayo wanaharakati tangu miaka 20 iliyopita wanapigania irekebishwe kwa kina halafu ndoa hiyo ikabatilishwa, tungejua kweli kuna mabadiliko hapa nchini.

Hata hivyo, isingekuwa nderemo kwa wanaharakati kwani hao ambao ndoa yao ingetenguliwa wangeweza kuhitaji mamlaka nyingine za kijamii ili waingilie kati ndoa hiyo iheshimiwe.

Ingekuwa ni tatizo la aina yake kijamii, na siyo ajabu lilete msuguano wa kijamii, kiitikadi.

Ndiyo maana nderemo za wanaharakati zinahitaji kutozishupalia sana kwani hakuna ushindi halisi katika suala hilo, kwani ni hoja tu za kisheria na siyo kubatilisha ndoa halisi iliyofungwa na mojawapo kati ya mamlaka za aina tatu zinazoweza kufungisha ndoa.

Zipo mamlaka za kidini, za kimila na za kiutawala, hasa katika serikali za mitaa (wilaya) au Mahakama ya Mwanzo.

Kwa maana hiyo sheria muhimu ya kuzuia ndoa za utotoni ni ile ya 2014 kuwa msichana husika ni mwanafunzi, hivyo kutaka aozeshwe ni kosa la jinai linaloleta kifungo kirefu kwa mhusika. Hadi iwe ndoa itakuwa zaidi ya mmoja, kiutaratibu.



Distributed via ippmedia

Wanafunzi kama hawa wana nafasi kubwa ya kuepuka ndoa na mimba za utotoni, kwa kuendelea na masomo hadi kidato cha nne, kiwango cha elimu ambacho mara nyingi mhitimu anakuwa na umri wa miaka 18. **PICHA: MTANDAO**

> "Lazima awe mtu mwenye maslahi halisi katika tukio hilo ili aweze kupeleka shauri mahakamani, inaitwa Kilatini 'locus standi' (wapi amesimama) kisheria.

Ndiyo sababu wanaharakati wanatakiwa kuelekeza macho yao katika sheria ya mwaka 2016, kwani serikali ina uwezo wa kusimamia sheria hiyo ipasavyo, lakini pale msichana husika siyo mwanafunzi, na mojawapo kati ya mamlaka za kufungisha ndoa imeridhia na kuratibu ndoa hiyo, haitaweza kulazimisha hiyo hukumu.

Sababu ni kuwa wanaohusika na ndoa hiyo hawatafika mahakamani kudai chochote kwani wanaridhika na kilichotokea, na kama kuna mwanaharakati asiyeridhika, hataweza kwenda mahakamani kwani atakosa mahali pa kusimama kupeleka kesi.

Lazima awe mtu mwenye maslahi halisi katika tukio hilo ili aweze kupeleka shauri mahakamani, inaitwa Kilatini 'locus standi' (wapi amesimama) kisheria.

Tafsiri ya kisheria ambayo mtu unaweza kuifanya ni kuwa ushindi huo ambao wanaharakati wameupata juu ya sheria yenyewe ni dhaifu, unaweza kupeperushwa na upepo; hauna udhati wa kuingilia mamlaka zilizoainishwa kufunga ndoa.

Mamlaka mbili zitatii au zinatakiwa kutii uamuzi wa Mahakama, yaani zile za kiraia (kwa mfano Ofisi ya DC au Mahakama ya Mwanzo, wakati zile za kidini kila moja itakuwa na tafsiri yake. Kwa mamlaka za kidini rai ya Mahakama ya Rufani ni mawaidha tu, hayawafungii nira.

Ina maana kuwa wanaharakati wawe macho wasije wakajipoteza kudhania kuwa wanaweza kufuatilia suala hilo 'hadi kieleweke,'kwani watagundua ambacho hadi sasa wameshindwa kukiona, kuwa yako makundi tofauti katika jamii kuhusiana na suala la ndoa.

Ina maana kuwa uhalali wa ndoa una pande tatu ili uthibitishwe, kwanza wahusika wa kuoana, halafu wazazi wao endapo wahusika wa ndoa ni vijana wadogo, na mwisho mamlaka mojawapo ya kufungisha ndoa inayotambuliwa kisheria.

Hakuna hata moja kati ya mamlaka hizo ambayo kwa msingi huo iko tayari kuachia mamlaka yake kwa nyingine, ijifute tu.

Ina maana pia kuwa uamuzi huo wa Mahakama ya Rufani ni sawa na kubatilisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kusema kuwa vyanzo vya sheria katika jamii siyo pamoja na jumuiya za kidini, ila ni Bunge na Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani.

Uamuzi wa mahakama hizo mbili unazifunga mamlaka za kiraia zenye uwezo wa kufungisha ndoa, kwa mfano Mahakama ya Mwanzo au DC (Mkuu wa Wilaya) lakini haizifungi mamlaka za kidini.

Ili mamlaka hizi ziendane na maamuzi hayo ya Mahakama, inabidi mabaraza yao ya kisheria yaangalie kama yatoe maelekezo kwa makadhi wanaofungisha ndoa, kuwa rai hiyo si mbaya kwa tafsiri hii au ile ya sheria ya kidini, na siyo kwamba inazifunga mamlaka kama ilivyo.

Ina maana kuwa sheria isiyopingika kwa kutumika kwake bado ni ile ya 2016 inayohesabiwa kuwa ni sehemu ya sheria kuhusu elimu, kuwa ni kosa kumwozesha mwanafunzi akiwa bado anaendelea na masomo yake, au kuyakatisha kwa dhamira ya kumwozesha.

Pale ambapo msichana hayuko shuleni halafu mamlaka mojawapo ikafungisha ndoa, siyo rahisi kwa mamlaka zilizobaki kubatilisha maamuzi ya mamlaka husika kwani upande wa jamii unaohusika na mamlaka hiyo unaweza kuamua kutetea mamlaka yake kufungisha ndoa kama inavyoeleweka, Ikifika hapo suala ya uamuzi wa mahakama litakuwa halipo.

Jambo la msingi ni kuwa silaha halisi ya kuzuia ndoa za utotoni ni wasichana kuendelea na shule hadi kukamilisha elimu ya sekondari, kwani katika hali hiyo serikali inaweza kutetea ulazima wa mtoto wa kike kusoma.

Utetezi huo na ulazimishaji wa kuendelea na masomo hadi amalize hauwezi kuleta tatizo katika jamii, lakini endapo serikali kwa wakati uliopo siyo mdau (mshirika wa moja kwa moja) katika hali ya kijamii ya msichana husika, yuko tu chini ya wazazi wake, kuzuia mamlaka nyingine za kuidhinisha ndoa zisifanye kazi inaweza kutuletea vurugu. Ni kuwapa mfupa wa kutafuna wahafidhina.

Uamuzi huo na furaha ya wanaharakati ni kielelezo tu cha udhaifu wa wanaharakati kuelewa masuala ya kijamii, wakidhani kuwa kila kitu kinaishia katika sheria na maamuzi ya Mahakama, wakati jadi ina nafasi yake.

Inabidi wanaharakati wapiganie haki ya mtoto kusoma hadi akamilishe elimu ya sekondari ambako atakuwa anapiga hodi umri wa miaka 18, siyo kumwacha nyumbani halafu kuzikoromea mamlaka za kijamii (wazazi, makadhi) kuwa asiolewe, bado mdogo.

Suluhu ya ndoa za utotoni ni elimu isisimamishwe hadi sekondari ikamilike, kwani ikidhamiriwa hivyo na miundombinu ipo, serikali itakuwa na uwezo wa kufuatilia na kutekeleza, lakini watoto wakiachwa nyumbani si rahisi walindwe wasiolewe kwani ni jitihada isiyo na mashiko kijamii (kuwa ni mwanafunzi) itagombanisha mamlaka zetu.

ELIMU

**NA BEATRICE PHILEMON**

# Mbeya, shule iliyoanza kwa nyasi yaonyesha inawezekana

- Bado inachangamoto zinazohitaji wadau waichangie
- Taaluma inapanda na utoro unatokomea

UKIZUNGUMZIA Shule ya Msingi Mbeya, si wananchi wote katika Kata ya Mnyeu, Wilaya ya Newala ilipo, wanaoifahamu.

Ilianza kama shule ya chekechea, watoto wakisoma chini ya mti wa Mwembe ambapo mwalimu wa kuwafundisha kipindi hicho alikuwa akitoka Shule ya Msingi Mnyehu, iliyo Kata ya Mtopwa, Tarafa ya Kitangari, Wilaya ya Tandahimba, mkoani Mtwara.

Ilianzishwa mwaka 2001, ikiwa ni maalumu kwa ajili ya kupunguza umbali mrefu (Access School au satellite) kwa wanafunzi kutoka vijiji vya Mbeya na Mbebede.

Wakati huo wanafunzi walikuwa wakitembea umbali wa kilometa tano kwenda, vivyo hivyo kurudi kutoka Shule ya Msingi Chaume, iliyo Kata ya Chaume, wilayani Tandahimba, walikokuwa wakifuata elimu.

Hayo ni kwa mujibu wa Mwenyekiti, wa Kamati ya Shule ya Msingi Mbeya, Mshamu Tepu, wakati akizungumza na waandishi wa habari na wafanyakazi kutoka Shirika la ActioAid Tanzania walipoitembelea shule hiyo.

Ilikuwa ni katika ziara ya kukutana na uongozi wa shule na kuona mazingira yake lakini pia wanafunzi kutoka vijiji vya Mbeya na Mbebede wanavyoendelea kielimu pamoja na changamoto zinazowakabili.

"Wakati shule inaanza, wanafunzi walikuwa wakipata shida kipindi cha mvua kwani ilibidi wabaki nyumbani hivyo kukosa masomo, lakini sasa hali ni nzuri ingawa baadhi ya miundombinu haijakaa vizuri kwa sababu ya uchakavu wa majengo, ikiwemo vyoo," anasema na kuongeza:

"Tulipoona kuna changamoto ya umbali kwenda shuleni kwa watoto wetu, tuliamua kama wazazi mwaka 2001, kujenga kibanda cha miti na kukiezeka kwa nyasi ili waweze kusoma hapa hapa kijijini."

Tepu anabainisha kuwa baadaye waliitisha mkutano wa kijiji uliokubaliana wafyatue matofali kwa ajili ya kuboresha darasa hilo la nyasi.

"Bahati nzuri tulipata ugeni kutoka Shirika la ActionAid Tanzania uliotembelea kijiji chetu kabla hatujaanza ujenzi wa darasa, kuangalia changamoto zinazotukabili," anasema na kuongeza:

"Tuliwaomba ActionAid Tanzania watusaidie kujenga madarasa kwa ajili ya watoto wetu, kwani wanafunzi wengi kutoka katika vijiji vyetu vya Mbeya na Mbebede walikuwa wanatembea umbali mrefu kwenda kutafuta elimu kijiji kingine."



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mbeya, Alphan Gama (aliyesimama), akimuelekeza mwanafunzi wa darasa la tano, Jabiza Abdallah somo la kingereza. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON**

> Tulipoona kuna changamoto ya umbali kwenda shuleni kwa watoto wetu, tuliamua kama wazazi mwaka 2001, kujenga kibanda cha miti na kukiezeka kwa nyasi ili waweze kusoma hapa hapa kijijini.





Fatuma Mtanda akionyesha darasa walilokuwa wanasomea wanafunzi kabla ya ujenzi wa madarasa mapya.

Aidha, anabainisha kwamba kutokana na umbali uliokuwepo, wanafunzi wa darasa la kwanza walikuwa wakichelewa kufika shule, kwa sababu umri wao mdogo uliowapa shida ya kutembea umbali wa kilometa tano kwenda na kilometa tano kurudi kila siku.

"ActionAid Tanzania walikubali kutujengea madarasa lakini waliomba wananchi nao wachangie katika ujenzi na sehemu itakayobaki wao watamalizia," anasema na kuongeza:

"Wananchi walifanikiwa kufyatua tofali na kuanza ujenzi hadi kufikia hatua ya boma na baada ya hapo ActionAid Tanzania walimalizia ujenzi wote, ikiwemo kutoa viti na meza kwa ajili ya wanafunzi."

Anasema mwaka 2008, ActionAid Tanzania walikuja tena kuitembelea shule hiyo na walipoona mazingira ya darasa si mazuri, walijenga tena madarasa mengine mawili na matundu manane ya vyoo kwa ajili ya wanafunzi.

"Ndipo tulipoamua kuanzisha darasa la kwanza rasmi mwaka huo wa 2008, shule ikianza na wanafunzi 39, wavulana wakiwa 18 na wasichana 21.

### CHAKULA SHULENI

Tepu anasema mfumo wa kuchangia chakula na uji shuleni kwa ajili ya wanafunzi ulioanzishwa na ActioAid Tanzania umeleta mafanikio makubwa.

Hiyo ni kwa sababu wanafunzi sasa wanapenda kwenda shule tofauti na miaka ya nyuma.

"Kila mwezi ActionAid walikuwa wanaweka fedha kwenye akaunti ya shule kuwezesha wanafunzi kupata chakula... kupitia mfumo huo watoto wengi wanahudhuria shule, utoro umepungua, watoto wanasoma kwa bidii na ufaulu umeongezeka," anasema.

Mwenyekiti anabainisha kwamba baada ya wazazi kuona mfumo huu ni mzuri, nao waliamua kuanzisha utaratibu wa kuchangia chakula shuleni, ambapo kila mzazi mwenye mtoto anatakiwa kuchangia.

"Kila mwaka tunachangia chakula kwa ajili ya wanafunzi, huku kila mzazi akichangia kilo 15 za mahindi na kilo tano za kunde na njugu kwa mwaka kwa kila mtoto," anasema.

Anabainisha, kamati imetenga ekari mbili za shamba kwa ajili ya kilimo cha korosho ili kujiongezea kipato kwa ajili ya maendeleo ya shule, mbegu wakipata kutoka Taasisi ya Utafiti ya Mtopa (Mtopa Research Institute).

### MIUNDOMBINU MINGINE

Mwenyekiti anasema kamati yake imepanga kujenga nyumba ya mwalimu kupitia michango ya wananchi.

Aidha, anasema imetenga ekari mbili za ardhi kwa ajili ya uwanja wa michezo na kuchimba vyoo viwili vya kudumu kwa ajili ya walimu.

### MKUU WA SHULE

Mwalimu mkuu wa shule hiyo, Alphan Gama, anabainisha kwamba shule hiyo ilisajiliwa mwaka 2008, maalumu kuhudumia wanafunzi kutoka vitongoji vya Mbeya na Mbebede.

Mwalimu Gama anasema kuwa mpaka sasa shule ina walimu wa kiume wanne na nyumba moja ya mwalimu. Vilevile, ina jumla ya wanafunzi 123, kati yao, wavulana 67 na wasichana 56.

Kwa upande wa darasa la awali, Mwalimu Gama anasema kuna wanafunzi 102 ambao wanasoma darasa moja na la kwanza, kutokana na uhaba wa madarasa.

### UHABA WA WALIMU

Mwalimu Gama anafafanua bado wana uhaba wa walimu, wakiwemo wa kike.

"Kwa mara ya mwisho walimu waliletwa katika shule yetu mwaka 2014, kipindi hicho kulikuwa na walimu watatu tu," anasema.

Kwa upande wa miundombinu, Mwalimu Gama anasema bado wanahitaji darasa moja kwa sababu darasa la kwanza na la awali wanasoma kwenye chumba kimoja cha darasa na kimechakaa.

"Pia hali ya vyoo si nzuri, vinahitaji ukarabati na kuna darasa lililojengwa na wananchi linahitaji kumaliziwa na kupakwa rangi," anasema.

### TAALUMA

Akizungumzia ufaulu, mwalimu Gama anasema ingawa shule imekuwa na changamoto, bado inafanya vizuri upande wa taaluma.

"Kwa mfano mwaka 2017, jumla ya wanafunzi 14 walifanya mtihani wa darasa la saba na kati yao 10 walichaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari, huku shule ikishika nafasi ya 28 kiwilaya kati ya shule 74," anasema na kuongeza:

Mwaka 2018, jumla ya wanafunzi 11 walifanya mtihani wa darasa la saba na wanafunzi watano miongoni mwao walichaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari, huku shule ikishika nafasi ya 56 kiwilaya kati ya shule 74.

### KUTHAMINI ELIMU

Mwalimu Gama anabainisha kwamba ingawa kwa hivi sasa wazazi wamekuwa na mwamko mzuri wa kupeleka watoto wao shuleni, bado changamoto ipo kwenye suala la umuhimu wa elimu.

"Wazazi wanaturudisha nyuma kwa sababu walimu tunatumia nguvu nyingi zaidi kuhamasisha wazazi katika suala la elimu na chakula.

"Unakuta masuala ya sherehe za unyago, ngoma na sherehe zingine ndizo zinazochangiwa fedha nyingi zaidi kuliko suala la elimu," anasema.

### USHAURI

Mkuu huyo wa shule anaasa kuwapo mikutano ya pamoja kati ya wadau wa elimu na wazazi ili kuwaelimisha wazazi juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto wao.

"Lakini pia mikutano ya jamii ili kuielimisha juu ya umuhimu wa elimu ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa chakula shuleni kwa ajili ya wanafunzi.

### RUZUKU YA ELIMU

Kwa upande wa ruzuku inayotolewa na serikali (Capitation grant), Mwalimu Gama anasema bado haitoshi.

"Kwa mwezi tunapokea Sh. 47,000/- tu za Capitation grant kwa ajili ya matumizi ya stationery, kuchangia mitihani ya elimu, michango ya elimu, kununua chaki, utawala, michezo, ukarabati na gharama za ujenzi," anasema na kuongeza: "Fedha hii ni ndogo ukilinganisha na matumizi ya shule, angalau tungepewa Sh. 100,000/- kwa mwezi."

### MAKAMU MWENYEKITI

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Shule, Fatuma Abdallah, anasema kamati imekuwa ikitumia nguvu nyingi kuhamasisha wazazi kuhusu masuala ya elimu.

Hiyo ni kwa sababu kabla ya mwaka 2002, asilimia kubwa ya wazazi walikuwa hawajui kusoma wala kuandika kwa sababu katika maeneo hayo hapakuwa na shule.

Anasema, kabla ya utoaji chakula shuleni, asilimia 25 ya watoto walikuwa watoro.

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

# Tujifunze darasa la haki kodi kutoka kwa wanaoisimamia



Aliyekuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Charles Kichere (kulia), alipozungumza na walipa kodi katika banda la TRA katika Maonyesho ya 42 Biashara Kimataifa maarufu Sabasaba, jijini Dar es Salaam. Kwa sasa Kichere, ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), akichukua nafasi ya Mussa Asaad. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Niko Kasera**

PROF. Mussa Assad, ana siku chache tangu aanze maisha ya ustaafu, akitoka kwenye wadhifu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Kabla ya hapo, alishika chaki kwa wanaosaka digirii mbalimbali za taaluma ya uhasibu au zenye somo hilo, alitafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Hili la mwisho alilostaafu nalo lilikuwa na unyeti wa kipekee kitaifa, kwani ni jukumu lenye dhamana ya kukagua na kusimamia rasilimali za kitaifa.

Alipokuwa amebakiza miezi mitatu ofisini mnamo Agosti 11, kwenye semina jijini Dodoma, Profesa Assad alipata fursa ya kutoa neno ndani ya mkusanyiko huo wa kitaaluma.

Hapo alitoa darasa kwa kutumia mfano uliowagusa wengi miongoni mwa waliohudhuria, hasa pale aliposema kwamba pamoja na kodi kuwa wajibu, ni muhimu kwa serikali yeyote kuwaonyesha walipa kodi kwamba kodi zao zinatumika kuboresha hali yao ya maisha.

Alieleza: "Chukua mfano wa eneo la makazi la Sinza Dar es Salaam. Ikiwa wakazi wa Sinza wataona wazi kwamba mitaa ya mle mle yanajengewa lami na huduma za upatikanaji maji inaboreshwa, itakuwa rahisi kupata walipa kodi wengi zaidi kujitokeza."

Tafsiri aliyoiotoa Profesa Assad, inaangukia katika kilekile ambacho Rais Dk. John Magufuli, ameisisitiza mara nyingi, akihimiza ulipaji kodi hata akatoa darasa kwa wanunuzi kwa kuwasisitiza kudai risiti, lengo kubwa ni kuhitimishiwa malipo ya kodi.

Anasema, kutokana na malipo ya kodi yakiwa vizuri, inaisaidia serikali kuwa na uwezo kuhitimisha majukumu yake na hasa ya kimaendeleo, ikitumia fedha zake za ndani.

Hapo anainisha miradi ujenzi wa reli ya kisasa, ununuzi wa ndege mpya zaidi ya 10 kwa ajili ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kwa kutumia fedha za ndani, ikimaanisha makusanyo ya kodi na vyanzo mbalimbali.

Ni dhahiri ulipaji kodi wa hiari ni msingi muhimu kwenye dhana ya uwajibikaji wa mwananachi kila mmoja kwa nafasi yake. Kadri tunapoendelea kupanua wigo wa idadi ya walipa kodi, ndivyo kiasi kinachokusanywa kitaongezeka, hivyo kuiwezesha serikali kutimiza ndoto yake ya maendeleo kwa jamii.

Prof. Assad katika kauli yake amehimiza dhana hiyo kwamba ili jamii kuhoji matumizi ya serikali kuu na serikali za mtaa, ni vyema sote tuwe walipaji kodi wa hiari na sio kwa shuruti au kuwajibishwa.

Uwajibikaji ni msumeno wa haki, unaojikita pande zote. Ni wajibu Watanzania wakalipa kodi na hilo wala halina ubishi. Miaka 50 ijayo, vizazi vinavyozaliwa leo vikiwa watu wazima, watakuwa na cha kuhadithia namna babu zao walivyothubutu, wakajenga reli za kisasa.

Wakati huohuo, miradi ya serikali kuu na serikali za mitaa sharti zionyeshe kwamba sio tu fedha zimetumika, bali zimetumika kukidhi viwango vya ubora na kuridhisha.

Mifano ni mingi ambayo kwa kazi za ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa vipindi tofauti, namna anavyoibua kwa miaka nenda rudi kuhusiana na baadhi ya miradi kutotendewa haki, mathalan ujenzi usokidhidhi viwango, kutokamilika kwa wakati au upotevu wa fedha za miradi.

Huku tukiadhimisha miaka minne ya Rais Dk. Magufuli kuwa madarakani, daima tusiwe mbali na hotuba zake zenye maelekezo, pia kukemea mabaya mbalimbali kwa taifa, hapo tukigusa rushwa, ubadhirifu wa mali za umma na watendaji na Watanzania kwa ujumla.

Iwapo tuna nia ya dhati kuandamanana kufikia dira ya taifa kuisaka uchumi wa kati, hatuna budi kuhakikisha tunawatumia vyema wataalamu wabobezi tulionao ambao nao ni muhimu wakawa waumini wa kulitakia mema taifa. Naamini sote tutafika.

**Kwamaoni na ushauri wasiliana kupitia: samawatiarts@yahoo.com**

JE, WAJUA?

# Kwa nini kupoteza ujauzito bado ni mwiko kuzungumzia?



Mama mjamzito ambapo ripoti imeonyesha kwamba bado inaonekana kama mwiko kuzungumzia kupoteza ujauzito kwa mujibu wa WHO. **PICHA: MTANDAO**

KUPOTEZA mtoto wakati wa ujauzito au ujauzito usio riziki bado ni jambo linaloonekana kama mwiko kulizungumzia ulimwenguni kote, mwiko unaoambatana na unyanyapaa na aibu.

Wanawake wengi bado hawapati matunzo sahihi na ya heshima wanapopoteza ujauzito au kupoteza mtoto wakati wa kujifungua.

Mimba inapotoka au kuharibika ni dhahiri umepoteza mtoto wakati wa ujauzito, lakini fikra huwa tofauti kutokana na sababu mbalimbali.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), asilimia 10 ya wanawake waliofahamu kuwa wao ni wajawazito, hutambua mimba inapoharibika.

Hali hiyo hufafanuliwa na kupokelewa kwa namna tofauti ulimwenguni, lakini kwa ujumla mtoto ambaye hufa kabla ya wiki 28 katika ujauzito husemekana kama ni kupoteza mimba, na watoto wanaokufa baada ya wiki 28, bado ni ujauzito usio riziki.

Kila mwaka, watoto milioni 2.6 hawaishi kutokana na mimba kuharibika au kutoka, na vifo vingi kati ya hivyo vinaweza kuzuiwa, inasema WHO.

Walakini, kupoteza mtoto au ujauzito usio riziki huwa hauwekewi kumbukumbu kwenye mfumo wa usajili wa watoto, hata katika nchi zilizoendelea, na hivyo kudhihirisha kwamba idadi hiyo inaweza kuwa kubwa zaidi.

Ulimwenguni kote, katika nchi nyingi, hospitali na kliniki mara nyingi hazina rasilimali na waajiriwa wa kutosha. Unyanyapaa, aibu na hatia huwa ni suala la kawaida linalozungumzwa na wanawake ambao wamepoteza watoto.

Wanabainisha hufanywa kuhisi kwamba wanapaswa kukaa kimya kuhusu huzuni yao, mara nyingi kwa sababu kupoteza mimba na ujauzito usio riziki bado ni jambo linalochukuliwa kuwa ni la kawaida sana, au kwa sababu linaonekana kwamba haliwezi kuepukika.

Suala la kupoteza mtoto bado linachukuliwa kama mwiko au kitu cha aibu. Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, kwa kawaida inaaminika kwamba mtoto aliyekufa kabla ya kuzaliwa au kuharibika kwa mimba, ni kunatokana na masuala ya uchawi au mashetani.

Haya yote yanasababisha madhara makubwa kwa wanawake,wengi wakikabiliana na masuala ya afya ya akili ambayo hudumu kwa miezi au miaka, hata wanapoendelea kuwa na watoto wengine wenye afya.

Larai, ni mfamasia aliye na miaka 44 kutoka Nigeria anasimulia alivyopoteza mtoto wake:

"Kukabiliana na hali ya kupoteza ujauzito wa mtoto wangu, iliniumiza sana...Wauguzi walichangia katika huzuni yangu licha ya mimi pia kuwa ni daktari," anasema na kuongeza:

"Suala lingine ni utamaduni... katika tamaduni nyingi za Kiafrika, watu hufikiria kwamba unaweza kupoteza mtoto kwa sababu ya laana au uchawi."

Mfamasia huyu anasema kwamba hapa ndipo huwa chanzo cha unyanyapaa kwa sababu watu wengine wanaamini kuwa mwanamke anayepoteza mtoto mara kwa mara ana nuksi, au laana.

"Na wengine huamini kwamba inawezekana kuwa ni mzinifu, hivyo ni kama adhabu kutoka kwa Mungu," anasema.

Kupoteza mtoto kunaweza kusababishwa na hali isiyo ya kawaida ya mfuko wa uzazi, umri wa mama, maambukizo, ambayo mengi huzuilika kama vile ugonjwa wa malaria na kaswende.

Hata hivyo, sababu halisi ya maambukizi haya mara nyingi ni ngumu kuitatua.

Distributed via inpmedia

Ushauri wa jumla wa kuzuia kupoteza mtoto wakati wa ujauzito ni kama vile lishe bora, kufanya mazoezi, kujizuia kuvuta sigara, dawa za kulevya na pombe, kupunguza kiwango cha kafeini, kudhibiti mfadhaiko, na kuwa na uzito wa mwili unaofaa.

Hii inasisitiza mwenendo wa maisha, ambayo, kusipokuwa na sababu maalum kunaweza kusababisha wanawake kuhisi hatia, kwamba wamesababisha kupoteza ujauzito wa watoto wao.

Suala la kupoteza mtoto bado linachukuliwa kama mwiko au kitu cha aibu. Kama ilivyo masuala mengine ya kiafya kama vile afya ya akili, ambayo bado kuna mwiko mkubwa kuijadili.

Wanawake wengi wanaripoti kuwa hajjalishi tamaduni zao, elimu au malezi yao, marafiki na familia zao hawataki kuzungumzia jinsi walivyopoteza mtoto wakati wa ujauzito.

Hiyo inatokana na ukimya wa kuzungumzia huzuni inayoletwa na hali hiyo kwa ujumla.

Huduma bora wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua, kunaweza kuzuia ujauzito usio riziki kwa zaidi ya nusu milioni ulimwenguni kote.

Hata katika nchi zenye kipato cha juu, utunzaji ni jambo muhimu kwa ujauzito usio riziki.

Kuboresha upatikanaji wa matunzo wakati wa ujauzito, kufuata mwongozo unaotolewa na wakunga na kuelimisha jamii umuhimu wa matunzo wakati wa ujauzito, kunaweza kupunguza idadi ya watoto wanaokufa wakati wa ujauzito.

Hiyo ikijumuishwa na matibabu ya maambukizo ya magonjwa mbalimbali wakati wa ujauzito, vipimo vya mara kwa mara na uangalizi mkubwa wakati mama anapokuwa na uchungu wa kujifungua.

Hatua hizo zinaweza kuokoa watoto milioni 1.3 ambao wangezaliwa wamekufa au mimba kupotea. **HABARI UN**

RIPOTI

# Binadamu wa kale nchini Israel walivyohifadhi nyama pangoni

WANASAYANSI nchini Israel, wanasema kuwa wamepata ushahidi kwamba binadamu wa kale walihifadhi nyama kwa lengo la kula siku zijazo.

Ushahidi huo umebainisha kuwa watu walioishi miaka kati ya 200,000 na 420,000 iliyopita, walikuwa na uwezo wa kung'amua mahitaji yao ya baadaye, wanasema.

Watafiti walichunguza mifupa iliyopatikana katika pango la Qesem karibu na mji wa Tel Aviv.

Waligundua alama katika mifupa iliyokatwa, ikiashiria ni mbinu ya kuhifadhi chakula kisiharibike ili kiweze kuliwa baadaye.

Watafiti wanasema alama hizo ziliwekwa kwasababu binadamu wa kale hawakuwa na uwezo wa kutoa ngozi iliyokauka kwenye mfupa uliohifadhiwa kwa muda mrefu.

Alama hizo zilionekana kwa asilimia 78 ya zaidi ya mifupa 80,000 ya wanyama waliochunguza.

"Mafuta yanayopatikana katika mfupa huwa chanzo muhimu cha lishe bora...Kufikia sasa, ushahidi umeashiria utumiaji wa mara moja wa korongo kufuatia uchunguzi uliofanyiwa mifupa hiyo baada ya kuondolewa kwa tishu laini," anasema Ran Barkai kutoka Chuo Kikuu cha Tel Aviv nchini Israel.

Binadamu wa kale walikuwa wakiwinda kulungu la mwendo, walihifadhi miguu na fuvu la kichwa cha wanyama hao pangoni na kisha kuondoa mabaki ya mnyama katika eneo alipouliwa, anasema Profesa Jordi Rosell wa Chuo Kikuu cha Rovira Virgili nchini Uhispania.

Watafiti walithibitisha kuwa hali katika pango hilo iliruhusu mafuta kwenye mifupa iliyohifadhiwa kuwa lishe kwa hadi wiki tisa, baada ya mnyama huyo kuuawa. **BBC**



Katika uchunguzi wao wanasayansi walipata alama katika ngozi ya mifupa iliyohifadhiwa. **PICHA: MTANDAO.**

TEKNOLOJIA

**NA JOSEPH MUHOZI**



Baadhi ya askari kutoka mojawapo ya kampuni za ulinzi nchini. **PICHA: MTANDAO**

# PSGP: Kanzi data ajira walinzi binafsi kuanzishwa, waajiri kuwachagua

KATIKA dunia ya sasa huwezi kutaja ulinzi bila kujumuisha sekta ya ulinzi binafsi ambayo inakuwa kwa kasi duniani kote ikitajwa kuwa inaajiri idadi kubwa ya watu.

Hiyo ni karibu mara mbili ya askari polisi kwenye nchi takribani 40 zenye jumla ya watu bilioni 4, ambao ni zaidi ya nusu ya idadi ya watu wote duniani (bilioni 7.5).

Hii ni kwa mujibu wa utafiti uliochapishwa kwenye Gazeti la The Guardian la Uingereza mwaka 2011. Sekta hii inatoa ajira kwa takribani watu milioni 20 duniani.

Kasi ya maendeleo ya Tanzania kuelekea uchumi wa kati inahuishwa na uhakika wa ulinzi na usalama.

Kwakuwa kazi nzuri ya majeshi yetu imefanya mipaka yetu kuwa salama na nchi yetu kuwa salama na yenye amani, Jeshi la Polisi limeipa nafasi sekta ya ulinzi binafsi kusaidia kuongeza nguvu ya ulinzi kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba ulinzi wenye tija na uhakika huhuisha ukuaji wa uchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja mithili ya mbolea ya samadi kwenye shamba la mchicha.

Uhakika wa ulinzi na usalama huwavuta wawekezaji kwa makumi elfu kwani wana uhakika uwekezaji wao na familia zao zitakuwa salama salmini!

Hata hivyo, changamoto ilikuwa katika kuidhibiti sekta hii na kusimamia ufanisi wake kwani baadhi ya kampuni hasa katika nchi zinazoendelea zimekuwa yakiajiri 'ili mradi mlinzi', bila kujali mafunzo aliyopitia, uwezo wake wa kufanya kazi, afya na mwenendo wa tabia yake.

Utafiti uliofanywa mwaka 2011 ulitahadharisha kuwa kasi ya kukua kwa sekta ya ulinzi binafsi duniani inazidi mifumo ya kuisimamia na kuidhibiti na kwamba nchi nyingi hasa zinazoendelea hazijaweka mifumo mizuri ya kudhibiti.

Lakini Serikali ya Tanzania imebaini changamoto hiyo na imeifanyia kazi kwa kasi kwa kutumia teknolojia itakayowachuja walinzi binafsi na kuhakikisha ufanisi na ubora wa sekta hii nyeti.

Ni kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Sekta ya Ulinzi Binafsi nchini kwa njia ya kielektroniki (PSGP), ambao uko chini ya Jeshi la Polisi, ukiratibiwa na Kampuni ya Kitanzania ya DataVision International ambayo mwaka huu ilishinda tuzo ya 'East Africa Brand Leadership 2019' kama kampuni bora zaidi katika utoaji wa huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), utafiti pamoja na utengenezaji wa mifumo ya malipo ya kielektroniki

Hatua hii ilitokana na hali iliyokuwa imeanza kubainika kwa baadhi ya kampuni kuwaajiri wazee wasiojiweza na vijana wasio na mafunzo mahsusi.

Hali hii ilisababisha Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola akiwa Mkoani Mara, Julai 19, 2019 kueleza kuwa watazifuta kampuni zote ambazo zinaajiri askari wazee wasiojiweza pamoja na vijana wasio na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au Jeshi la Akiba la Mgambo.

Katika kuboresha sekta hii, kwa mujibu wa Ofisa Mratibu wa Mradi huo, Macmillan George, PSGP imeshawasajili na inaendelea kuwasajili wafanyakazi wa kampuni binafsi kwenye kanzi data kwa hatua ya kwanza ya utambuzi na kuwapa askari vitambulisha; na sasa inaanza zoezi la kuwaweka kwenye kanzi data ya ajira wenye sifa na waliothibitishwa na Jeshi la Polisi.

Kupitia kanzi data hiyo, kutakuwa na makundi yote ya askari na sifa zao, ikiwa ni pamoja na mafunzo waliyopitia, jinsia, namba yake ya utambulisho na sifa nyingine mtambuka.

Hivyo, kanzi data hiyo itawapa uhakika na urahisi wadau kwenye sekta ya ulinzi binafsi kuchagua walinzi wanaowahitaji wakiwa na uhakika wa uwezo wao, uzoefu wao, mienendo yao na hata uimara wa afya zao.

Kwa mfano, kama unahitaji mlinzi wa kike mwenye uwezo wa kutumia bunduki na mwenye uzoefu usiopungua miaka mitatu, utaingia moja kwa moja kwenye kanzi data na utafanya machaguo kwa urahisi.

Hatua nyingine inayofanywa na Jeshi la Polisi ni kuhakikisha inaratibu mafunzo kwa walinzi wote wa sekta binafsi na kuwapa vitambulisho kupitia PSGP, ili kuondoa mianya ya wasio na sifa kujipenyeza.

> "Kupitia kanzi data hiyo, kutakuwa na makundi yote ya askari na sifa zao, ikiwa ni pamoja na mafunzo waliyopitia, jinsia, namba yake ya utambulisho na sifa nyingine mtambuka.

Hivyo, unaweza kulala usingizi ukiwa na uhakika wa mlinzi binafsi anayekulinda wewe na mali zako.

Kanzi data hii pia itasaidia Serikali kuongeza nyenzo ya kukusanya kodi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Hii ni kodi ambayo ingeweza kuwa inapotea kwa kutokuwepo mfumo wa kumtambua kila mfanyakazi wa sekta hii yenye idadi kubwa ya askari hata zaidi ya askari wa jeshi la polisi.

Mfano, Kampuni kubwa zaidi ya ulinzi binafsi duniani, G4S yenye wafanyakazi takribani nusu milioni duniani kote ikiwa ni pamoja na Tanzania, imewahi kueleza kuwa iliingiza Pauni bilioni 6.8 mwaka 2016 tu na ilipata faida ya Pauni 454 milioni (sawa na Sh. 1.4 Trilioni za Tanzania) kati ya mwaka 2015-2016, na kwamba kwa Afrika tu pato lake lilikua kwa asilimia saba kwa mwaka.

Hii ni kampuni moja tu. Lakini kwa kutumia PSGP na mifumo mingine ya Serikali ya ukusanyaji kodi ni rahisi kutambua idadi ya wafanyakazi na kodi yao ikalipwa kwa usahihi.

Hivyo, Serikali, kampuni binafsi na wananchi kwa ujumla watafaidika na kuboreshwa kwa sekta ya ulinzi binafsi kupitia PSGP.

***Mwandishi anapatikana kwa simu: 0754999541***



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

MOJA ya tuhuma zinazoelekezwa kwa baadhi ya wahadhiri na wanafunzi wao katika vyuo vya elimu ya juu, ni rushwa ya ngono. Wadau wanasemaje?



**KELVIN MKINGA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

MIMI kwa mtazamo wangu ni kwamba wanafunzi wa kike wamekuwa ni chachu ya rushwa ya ngono kwasababu ya uvivu wao wa kusoma na kujikuta wakijirahisisha kwa wahadhiri ili wapate alama nzuri bila kuumiza kichwa.

Unakuta baadhi yao wanajihusisha na mambo ya kihuni, huku wakitaka wawe na ufaulu mzuri kwenye vyeti vyao.

Na wengine pia hufanya hivyo kutokana na ugumu wa maisha. Kinachotakiwa sasa ni wadau wa elimu kutoa mafunzo kwa wanafunzi, ambayo yanahusu madhara ya rushwa ya ngono.


Hatua hiyo inaweza kusaidia kupunguza tatizo hilo kama si kulimaliza kabisa. Kimsingi, chanzo kikuu cha rushwa ya ngono vyuo vikuu ni ukosefu wa maadili kwa baadhi ya wahadhiri na wanafunzi wenyewe, hali inayosababisha vita ya kukabiliana na tatizo hilo kutozaa matunda.

Lakini iwapo mafunzo yatatolewa, kuna uwezekano angalau wa kuokoa baadhi yao, na ikumbukwe kuwa kwenye msafara wa mamba, kenge nao huwa wapo.

Hivyo hata katika vyuo vikuu wapo wanafunzi waliokwenda kwa dhamira ya kusoma na wengine ndio hao ambao wanajihusisha na rushwa ya ngono ili kupata alama nzuri katika mitihani wakati hawana lolote kichwani.

Distributed via ippmedia

Wanafunzi wa aina hiyo ndio wanaojilengesha kwa wahadhiri na kugeuzwa kuwa wapenzi wao wanaowasaidia katika masomo au mitihani badala ya kujibidisha wenyewe.



**FATMA MALECHE (MDAU WA ELIMU, MKAZI WA DAR ES SALAAM)**

KWA kweli rushwa ya ngono ni tatizo kubwa katika vyuo vya elimu ya juu na sababu mbalimbali zinazochangia kuwapo kwa vitendo hivyo, ambavyo vinadhalilisha utu wa msichana au mwanafunzi, kwa kulazimishwa kufanya ngono bila ridhaa.

Ninasema bila ridhaa kwasababu kumwambia afanye kitendo hicho ndipo atimiziwe au apewe unafuu wa jambo fulani, ina maana amefanya bila ridhaa ili asaidiwe jambo fulani.

Hapa nitataja sababu chache zinazochochea vitendo vya ngono vyuoni, mojawapo ikiwa inachangiwa na baadhi ya Wahadhiri wasio na maadili, wanaendekeza ngono, mfumo mzima wa uwajibikaji wa baadhi ya wahadhiri ni kwamba huwa wanatumia vyeo vyao kama kinga kwa ajili ya kutimiza matakwa yao.

Na hiyo inachangia kuwafanya baadhi ya wanafunzi wa kike kuendelea kuwa waathirika kwa kushindwa kujikwamua katika mtego huo ambao ni hatari sana katika maisha. Sababu nyingine ni kwamba inachangiwa na wanafunzi wenyewe, kwani baadhi yao wanajilengesha wenyewe kuanzia kwenye mavazi na jinsi wanavyojiweka na kujikuta wakitamaniwa na walimu wao.

Ni wajibu wa wanafunzi wenyewe kutambua ni kwa namna gani mavazi na matendo yao yanaweza kuwafanya wawe waathirika wa rushwa ya ngono. Vilevile wahadhiri wanatakiwa kufuata maadili ya kazi.

Binafsi ninaamini kwamba hayo yakifanyika, hakutakuwa na tuhuma kuwa baadhi ya wanafunzi wa kike wanalazimika kutoa rushwa ya ngono ili wasaidiwe kufaulu katika masomo yao.



**DOREEN TUPPA (MHITIMU CHUO KIKUU SAUT MWANZA)**

HAPA ni muhimu tuelewe kwamba masuala ya ngono hayapo vyuoni tu bali hata mitaani, hivyo wazazi wana wajibu wa kuwasaidia watoto wao kwa kuwaelimisha ili wajue kuwa wanakwenda vyuoni kusoma, hivyo wanatakiwa kuzingatia masomo kwa kujibidisha badala ya kusubiri mteremko.

Kikubwa zaidi ni mtoto wa kike kuwa na msimamo, vinginevyo atayumbishwa na kujikuta kwenye hiyo rushwa ambayo mimi ninaiona kama inadhalilisha utu wa mwanamke. Wanafunzi wa kike wanatakiwa kutambua kuwa maisha vyuoni ni tofauti na yale ya sekondari, kwani ukiwa chuo mhadhiri ndiye anayeweza kuamua uhitimu chuo au la, hivyo baadhi ya wasichana wanajikuta wanaingia katika mtego wa rushwa ya ngono ili kutimiza malengo yao bila kutazama madhara.

Lakini wakiwa na msimamo wanaweza kusoma na kuhitimu bila kukutana na tatizo hilo. Rushwa ya ngono inafanyika vyuoni, kwasababu baadhi ya wanafunzi wa kike wanaamini bila kutoa hongo hiyo hawawezi kuhitimu vizuri katika masomo yao.

Ombi langu ni kwamba serikali ishirikiane kwa karibu na taasisi zinazopambana na rushwa ili kudhibiti vitendo viovu kama hivi, ambavyo vinachangia baadhi ya wanafunzi wa kike kutofikia ndoto zao katika elimu. Pia wanafunzi nao watambue kuwa maisha ya chuo si raha bali ni kujituma na hatimaye kufikia malengo.



**LOYCE KABUCHE (MWANAFUNZI CHUO KIKUU MZUMBE MOROGORO)**

SUALA hili ni la kujadili kwa umakini sana, kutokana na ukweli kwamba pande zote zina matatizo. Baadhi ya watu wamekuwa wakilaumu sana wahadhiri, lakini mimi ninagusa sehemu zote kwa kutambua kwamba hata baadhi ya wanafunzi wanachangia kuwapo kwa rushwa ya ngono vyuoni.

Kwa ujumla ni kwamba wanafunzi wa kike nao wanalaumiwa kwa kutumia jinsia yao kama kishawishi cha kuwatega wahadhiri kwa lengo la kupata alama bora. Sasa kwa kuwa wahadhiri nao ni binadamu wana udhaifu wao, hujikuta wakiingizwa kwenye mtego wa kufanya ngono na wanafunzi.

Hii yote inatokana na kutojituma katika masomo badala yake wanatumia miili yao kwa kukubali kuwa wapenzi wa wahadhiri wao ili kusaidiwa kitaaluma. Pamoja na hayo, nikumbushe kuwa rushwa ya ngono vyuoni sio msingi wa tatizo, bali msingi ni nidhamu ya kielimu inayodhaminiwa na mfumo mbovu wa kisiasa yaani demokrasia na ubepari wake, kwani udhaifu huo kwenye mfumo wa elimu hasa katika nchi za dunia ya tatu unaonekana katika sehemu hizi.

Mfumo wa uendeshaji wa masomo wa vyuo vikuu umejengwa katika hali mbovu na kutoa mwanya wa rushwa za ngono. Kuwekwa kiwango cha alama takriban 40 kuwa chini ya umiliki wa mkufunzi. Mfumo huu umewapa wakufunzi wengi wenye ulevi wa ngono kutumia upenyo huo kugawa alama hizo kwa wanafunzi wanaowataka kufanya nao zinaa.



**GERMANA MVUNGI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

NAKUMBUKA Novemba mwaka jana Mhadhiri wa Chuo Kikuu Dar es Salaam, Dk. Vicensia Shule aliweka wazi kuhusu vitendo vya rushwa ya ngono chuoni hapo.

Hii inaonyesha kuwa alikerwa sana na vitendo hivyo ambavyo vinamfanya mwanafunzi wa kike kuendelea kudhalilika kana kwamba hana uwezo wa kujitegemea katika masomo.

Kitendo cha mhadhiri huyo kuweka wazi mambo, kilitosha kuwa fundisho kwa wahadhiri wapenda ngono na walimu wengine wakiwamo wa shule za sekondari na msingi ili kuwaacha wasichana wasome.

Hata hivyo ninaamini tatizo la rushwa ya ngono bado lipo kuanzia shule za chini hadi vyuo. Inasikitisha jamii inaposikia kwamba kuna baadhi ya wahadhiri wanalaumiwa kwa kuwanyanyasa kijinsia wanafunzi wa kike kwa kuwaomba rushwa ya ngono au kuwawekea mazingira ya kuwataka kimapenzi kwa nguvu.

Lakini pia wasichana wanapaswa kujiuliza kwanini watafute alama za bure, kwanini usisome vizuri na wakubali matokeo ambayo watapata?

Ninaamini kwamba iwapo mwanafunzi atajiuliza hayo hawatakubali kujiingiza katika rushwa ya ngono, badala yake watajiheshimu na wanapojiheshimu si rahisi kusogelewa na wakware.



## HABARI MBEYA

# DC akemea ukatili dhidi ya watoto

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

MKUU wa Wilaya ya Chunya, Mhandisi Marypriscar Mahundi, amekemea vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ikiwamo ubakaji na utumikishwaji kwenye madini na shughuli za mashambani akidai vinawaharibia maisha.

Alikemea vitendo hivyo alipokuwa katika ziara ya kikazi kwenye Kata za Chokaa, Matundasi na Mamba ambako ndiko shughuli hizo zinafanyika zaidi na aliwatahadharisha wanaofanya vitendo hivyo kuwa watakabiliwa na mkono wa sheria.

Alisema vitendo vya ukatili vinavyofanyika zaidi wilayani humo ni ubakaji wa watoto na ulawiti unaoambatana na imani za kishirikina hasa kwa imani kuwa vinasaidia kupata bahati ya kupata madini kwenye migodi.

Mahundi aliwataka wananchi kuacha kuamini imani za kishirikina huku akiwatahadharisha waganga wa jadi wanaowadanganya wachimbaji akidai kuwa wao ndio wanaochochea vitendo hivyo kukithiri katika wilaya hiyo.

"Ni aibu kubwa sana maana unajiuliza huyu mtu anapata nini kwa huyo mtoto? Lakini pia hebu fikiria anayefanyiwa vitendo hivyo ni mtoto wako utajisikiaje? Tafadhari wananchi naomba tushirikiane kutokomeza vitendo hivi kwa kuwafichua wanaoshiriki," alisema Mahindi.

Alisema katika Kata za Chokaa na Matundasi ndiko vitendo vya ubakaji na ualawiti vimekithiri lakini katika Kata ya Mamba watoto wananyanyaswa kwa kutumikishwa kwenye mashamba ya tumbaku.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Chokaa, Samwel Komba alikiri kata yake kuwa miongoni mwa maeneo yenye matukio mengi ya ubakaji wa watoto kutokana na kuwa na madini.

Alisema vitendo hivyo vinakera na vinachafua wilaya nzima, hivyo akawataka wananchi kushirikiana na Serikali kuvitokomeza kwa kutoa taarifa za watu wanaoshiriki ili wachukuliwe hatua.

Vilevile, alisema watoto wanaotumikishwa kwenye migodi na mashambani wanakosa haki yao ya msingi ya kwenda shuleni na hivyo atakayekamatwa atachukuliwa hatua kali.

**"Ni aibu kubwa sana maana unajiuliza huyu mtu anapata nini kwa huyo mtoto? Lakini pia hebu fikiria anayefanyiwa vitendo hivyo ni mtoto wako utajisikiaje? Tafadhari wananchi naomba tushirikiane kutokomeza vitendo hivi kwa kuwafichua wanaoshiriki," alisema Mahindi.**

# Kiwanda matatani tuhuma kuzalisha mifuko ya plastiki

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

IKIWA ni miezi mitano sasa tangu serikali ipige marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki, kiwanda kimoja kijulikanacho kwa jina la Mbalizi Plastic LTD kinachomilikiwa na raia wa China mkoani Mbeya, kimenaswa kikiendelea na uzalishaji wa mifuko hiyo.

Kiwanda hicho kilinaswa mwishoni mwa wiki kwa ushirikiano kati ya maofisa wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Shirika la Viwango nchini (TBS) na Jeshi la Polisi.

Maofisa hao walifanya ziara ya kushtukiza katika kiwanda hicho kilichopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi na kunasa viroba 30 vya mifuko hiyo ikiwa imezalishwa na iko tayari kwenda sokoni.

Meneja wa Nemc Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Anord Mapinduzi, alisema ukaguzi huo ulikuwa ni ufuatiliaji wa utekelezaji wa agizo la serikali la kusitisha matumizi ya mifuko hiyo.

Alisema kiwanda hicho kimesajiliwa kwa ajili ya kuzalisha mifuko ya viroba ambayo inaruhusiwa, lakini baada ya kufuatilia walibaini kuwa kinazalisha pia mifuko ya plastiki na ndio maana waliamua kufanya ukaguzi wa kushtukiza.

"Tulipata taarifa za siri kuwa kiwanda hiki kinazalisha mifuko hii kwa 'odder' na kazi ya uzalishaji inafanyika usiku, tumekuja hapa na tumekuta kweli wana shehena hii na tayari kwa kuipeleka sokoni, sasa lazima sheria ichukue mkondo wake," alisema Mhandisi Mapinduzi.

Alisema kwa mujibu wa sheria kiwanda hicho kitatakiwa kulipa faini ya Sh. milioni 20 na kama watashindwa kulipa watapelekwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Mkaguzi Ubora kutoka TBS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Yekonia Sanga, alisema kiwanda hicho pamoja na kuzalisha mifuko ya viroba, lakini hakitambuliki na shirika hilo.

Alisema kutokana na kutotambuliwa na shirika lake, hivyo kuna utata wa ubora wa bidhaa zake na akawataka wananchi kuwa makini wanapozinunua kwa madai kuwa sheria inaruhusu mpaka mtumiaji kushughulikiwa.

Alisema kinachosimamiwa sasa hivi ni sheria mama ya Nemc pamoja na katazo la serikali juu ya matumizi ya mifuko hiyo na kwamba ukaguzi utaendelea kwenye viwanda vingine.

"Sheria inaruhusu mzalishaji, msambazaji na watumiaji wote kuchukuliwa hatua na kuna hatua mbalimbali za kuchukua ikiwa ni pamoja na kulipa faini, kupelekwa mahakamani ama vyote kwa pamoja, sasa tunawataka wananchi kuwa makini," alisema Mhandisi Sanga.

Mmiliki wa kiwanda hicho, Yong Le, alijitetea akidai kuwa mifuko hiyo aliizalisha kabla ya katazo la serikali na kwamba haisambazwi.

Alisema kwa sasa kiwanda chake kinazalisha mifuko halali, ambayo inaruhusiwa hivyo akaomba asichukuliwe hatua.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kulia), akikagua ubora wa nondo zinazotumika kwenye ujenzi unaoendelea wa jengo la wazazi la Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, kitengo cha wazazi Meta, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Upanuzi hospitali ya rufani kanda waanza

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SERIKALI imeanza upanuzi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani Mbeya Kitengo cha Wazazi Meta kwa kujenga jengo la ghorofa sita ili kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye wodi zilizopo ambazo ni chache.

Akizungumza wakati wa kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo hilo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema serikali imetoa Sh. bilioni nne kwa ajili ya kukamilisha jengo hilo na kwamba linajengwa kwa kutumia utaratibu wa akaunti ya dharura (Force account).

Alisema ujenzi wa jengo hilo unaenda vizuri na kwa mujibu wa mkataba linatakiwa likamilike baada ya miaka miwili na sasa hivi tayari mkandarasi amefikia ghorofa ya pili.

Chalamila alisema tangu hospitali hiyo ilipojengwa na wakoloni miaka ya 1950 hakuna jengo lingine lililojengwa mpaka serikali ilipoamua kujenga jengo hilo jipya.

"Kwa mujibu wa maelezo, majengo yetu ya zamani yana uwezo wa kuchukua wagonjwa 172, lakini hili peke yake litakuwa na uwezo wa kuchukua wagonjwa 204 hivyo kitengo hiki kitakuwa na uwezo wa kuchukua wagongwa 376," alisema Chalamila.

Alisema hospitali hiyo inahudumia mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ina watu wasiopungua 8,000,000 na ina madaktari bingwa wa kutosha kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wenye matatizo ambayo yanashindikana kwenye maeneo yao.

Alisema ujenzi wa jengo hilo, hospitali za wilaya, vituo vya afya kwenye kata na zahanati kwenye ngazi za vijiji ni juhudi za serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya.


Alimpongeza Mkurugenzi wa Hospitali hiyo pamoja na wasaidizi wake kwa kusimamia vyema ujenzi wa jengo hilo pamoja na majengo mengine likiwamo jengo la vipimo vya mionzi na kitengo cha watoto katika hospitali kuu.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha hizo ambazo alidai zitamaliza tatizo la msongamano wa wagonjwa ndani ya hospitali hiyo.

Alisema kwa sasa hospitali hiyo imeanza kuimarisha kila idara ili kila huduma inayotakiwa katika hospitali ya kanda ipatikane na kwamba anatamani hospitali hiyo iwe na huduma zote kama zinazopatikana katika Hospitali ya Taifa ya Mhimbili.

Alisema kwa sasa jengo la mionzi tayari limekamilika na baadhi ya vipimo vikubwa tayari vimeshawekwa kwa ajili ya kuanza kutoa huduma ikiwamo mashine ya CT-Scan ambayo ilikuwa haipatikani hospitalini hapo.

"Tunamshukuru mheshimiwa Rais kwa kutupatia fedha kwa ajili ya mradi huu mkubwa, tunaamini zitamaliza mradi wote na kwa viwango vinavyotakiwa, lakini tunawaalika wadau mbalimbali kushiriki kwenye ujenzi wa miradi kama hii," alisema Dk. Mbwanji.





# Waislamu watakiwa kutunza mazingira

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

KATIBU Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, amewataka viongozi wa dini ya Kiislamu kuwahamasisha waumini wao utunzaji mazingira na maliasili zilizopo nchini.

Dk. Bashiru alisema hayo alipokuwa akizungumza na viongozi wa dini, serikali pamoja na waumini wa dini ya kiislamu kwenye sherehe ya kuadhimisha kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) iliyofanyika kimkoa jijini Dodoma.

Aliwataka viongozi hao kutumia nafasi zao kuhakikisha wanatoa elimu hiyo kwa waumini ili kutunza mazingira na rasilimali zilizopo katika taifa.

"Tumieni nafasi zenu nyinyi viongozi wenzangu katika kuwaelimisha waumini kulinda mazingira na mali za Watanzania," alisema.

Aidha, aliwataka viongozi hao kuwekeza elimu ya dini kwa vijana, ili waipende na kuifuata kwa vitendo kiroho na kimwili.

Akizungumza kwenye sherehe hiyo pia amewataka viongozi hao kuisaidia serikali katika kukemea vitendo vya rushwa na ufisadi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema wao kama wabunge watahakikisha wanatimiza maelekezo ya Rais ili kuleta ufanisi wa maendeleo ya nchi.

Kaimu Katibu wa Bakwata Mkoa wa Dodoma, Twaha Mwanya, alisema moja ya changamoto ni maeneo ya yaliyowekwa kwa ajili ya uwekezaji hayajatengewa nyumba za ibada kama misikiti na makanisa.

**"Tumieni nafasi zenu nyinyi viongozi wenzangu katika kuwaelimisha waumini kulinda mazingira na mali za Watanzania," alisema.**

# Madiwani wakataa taarifa za h/shauri

**Peter Mkwavila, CHAMWINO**

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma , limekataa kupokea na kujadili taarifa zote za kamati za kudumu za halmashauri hiyo na kuagiza kuchukuliwa hatua za kisheria kwa mwandishi wa vikao (CC), Bernard Luhamu, wakimtuhumu kughushi saini za wenyeviti wa kamati.

Hatua hiyo inafuatia baada ya wenyeviti wote wa kamati za kudumu, ikiwamo ile ya Fedha, Uongozi na Mipango inayoongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Samwel Kaweya, kushangazwa na hatua ya makablasha hayo kuonekana kusaini kwa saini zao, wakati hawakuwahi kufanya hivyo.

Hayo yalijitokeza juzi katika kikao cha Baraza la Madiwani, kilichoketi kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji za kamati za kudumu kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Madiwani hao walimtuhumu mwandishi huyo kuwa alidiriki kulidanganya baraza kwa kughushi saini za wenyeviti wa kamati hizo za kudumu, huku wakitilia shaka baadhi ya vipengele vya taarifa iliyowasilishwa kikaoni hapo kunyofolewa.

Awali kabla ya madiwani hao kufikia uamuzi huo wa kuikataa taarifa hiyo, Diwani wa Kata ya Buigiri, Keneth Yindi, aliomba mwongozo, akihoji kutoonekana kwa baadhi ya taarifa.

Akijibu hoja ya mwongozo huo, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Elias Kaweya, alikiri kutoonekana kwa baadhi ya vipengele vilivyojadiliwa kwenye kamati ya fedha.

"Mwenyekiti niwe mkweli juu ya hili, mimi kama mjumbe wa kamati ya fedha kuna mambo tuliyajadili kule na yalitakiwa kuwasilishwa kwenye kikao hiki cha baraza, lakini havionekani."

Kutokana na maelezo hayo ndipo aliposimama Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Samweli Kaweya na kukiri kuwapo kwa tatizo hilo la baadhi ya taarifa kunyofolewa, huku akishangazwa na hatua ya taarifa hiyo kuonekana kusainiwa na yeye wakati hakuwahi kufanya hivyo.

"Mkurugenzi hata hii saini inaonekana ni ya yangu, lakini niseme kweli mimi sijawahi kuja kusaini hili kablasha kama taratibu zinavyota na nashangazwa na hiki kilichotokea humu, labda wenzangu katika kamati wao walisaini," alisema mwenyekiti huo.

Hata hivyo, Mwenyekiti huyo wa Halmashauri alitumia nafasi hiyo kuwahoji wenyeviti wa kamati za kudumu kama walihusika kusaini makablasha kama taratibu zinavyoagiza, ambapo kwa pamoja walikana.

Kutokana na mkanganyiko huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Athumani Masasi, alilazimika kumnyanyua mwandishi wa vikao ili kutoa ufafanuzi juu ya tuhuma za kughushi saini.

Akijibu tuhuma hizo mwandishi huyo wa vikao, licha ya kukiri kuwa utaaratibu huo umekuwa ukitumika mara nyingi kutokana na makubaliano kati yake na wenyeviti hao.

Akifafanua zaidi baada ya kikao kumalizika, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Masasi alionekana kushangazwa na uamuzi wa madiwani kwani hata kama walibaini kuwapo kwa kasoro walipaswa kuwasiliana na ofisi yake mapema na kurekebisha.

"Kama mlivyomsikia, pale hakuna fojali bali kilichotokea ni madiwani kutafuta sababu tuu, baada ya kutaka hoja ambazo hazikufuata taratibu ziingizwe kwenye ajenda za kikao," alisema.

Mapema kulionekana dalili za kuvunjika kwa baraza hilo kufuatia malumbano ya kikanuni kufuatia baadhi ya madiwani kutaka baadhi ya hoja zilizoibuliwa kwenye kikao cha chama kuingizwa kama ajenda katika kikao hicho.

Baadhi ya taarifa hizo ambazo madiwani walitaka ziingizwe kama ajenda kwenye kikao hicho ni azimio lao la kutaka taarifa ya fedha kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 700 za maendeleo ya upimaji ardhi kupitia kampuni ya LIC.

Nyingine ni taarifa ya baadhi ya watumishi wa halmashauri kujigawia kwa upendeleo viwanja 19 bila kufuata taratibu, pamoja na gari la halmashauri lililotolewa msaada na serikali ya Korea ya Kusini, kukamatwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ikidaiwa kukodishwa kifisadi, huku dereva aliyekuta akiendesha gari hilo si mtumishi wa umma.

Distributed via Inmedia



Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustafa Rajabu, akiwa amepanda ngamia, wakati akiongoza maandamano ya waumini wa Kiislamu kuadhimisha Siku ya Kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W), jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wabunge waziomba azaki kusaidia utafiti

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WABUNGE wameziomba asasi za kiraia (Azaki) kuwasaidia kufanya utafiti na uchambuzi wa sera ili ziwasaidie katika kuisimamia serikali, ikiwamo kutekeleza majukumu yao ya uwakilishi wa wananchi.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Seleman Kakoso, katika kikao cha pili cha mwaka kilichoandaliwa na muungano wa mashirika yasiyo ya kiserikali Tanzania (TANGO) baina ya wawakilishi wa azaki na wenyeviti, makamu mwenyeviti na makatibu wa kamati za kudumu za Bunge kilichofanyika jijini hapa.

Kakoso, alisema kutokana na azaki, kufanya kazi na watu katika maeneo mbalimbali hivyo ni vema kushirikiana ili kushughulikia masuala yanayowahusu wananchi kiufasaha.

Alisema ni vema kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuliwezesha Bunge kuelewa vyema mazingira na kazi za azaki hizo ili kushauri ipasavyo na kurekebisha pale inapohitajika kufanya.

"Ni vema azaki na wabunge kufanya kazi kwa pamoja kwa sababu itarahisisha kuweza kuibua changamoto za sehemu husika na kulifanyia kazi," alisema Kakoso.

Alisema zipo njia mbalimbali ambazo zinatumika katika ushirikiano baina ya Bunge na Azaki pamoja na wadau wengine ambazo zinaweza kuleta tija kwa taifa endapo tu majadiliano yatakuwa na afya.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TANGO, Ngunga Tepani, alisema wamekubaliana kuhusiana na upatikanaji wa taarifa za miswaada katika wavuti.

Alisema wakifanya hivyo, itawasaidia kupata taarifa mbalimbali za Bunge ambazo wanaweza kulifanyia kazi ipasavyo na kuwaelimisha wananchi juu ya nini kinaendelea katika taifa lao.

Alisema wamekubaliana kutekeleza majukumu mbalimbali kiufasaha ambayo yanawahusu na kuyatolea majibu kwa pamoja pale inapobidi kufanya ili kuhakikisha wanafikia malengo waliojiwekea katika kuleta maendeleo.

Naye Michael Chikokoto kutoka Idara ya Kamati za Bunge, alisema jukumu la Bunge ni kuisimamia na kuishauri serikali katika mambo mbalimbali ya maendeleo ya wananchi.



# Wapewa mbinu za kupunguza talaka

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MWENYEKITI wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Jaji Mshibe Ali Bakari, amezishauri jamii kuacha kukwepa majukumu ya malezi ili kupunguza migogoro ya ndoa na wimbi la ndoa kuvunjika na kutoa talaka.

Akizungumza katika mafunzo ya makadhi wa wilaya kuhusu uendeshaji wa kesi na utoaji wa hukumu kwa misingi ya Kiislamu, alisema kitendo cha kwenda mahakamani kudai talaka si suluhisho la kutatua kero za kifamilia bali linaongeza mivutano ya kijamii hasa kwa malezi ya watoto.

Alieleza kuwa ndoa nyingi zinazovunjika zimekuwa zikileta athari kubwa kwa watoto kutokana na kukosa malezi ya wazazi wawili.

Alieleza kuwa ndoa hizo zinapovunjika kinababa hukwepa kutoa matunzo ya watoto na mzigo huo huwaelemea kinamama zaidi.

Alieleza kuwa hali hiyo husababisha watoto hao hufanyiwa vitendo vya udhalilishaji kutokana na kutokua na usimamizi.

Jaji Mshibe aliwataka viongozi wa dini kubeba dhima waliyokuwanayo kuiunganisha jamii hasa katika kutatua migogoro ya ndoa kwa misingi ya kimaadili ya dini na utamaduni kabla ya kuzifikisha kesi mahakamani.

Akiwasilisha mada kuhusu uandishi wa hukumu Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar, Abdulhakim Ameir Issa, alisema ni lazima makadhi kufahamu wanafanyakazi ya umma katika kuiambia jamii kuhusu uamuzi wa kesi mbalimbali kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Kwa upande wao makadhi hao walisema kuwa watahakikisha wanayafanyia kazi mafunzo waliyopewa ili kupunguza wimbi la talaka linalosababishwa na migogoro ya ndoa.

Jumla ya mada mbili ziliwasilishwa ikiwamo uandishi wa hukumu katika mkutano huo uliowakutanisha makadhi wa wilaya kutoka Unguja na Pemba.

Waandaji walikuwa ni Mahakama Kuu Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

## Wajasiriamali waanza kusindika matunda

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAKAZI wa Mkoa wa Kusini Unguja wameelezea furaha ya kuanzishwa kiwanda cha kusindika matunda katika Kijiji cha Mtule mkoani humo, wakisema kuwa ni mkombozi wa wakulima na wajasiriamali.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud alipotembelea kiwanda hicho kwa lengo la kufuatilia malengo na changamoto zilizopo kiwandani hapo.

Alisema kiwanda hicho kitakapoanza kazi kitatoa fursa mbalimbali ikiwamo ajira kwa wakazi wa mkoa huo kama wakulima kuuza bidhaa zao.

Aliwapongeza waanzilishi wa kiwanda hicho kwa kutekeleza azma ya serikali zote mbili ya Zanzibar na Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania ya kuwa na uchumi wa viwanda kutokana na kuwa viwanda vinavyotoa nafasi nyingi za ajira.

Alieleza kuwa uwepo wa kiwanda hicho kutaongeza kasi ya uzalishaji kwa wakulima wa mkoa huo.

Alisema miongoni mwa wateja watakaotumia bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hicho kuwa ni watalii na kuahidi siku atakayokutana na wawekezaji wa sekta ya utalii atawaomba wanunue bidhaa zinazozalishwa hapo kwa ajili ya matumizi yao ya kihoteli.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Idrisa Kitwana Mustafa, alisema wilaya hiyo kupitia asasi na jumuiya zilizomo wilayani humo imeanza na wataendeleza kuanzisha viwanda ili azma ya serikali ya kufikia uchumi wa kati wa viwanda itimizwe.

Kwa upande wao wanachama wa jumuiya ya ushirika wa Mtule ambayo ndiyo waanzilishi wa kiwanda hicho, walisema wameshawawezesha wanachama wengi wa jumuiya hiyo kwa kuwapatia mikopo na hadi sasa Sh. milioni 30 zimeshatolewa.

Walisema licha ya kuwawezesha wanachama wao changamoto kubwa ni wadau wao hao kutorejesha fedha kwa wakati.



Wakulima wa kaya maskini wa vijiji vya Mpapa na Umbuji, Mkoa wa Kusini Unguja, wakivuna vitunguu maji jana, kwenye mashamba waliyolima baada ya kuwezeshwa na mfuko wa Tasaf. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanakaya maskini wafanya maajabu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANANCHI wanaohudumiwa na mpango wa kupunguza umaskani kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) wamebuni miradi ya kipekee iliyosaidia kujiingizia kipato na kubadilisha maisha yao.

Mkurugenzi Uratibu wa Shughuli za Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Khalid Bakari Hamrani, alieleza hayo wakati wa uvunaji wa vitunguu maji.

Mradi huo uliwahusu wananchi wanaonufaika na mpango huo katika Vijiji vya Mpapa na Umbuji Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja.

Mkurugenzi huyo aliwapongeza wananchi hao kwa jitihada zao za kuendeleza mradi wa kilimo cha mboga ambao umekuwa ukiwasaidia kuinua kipato na kukabiliana na hali ngumu ya umaskini.

Alisema ni jambo linalotia moyo kwa viongozi wa serikali kwa kuona kwamba wananchi wamekuwa na mwamko wa kulima na kuzalisha bidhaa ambazo awali hazikuwa zikilimwa Zanzibar.

"Zanzibar tulikuwa hatulimi vitunguu maji tulitegemea zaidi Tanzania Bara, lakini hivi sasa bidhaa hii inapatikana hapa hapa kwetu ni jambo la kufurahisha," alisema Hamrani.

Alieleza kuwa hapo awali jamii ya Zanzibar ilikuwa haina uelewa kuhusu kilimo hicho cha vitunguu na ilijenga dhana ya kwamba zao hilo huota katika ardhi maalum.

Alisema mambo yamebadilika baada ya kupata elimu ya kilimo na sasa wameondoka na fikra hizo, wananchi wanalima zao hilo na mazao mengine ambayo awali yalikuwa hayalimwi.

Aidha, Mkurugenzi aliwahakikishia wananchi hao kuwa hivi karibuni Ofisi ya Tasaf itaanza rasmi zoezi la kuwalipa wananchi fedha zao kabla ya mpango mpya wa awamu ya tatu kipindi cha pili hakijaanza utekelezaji wake.

Aliwataka walengwa hao kuendeleza kilimo hicho ambacho kimekua na faida kubwa ili kujikwamua kiuchumi na kuondokana na hali ya utegemezi.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wenzake katika mradi huo, Zainab Hassan Ameir, alisema kupitia mradi huo wa kilimo cha vitunguu maji, wanajikimu kimaisha na kufikia azma ya serikali katika kupambana na umaskini.

Zainab alisema kuwa wananchi wa Zanzibar si maskini ila jambo la msingi linalohitajika kwao ni kupatiwa elimu pamoja na usimamizi imara wa miradi mbalimbali.

"Nawaomba wananchi wa maeneo mengine hasa wanawake kuiga mfano wetu kwa kuanzisha miradi kama hiyo katika sehemu zao ili waweze kunufaika kuliko kukaa nyumbani bila ya kuwa na kazi yoyote," alisema.

Mratibu wa Tasaf Unguja, Makame Haji Ali, alisema serikali itaendeleza mpango wake wa kuwafikia wananchi katika shehia zote Unguja na Pemba kwa kuwapa elimu ya uendelezaji wa miradi yao walioianzisha.

Alisema kuwa, kutokana na matokeo mazuri yaliopatikana katika majaribio ya kulima vitunguu maji katika ardhi ya Zanzibar ofisi yao itaangalia uwezekano wa kufanya majaribio ya kulima viazi mbatata ikiwa ni sehemu ya kuendeleza ubunifu kwa walengwa wa mpango huo.

Mratibu Makame alitoa wito kwa maofisa ugani waliopo katika kila wilaya kuweka utaratibu wa kuwapitia wakulima na wafugaji kwa kuwasikiliza changamoto zao zinazowakabili na kuzipatia ufumbuzi ili walengwa hao waweze kupata faida zaidi juu ya miradi wanayoiendeleza.

Kwa upande wake kiongozi wa wanakaya maskini wa Kijiji cha Mpapa, Abdi Mussa Khamis, alisema mradi wa vitunguu maji umekuwa na tija kutokana na uzalishaji kuongeza kila kipindi cha mavuno na kupata vitunguu vyenye ubora zaidi.

Alizitaja changamoto kubwa zinazowakabili kuwa ni mabadiliko ya tabianchi kutokana na kubadilika kwa taratibu za mvua na misimu.

# Viongozi Amcos watiwa mbaroni

Na Rose Jacob, MWANZA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) wilayani Sengerema mkoani Mwanza, inashikilia viongozi 11 wa vyama vya ushirika kwa makosa ya ubadhirifu wa fedha.

Viongozi hao wanadaiwa kufanya ubadhirifu wa fedha kiasi cha Sh. 12,415,000 kwa kutowalipa wakulima 120 fedha zao za mauzo ya pamba, baada ya kampuni za ununuzi kulipa fedha zote.

Mkuu wa Takukuru mkoani Mwanza, Emmanuel Stenga, alisema viongozi hao ni Benard Magongo, Godfrid Bota na Samweli Mahinduka wote wa Amcos ya Kasisa na katibu wa Amcos ya Karumo, Paschal Malifefha.

"Wengine ni Lucas Manyecha wa Amcos Kasungamile tawi la Nyantakubwa, Honorius Butarutsi na Godfrey Lutanagi mjumbe wa bodi na mwenyekiti wa Amcos ya Sima, Charles Gogomoka, Alexander Shabo katibu, Tereza Mhangwa mjumbe wa bodi na Sylvester Malugu katibu wa Amcos ya Mami," alisema Stenga.

Aidha, Stenga alisema viongozi hao wamekiuka kifungu cha 28 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11ya mwaka 2007 na kwamba pamoja na kushikiliwa na Takukuru, tayari wamerudisha Sh. 6,247,600 ambazo zitalipwa kwa wakulima.

**"Wengine ni Lucas Manyecha wa Amcos Kasungamile tawi la Nyantakubwa, Honorius Butarutsi na Godfrey Lutanagi mjume wa bodi na mwenyekiti wa Amcos ya Sima, Charles Gogomoka...**

# RC ataka watumiaji Bandari Kigoma kufuata utaratibu

Na Felix Andrew

WATUMIAJI wa Bandari ya Kigoma na mpaka wa Manyovu mkoani humo, wametakiwa kutambua kuwa wao ni sehemu muhimu katika kuendeleza sekta binafsi inayochangia uingizaji wa mapato, ajira na kukuza uchumi wa nchi.

Kutokana na hali hiyo, wanapaswa kufuata taratibu zinazowekwa na serikali ili kuepuka usumbufu na hasara inayoweza kujitokeza kwa kutofuata utaratibu.

Hayo yalielezwa hivi karibuni na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali mstaafu Emmanuel Maganga, wakati wa ufunguzi wa semina ya wazalishaji, wasindikaji wa bidhaa pamoja na watumiaji wa Bandari ya Kigoma na mpaka wa Manyovu, iliyofanyika mkoani Kigoma.

Akisoma hotuba ya ufunguzi kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Kaimu Katibu Tawala, Uchumi na Uzalishaji, Dk. Vedast Makota, alisema elimu itakayotolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) itawawezesha washiriki kujua taratibu za kufuatwa wakati wa uingizaji na uthibitishaji wa bidhaa pamoja na changamoto zinazohusiana na mifumo na taratibu husika.

"Waalikwa wote ninawaomba mshiriki vyema ili kuweza kuboresha mifumo ya kiutendaji katika taasisi na serikali kwa ujumla kwani lengo la semina hii ni kuwapatia elimu washiriki juu ya taratibu na mifumo ya ukaguzi wa bidhaa mbalimbali kabla ya kuingizwa nchini yaani 'Pre-shipment Verification of Conformity'(PVoC), ukaguzi wa bidhaa baada ya kuwasili nchini 'Destination Inspection' (DI) na uthibitishaji wa bidhaa zinazozalishwa nchin," alisisitiza.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora, Gervas Kaisi, akimkaribisha mgeni rasmi kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, alisema ili kwenda sambamba na mikakati ya kitaifa, TBS imeendelea kutoa semina kama hizi kwa wazalishaji na waagizaji wa bidhaa mbalimbali zitokazo nje katika Mikoa wa Dar es Salaam, Mwanza, Tanga na Kilimanjaro ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na viwango.

Alisema kwa kuzingatia Kifungu cha 36 cha Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009, serikali ilipitisha Kanuni za Uthibiti wa Shehena - The Standards (Compulsory Batch Certification of Imports Regulations) kupitia Notisi ya Serikali Na. 405 ya Desemba 25, 2009.

Kaisi alisema kanuni hizo ziliipa TBS mamlaka ya kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingia nchini kabla ya kusambazwa kwenye soko la ndani, hivyo waagizaji wa bidhaa wanapaswa kufanya biashara bila kukinzana na kanuni zilizopo.

Alisema mbali na kanuni hizo, Februari 01 mwaka 2012, TBS ilianzisha mfumo wa ukaguzi wa bidhaa kabla ya kusafirishwa kuja nchini (PVoC) kama mpango wa udhibiti ubora wa bidhaa katika nchi zinakotoka ambao unasaidia katika kutatua changamoto zilizokuwapo wakati bidhaa zilipokuwa zinakaguliwa baada ya kufika nchini.

Alizitaja changamoto zilizokuwapo ni ucheleweshaji wa kuondosha mizigo bandarini, kuwapo kwa waagizaji wa bidhaa kutoka nje wasio waaminifu wanaopitia njia zisizo rasmi (njia za panya) na kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kupimia kila bidhaa inayoingizwa hapa nchini.

Kaisi alisema mpango wa udhibiti ubora wa bidhaa unaongozwa na kanuni ya uingizaji wa bidhaa hapa nchini na upo kwa mujibu wa Kifungu cha 4 (1) (s) cha Sheria ya Viwango Na. 2 ya 2009.



Wafanyabiashara wa matunda katika Soko la Buguruni jijini Dar es Salaam, wakiwa wamepanga bidhaa zao chini katika mazingira yasiyo salama kwa afya za walaji, kutokana na kuzingirwa na matope, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kifaa cha kisasa kukabili uhaba wataalamu maabara

Na Romana Mallya

TAASISI ya Afya Ifakara (IHI) kupitia kituo chake cha Bagamoyo, katika kukabiliana na uhaba wa wataalamu wa maabara wa uchunguzi wa magonjwa, imeamua kubuni kifaa cha adubini cha kisasa ambacho kinajiendesha chenyewe.

Injinia wa Mazingira kutoka IHI, Bagamoyo, Joram Mbuda, aliyasema hayo juzi baada ya waandishi na wahariri kutembelea maabara ya IHI iliyopo ndani ya Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo.

Ziara hiyo ilifanyika baada ya kundi hilo kupatiwa mafunzo na taasisi hiyo kuhusu utafiti wanazozifanya ikiwa ni pamoja ufugaji wa mbu ambao wanatumika kwa ajili ya kuwatafiti ili kubaini tabia zao na dawa gani ambayo inaweza kuwaua.

Akizungumza na vyombo vya habari ndani ya maabara ya taasisi hiyo, Mbuga alisema kwa sasa kuna uhaba wa wataalamu wa maabara wa kufanya uchunguzi wa malaria.

"Kwa mfano vituo vyetu ukifanya ukaguzi unakuta kituo kimoja kinapokea wagonjwa 60 hadi 120 kwa siku ukienda vijijini na baadhi ya hospitali za wilaya, unakuta kila zamu kuna wafanyakazi wawili.

"Kwa kawaida ukifanya uchunguzi wa magonjwa kwa kutumia adubini zilizopo sasa ambazo zinamlazimu mtu kuchungulia sampuli za vipimo vya wagonjwa 60 au 120 ni ngumu. Viwango vya Shirika la Afya Duniani, vinataka mtaalamu mmoja asome sampuli 49."

Alisema taasisi hiyo ya Ifakara imeamua kuunda kifaa ambacho kinajiendesha chenyewe kwa kutumia lugha ya kompyuta kwa kukiambia kwamba kitembee kwa namna fulani.

"Mfano ukichukua sampuli ya mtu ili kuipima kujua kama ana malaria ama la, unaiweka eneo maalum katika kifaa hiki kisha mtaalamu wa maabara atatumia kompyuta kusoma sampuli hiyo, kisha ataangalia kama seli zinaonekana vizuri, akishajiridhisha atabonyeza kwenye kompyuta kukiarifu kifaa hiki kipige picha 100 bila kuweka nafasi.

"Tunataka licha ya kujiendesha chenyewe kiwe na uwezo wa kutambua yaani kikiona mdudu wa malaria kimtambue na kuhesabu, kwa sasa tupo katika hatua ya kupata takwimu za kutosha, kwa sababu ili itambue lazima ukifundishe ili kiwe na takwimu."

Alisema kifaa hicho kina programu maalum ambazo kinaweza kupiga picha na kuandika yale ambayo yameonekana kwenye vipimo.

"Mradi huu unashirikisha taasisi nne ambazo mbili ni za Tanzania ikiwamo IHI na nyingine ni vyuo vikuu viwili vya nchini Uingereza," alisema.

Katika ziara hiyo, waandishi na wahariri walitembelea na kujionea mashine mbalimbali zilizopo kwenye taasisi hiyo za kupima kifua kikuu, figo na ini na nyingine ya kufanya uchunguzi wa damu.

HABARI KIMATAIFA

# Rwanda waua wawili mpakani na Uganda

**KIGALI,** Rwanda

JUMAPILI iliyopita polisi nchini Rwanda wanadaiwa kuwaua raia wawili wa Uganda baada ya kuvuka mpaka kuingia nchini humo na kuwashambulia maofisa wengine wa jeshi hilo waliokuwa karibu na mpaka Wilaya ya Nyagatare.

Aidha, kufuatia tukio hilo, polisi wa Uganda walisema wanafanya uchunguzi wa vifo vya wafanyabiashara Job Ebidishanga (32) na Bosco Tuheirwe (35) walipigwa risasi na polisi huku wenzao wengine watatu walitoroka kurudi Uganda.

Polisi walisema kuwa "watu waliokuwa wakivuka kwa magendo waliwashambulia maofisa wa polisi nao walichukua hatua za kujihami kwa kuwafyatulia risasi na kuwaua.

Juma lililopita, Havugimana Peter w'imyaka (26) raia wa Rwanda, alipigwa risasi kwenye bega na mwenzake aliyefahamika kwa jina la Muhirwa alipigwa kifuani walipovuka mpaka kuingia Rwanda wakiwa na viazi vitamu kutoka Uganda.

Havigimana alitoroka na kurudi Uganda na kupatiwa matibabu huku mwenzie, akiwa amejeruhiwa vibaya alibaki Rwanda, msemaji wa polisi nchini Uganda aliiambia BBC.

**Joto la kisiasa limekuwapo tangu mwanzoni mwa mwaka huu na limeathiri maisha ya watu kijamii na kiuchumi katika mataifa hayo jirani.**

Wiki mbili zilizopita, wanawake wawili raia wa Rwanda waliuawa katika Wilaya ya Nyagatare Kaskazini mwa Rwanda, kwa madai ya kukamatwa wakivusha bidhaa kwa magendo kutoka Uganda na kujaribu kuwakimbia polisi.

Tangu Februari mwaka huu, mvutano kati ya Rwanda na Uganda umesababisha mamlaka za Rwanda kuzuia raia wa nchi hiyo kuvuka mpaka kuingia nchini Uganda, eneo ambalo biashara ya mpakani kati ya nchi hizo mbili imeshamiri.

Tangu wakati huo, raia kadhaa wa Rwanda wameuawa, wakijaribu kuvusha bidhaa kwa njia ya magendo kutokea Uganda kinyume na marufuku iliyowekwa, polisi walisema wanafikia hatua hiyo kwa kuwa watu hujaribu kupambana na polisi.

Mwezi Agosti, Raisi wa Rwanda, Paul Kagame na Yoweri Museveni wa Uganda walikubaliana kumaliza mzozo wa kisiasa ambao umeathiri maelfu ya watu wa pande mbili hizo.

Raisi Yoweri Museveni wa Uganda na Paul Kagame wa Rwanda walisaini makubaliano ya amani katika mji mkuu wa Angola, Luanda kumaliza uhasama uliopo kati ya mataifa hayo jirani. Walifikia makubaliano hayo katika mkutano wa pili huko Luanda mbele ya maraisi wa Jamhuri ya Kidmeokrasi ya Congo, Angola na rais wa Congo Brazaville waliokuwa wapatanishi katika mzozo huo.

Joto la kisiasa limekuwapo tangu mwanzoni mwa mwaka huu na limeathiri maisha ya watu kijamii na kiuchumi katika mataifa hayo jirani.

Maofisa nchini Rwanda wameishutumu Uganda kwa kuwafunga na kuwatesa kinyume cha sheria raia wake nchini Uganda, wakati Uganda nayo inaishutumu Rwanda kutekeleza ujasusi katika ardhi yake.

"Tutashughulikia matatizo haya yote". Raisi Kagame aliwaambia waandishi wa habari baada ya kusaini makubaliano hayo.

Makubaliano hayo yalifikiwa baada ya "jitihada zilizoidhinishwa na Angola kwa usaidizi wa Congo" kwa mujibu wa Ikulu ya Angola.

Viongozi hao wawili walikubaliana kutilia mkazo kutatua mzozo wowote baina ya mataifa yao kwa njia ya amani shirika la habari nchini Angola, Angop liliripoti. **BBC**

Distributed via ippmedia



Agosti mwaka huu Marais Yoweri Museveni wa Uganda (kushoto) na Paul Kagame wa Rwanda walitiliana saini mkataba wa kumaliza mzozo wa mipaka yao. **PICHA: IKULU RWANDA**

# Mkutano maendeleo ya watu waanza

**NAIROBI,** Kenya

MKUTANO wa kimataifa kuhusu masuala ya idadi ya watu na maendeleo duniani ( ICPD25) unatarajiwa kuanza leo Jumanne jijini Nairobi.

Jana, maelfu ya wajumbe kutoka mataifa mbalimbali duniani walikuwa wamekusanyika jijini Nairobi nchini Kenya, kuhudhuria mkutano wa siku tatu, unaoanza leo kujadili masuala ya idadi ya watu na maendeleo.

Idadi kubwa ya wajumbe hao ni vijana, lakini pia mkutano huo unatarajiwa kugusia masuala yanayowaathiri vijana hasa afya, mapenzi (uhusiano) na suala la kupanga uzazi.

Viongozi wa Kanisa Katoliki walishtumu hatua ya Kenya kukubali kuwa mwenyeji wa mkutano huo na kusema kuwa kanisa hilo halitahudhuria mkutano huo.

Rais wa muungano wa mashirika ya kiraia nchini Kenya Suba Churchil, alisema baadhi ya watu hawajaelewa kiini cha mkutano huo.

Wadadisi walisema idadi ya watu barani Afrika inakuwa kwa kasi ambayo kufikia mwaka 2050 itakuwa imeongezeka maradufu ya ilivyo sasa, huku asilimia 40 ya watu masikini zaidi duniani wakihofiwa kuishi kwenye mataifa mawili tu ya bara hilo. **REDIO UFARANSA**

## FDLR wapata pigo kubwa

**KINSHASA,** Congo

JESHI la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo limetangaza kumuua Juvenal Musabimana, kiongozi mwengine wa juu wa kundi la waasi wa Rwanda la FDLR, mashariki mwa nchi hiyo.

Miezi miwili baada ya kifo cha Sylvestre Mudacumura, (kiongozi wa kijeshi wa kundi la FDLR), jeshi la DRC lilitangaza kifo cha kiongozi mwingine wa kihistoria wa kundi la waasi wa Rwanda, anayejulikana kwa jina la "Jenerali Jean Michel Africa".

Jenerali Jean Michel Africa, ni mmoja wa viongozi wa juu wa moja ya makundi ya RUD (makundi yaliyojitenga na FDLR), ambaye aliuawa. Juvenal Musabimana, anayejulikana zaidi mashariki mwa Kongo kwa jina la "Jenerali Jean Michel Africa," aliuawa akiwa pamoja na walinzi wake wanne.

Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, limetangaza kumuua Juvenal Musabimana, kiongozi mwengine wa juu wa kundi la waasi wa Rwanda FDLR, mashariki mwa nchi hiyo.

Miezi miwili baada ya kifo cha Sylvester Mudacumura aliyekuwa kiongozi wa kijeshi wa kundi la FDLR, jeshi la DRC limetangaza kifo cha kiongozi mwingine wa kihistoria wa kundi la waasi wa Rwanda, anayejulikana kwa jina la "Jenerali Jean Michel Africa".

Jenerali Jean Michel Africa, ni mmoja wa viongozi wa juu wa moja ya makundi ya RUD makundi yaliyojitenga na FDLR ambaye aliuawa.

Juvenal Musabimana, anayejulikana zaidi mashariki mwa Kongo kwa jina la Jenerali Jean Michel Africa, aliuawa akiwa pamoja na walinzi wake wanne.

Ofisa mwandamizi wa jeshi la DRC alibaini kwamba kijiji cha Binza, ambako kiongozi wa RUD aliuawa, ni mbali na mpaka wa Rwanda. "Vipi jeshi la Rwanda (RDF) linaweza kuwa upande huo," ofisa huyo mwandamizi wa jeshi la DRC alihoji.

Mmoja wa wasemaji wa jeshi la DRC alithibitisha kwamba Jean Michel Africa aliuawa katika mapigano makali kati ya FARDC na waasi. **REDIO UFARANSA**



Mwili wa Sylvestre Mudacumura, baada ya kupigwa risasi. **PICHA MTANDAO**

# Mbunge ataka uchunguzi wa safari za wabunge

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Nkasi Kaskazini (CCM), Ally Kessy, amesema kuna haja ya kuanza kuchunguza safari za wabunge wanapokwenda nje ya nchi, kwani wengi wao wanafuata posho kuliko maslahi ya Taifa.

Amesema mfano mzuri ni hivi sasa wabunge wengi wamejitokeza kwa wingi katika kufanya mazoezi wakijua kuna safari ya kwenda nje ya nchi ambayo inaposho kubwa.

Kessy aliyasema hayo jana bungeni wakati akichagia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2020/21.

Kessy aliwataka wabunge wawe na moyo wa kumsaidia Waziri wa Fedha kuhusu matumizi.

Alisema wabunge wengi hawaendi katika mazoezi, na kwamba mara chache sana wanakwenda kwenye mazoezi wakisikia kuna safari kwa sababu wanafuata maslahi, na hawaoni huruma wananchi waliowaacha majimboni wakiwa na shida za maji.

"Leo nimeshuhudia, wamesikia kuna safari ya kwenda Uganda wamejazana kule kwa makundi, si kinamama wala kinababa, mimi nimewaambia kuwa naenda kuwachafua bungeni, mmezidi kama sisi ni muhimili wa Bunge lazima tuchunguze safari za wabunge wanapokwenda nje watatuletea aibu kubwa," alisema na kuongeza:

"Huwezi kwenda kucheza mpira huna mazoezi... hii lazima tuchunguzane ndugu zangu, sio tunapiga kelele hatuna maji hatuna barabara wakati nyie mnatanua, mnakwenda kustarehe huko hamna faida yoyote kwenda nje."

Akilitolea ufafanuzi suala hilo, Spika Job Ndugai, alisema ni kweli kutakuwa na safari ya wabunge kwenda Uganda kushiriki katika michezo.

Alisema wataufanyia kazi ushauri wa mbunge Kessy, na kwamba watakuwa makini katika kuchagua wabunge.

"Tunajua kinachoendelea, nani afanye mazoezi nani hafanyi, niwaombe wabunge tujenge utamaduni wa kuhudhuria mazoezi kwani tukifanya vizuri ni sifa kwa Taifa, ni bora tusiende kuliko kwenda na watu ambao hawafanyi mazoezi, mbona Mama Salma Kikwete anajitahidi nyie wengine vipi?" Alihoji Spika Ndugai.



Distributed via ippmedia

Meneja Mawasiliano wa Kampuni ya Bima ya Jubilee, Angela Tungaraza (kulia), akimsaidia kupata vipimo vya damu mmoja wa watoto wa kituo cha kulela watoto yatima cha Umra Orphange Centre, Hassani Hijja, katika hafla ambayo Jubilee Insurance walipima afya watoto hao kwa kuchukua vipimo vya malaria, wingi wa damu, meno pamoja na macho ikiwa ni sehemu ya majukumu yao ya kusaidia jamii. **NA MPIGAPICHA WETU**

## TCAA yasaini mikataba 12 ya kibiashara

**Na Beatricr Moses**

MAMLAKA ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), imeingia mikataba 12 ya kibiashara ya kimataifa, hatua ambayo inatajwa kuwa inaweza kusaidia Shirika la Ndege nchini (ATCL) kujitanua kwa kuongeza safari za kimataifa.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, Hamza Johari, alipokuwa akielezea mafanikio waliyoyapata tangu mwaka 2015 hadi 2019, na kutaja baadhi ya nchi walizoingia nazo mikataba ni China, India, Uturuki, Thailand, Uingereza, Marekani , Ghana na Singapore.

Alisema kusainiwa kwa mikataba hiyo ni miongoni mwa mafanikio yanayoweza kutajwa kwa kuwa imewekeana kutokana na TCAA kufanikiwa kukua katika viwango vya kimataifa na kuwa wamepanda kutoka asilimia 38 hadi asilimia 60.

Johari alisema mafanikio hayo yanatokana na TCAA kujipanga vyema katika kuhakikisha wanasimamia na kudhibiti mifumo, sheria, taratibu na kanuni kulingana na taratibu zinavyotakiwa.

Alisema utekelezaji wa mradi wa rada unaogharimu Sh. bilioni 67.3 inasaidia kupata taarifa za ndege zote zinazoingia nchini, hivyo kuboresha mapato.

"Hali ya mapato TCAA imeimarika sana kutoka Sh. bilioni 44.7 mwaka 2015 hadi Sh. bilioni 73 mwaka 2019, tunatarajia yatapanda hadi kufikia Sh. bilioni 80.2 mwaka 2020," alisema mkurugenzi huyo.

Alibainisha kuwa mapato mwaka 2016 yalikuwa Sh. bilioni 48.4, mwaka 2017 Sh. bilioni 63 na mwaka 2018 ilikuwa Sh. bilioni 66.3.

## JPM abatilisha ufutaji shamba

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amebatilisha pendekezo la kufutwa shamba lenye ukubwa wa ekari 1,000 lililopo Kidunda wilayani Mvomero mkoani Morogoro linalomilikiwa na Rusimbi.

Uamuzi wa Rais Magufuli kubatilisha ufutaji shamba hilo unatokana na kubainika kuwa pendekezo lililowasilishwa la kufutwa shamba hilo kwa madai ya kutoendelezwa kutokuwa za kweli na ulilenga kumdhulumu mmiliki wake.

Akitangaza uamuzi huo wa Rais jana wilayani Mvomero, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema baada ya kufuatilia mashamba yaliyopendekezwa kufutwa, Rais Magufuli alibaini taarifa alizopelekewa za kufuta shamba Cecilia hazikuwa sahihi, hivyo kuamua kubatilisha pendekezo lililowasilishwa kwake na kumpatia haki yake mmiliki.

Kufuatia hali hiyo Waziri Lukuvi aliwaonya maofisa ardhi nchini kuhakikisha wakati wa kufanya ukaguzi/upekuzi wa mashamba yasiyoendelezwa wanazingatia haki pamoja na kufuata sheria badala ya kufanya kazi hiyo kwa upendeleo au kumwonea mtu.

Kwa upande wake Cecilia George Rusimbi alimshukuru Rais wa Magufuli kwa uamuzi wake wa kubatilisha ufutaji sahamba lake na kuuelezea uamuzi huo kuwa umezingatia haki na kusikia kilio chake ambapo alisema umempa faraja baada ya kuhangaika sana kuhusiana na shamba hilo.

"Nimemiliki shamba tangu mwaka 1987 na kuhangaikia hati kwa muda mrefu, na nimeshangazwa kuelezwa kuwa shamba langu liko katika mpango wa kufutwa kutokana na kutoendelezwa, hii imenifanya kuishi kwa wasiwasi," alisema Cecilia.

## Mbunge ataka uchunguzi wa safari za wabunge

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Nkasi Kaskazini (CCM), Ally Kessy, amesema kuna haja ya kuanza kuchunguza safari za wabunge wanapokwenda nje ya nchi, kwani wengi wao wanafuata posho kuliko maslahi ya Taifa.

Amesema mfano mzuri ni hivi sasa wabunge wengi wamejitokeza kwa wingi katika kufanya mazoezi wakijua kuna safari ya kwenda nje ya nchi ambayo inaposho kubwa. Kessy aliyasema hayo jana bungeni wakati akichagia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2020/21.

Kessy aliwataka wabunge wawe na moyo wa kumsaidia Waziri wa Fedha kuhusu matumizi.

Alisema wabunge wengi hawaendi katika mazoezi, na kwamba mara chache sana wanakwenda kwenye mazoezi wakisikia kuna safari kwa sababu wanafuata maslahi, na hawaoni huruma wananchi waliowaacha majimboni wakiwa na shida za maji.

"Leo nimeshuhudia, wamesikia kuna safari ya kwenda Uganda wamejazana kule kwa makundi, si kinamama wala kinababa, mimi nimewaambia kuwa naenda kuwachafua bungeni, mmezidi kama sisi ni muhimili wa Bunge lazima tuchunguze safari za wabunge wanapokwenda nje watatuletea aibu kubwa," alisema na kuongeza:

"Huwezi kwenda kucheza mpira huna mazoezi... hii lazima tuchunguzane ndugu zangu, sio tunapiga kelele hatuna maji hatuna barabara wakati nyie mnatanua, mnakwenda kustarehe huko hamna faida yoyote kwenda nje."

Akilitolea ufafanuzi suala hilo, Spika Job Ndugai, alisema ni kweli kutakuwa na safari ya wabunge kwenda Uganda kushiriki katika michezo.

Alisema wataufanyia kazi ushauri wa mbunge Kessy, na kwamba watakuwa makini katika kuchagua wabunge.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA 2 ENEO MOJA ZINAUZWA** Zipo Ukonga Mombasa. Ya mbele njengo wa kisasa vyumba 4 nyingine chumba na sebule 4 kiwanja robo eka. Za kupaua. Bei maelewano. Piga simu: 0719 619444 / 0782 574669.

**VIWANJA VITATU VINAUZWA,** NO.1-1341-1890 SQM NO. 2-1342- 1391 SQM NO.3 1343- 1556 SQM BLOCK A KISUKURU-TABATA. SIMU. 0754 857523/0786 857523

### NAFASI ZA KAZI

**Wanahitajika wanaume wenye umri kuanzia miaka 30 hadi 45** kwa nafasi za udereva (Ikiwemo Class C, C1, C2 na C3). Wanahitajika wanawake wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 35 kwa nafasi za mauzo (sales za bidhaa). Mshahara wa kuvutia utatolewa. Mawasiliano piga 0714 634 046. Piga simu kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni tu.

### 2 ACRE YARD FOR RENT


Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

### MCHANGANYIKO

**GENERATE MONEY AND JOBS* Learn DESIGNING** winning project proposals *Find DONORS *Establish NGO 0784505108 /0769505108.

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe**

### KUPOTEA KWA RESULT SLIP/HATI YA MATOKEO




**Leonard Lawrence Mushi** anatangaza kupotelewa na Hati ya Matokeo (ResultSlip) ya kidato cha sita yenye **index namba S0158/0632** iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2019 katika shule ya Sekondari Tosamaganga .

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa: 9910810624383

115511902


### KUPOTEA KWA VYETI



**ODILO YONAS KUIGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kumaliza darasa la saba kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Msingi MAHUTANGA mwaka 1982. Cheti cha Chuo cha Utabibu Msaidizi kilichotolewa na SONGEA RURAL MEDICAL AIDS TRAINING CENTRE (RMA) mwaka 1991.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **IFA/RB/4313/2016.**

### KUPOTEA KWA CHETI NA RESULT SLIP/HATI YA MATOKEO



115511802

**Hamisi Selemani Namyundu** anatangaza kupotelewa kwa cheti kidato cha nne yenye index namba S.3507.0029.2016 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Libobe na Result Slip/Hati ya matokeo ya Kidato cha nne yenye index namba S324/0514 iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2019 katika shule ya Lindi Sekondari

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **MS/RB/9015/2019**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;226/2019
Ombi la MAULID G MAGENI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu GERALD AGUSTINO MAGENI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 06/11/2019

115513302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI SHAHIDI**
**(MCA/84)**
**MAHAKAMA YA MWANZO YA MIKONGENI**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MADAI NAMBARI: 208...2018**

Mdai: DOROTEA ALBERT ANAMDAI
Mdaiwa: JOHN MARTIN CHAMZILA
Kwa: JOHN MARTIN CHAMZILA MKAZI WA KISAKI, IFAKARA MOROGORO

Ombi la Mdai: DOROTEA ALBERT
Madai ya: PESA SHILINGI 2,956,000/= PIA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI.

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani Siku ya JUMANNE ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 19 mwezi 11 mwaka 2019 saa 02:30Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 29 mwezi 10 mwaka 2019.

115513202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA**
**SHAURI LA MADI YA PESA NAMBARI 223 YA 2017**

**MDAI.......... NEWTON KITUNDU (MKURUNGEZI PUNUNTA'S FINANCE CO. LTD)**
DHIDI YA
MDAIWA.........................................SIMON IGOTI

KWA: SIMON IGOTI

**YAH: KUITWA SHAURINI**

POPOTE PALE ULIPO

Fahamu kwamba mdai ameleta madai yake Mahakamani dhidi yako. Madai haya yamesikilizwa na kusoma hukumu siku ya tarehe 27/11/2017 kwa kuamriwa kulipa.

Shauri limepamgwa kwa ajili ya utekelezaji tarehe 29/11/2019.

Fahamu kwamba unatakiwa kuhudhuria Mahakamani wewe mwenyewe siku hiyo bila kukosa. Kutohudhuria kwako kutaifanya Mahakama hii iendelee na utekelezaji bila wewe kuwepo

Imetolewa kwa amri na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 08/11/2019

115513102

TANZANIA CHINA TRADE & TOURISM DEVELOPMENT LTD anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 643 BWJ.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MUH/RB/3791/2019.**

115513002

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**HELENA IZAHAKI TANO** anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI aina ya BAJAJI BOXER yenye namba za usajili MC452 BJR Chassis namba MDZA21BZ8GWB52953 Engine na. PFZWGBO8868 range Black.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DOM/RB/5287/2019

215512302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA: 272..2019**

Mdai: MOHAMED ATHUMANI DHIDI YA
Mdaiwa: MATHIAS KABELEBENZE
Kwa: MATHIAS KABELEBENZE K/MBUYUNI-MOROGORO

Ombi la Mdai: MOHAMED ATHUMANI
Madai ya: PESA SHILINGI 3,720,000/=

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 13 mwezi 11 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 06 mwezi 11 mwaka 2019.

215512202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;219/2019
Ombi la **DINA KAPELELE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SAMORA ERNEST MDOE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/11/2019

2155121002

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**PIUS MUKULASI JULIUS.**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Bajaji Boxer, yenye Namba MC941BRL, chasis No. MD2A18AZ4HWM52694, Engine No.DUZWHMI4204. Kadi ilipotea, na aliripoti kituo cha polisi cha Bukoba tarehe 6/11/2019 na kupewa No: **KAG/BUK/RB/455931/2019.**

Kwa yeyote atakayeiona haipeleke kituo cha polisi kilichoko karibu naye.

Au awasiliane naye. **No: 0756695768.**

215512402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 270 YA 2019**
**BAINA YA**
**ROBINSON JOHN KAYUNI......................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**DOTTO HUSSEIN KAOBA ...............MDAIWA**

KWA:- DOTTO HUSSEIN KAOBA POPOTE ULIPO
YAH: KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 27.11.2019 saa 3.00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

ANGALIZO:-Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 07 ya Mwezi wa November,2019.

215512002

**Kwa Habari Motomoto**

usikose

Nipashe

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# LACAZETTE: MAPUMZIKO YATARUDISHA NGUVU




**LONDON,** England

ALEXANDRE Lacazette amesema mapumziko ya mechi za kimataifa yamekuja wakati muafaka kwa kikosi chake cha Arsenal kupata nafasi ya kujiimarisha na kurudisha kujiamini.

'Washika Bunduki' hao walipata kichapo cha mabao 2-0 kutoka Leicester City Jumamosi na sasa wamecheza mechi tano mfululizo bila ushindi kwenye mashindano yote.

Uvumi kuhusu majaliwa ya kocha Unai Emery yameendelea kuwa gizani na presha imeongezeka kwa raia huo wa Hispania.

Mshambuliaji huyo wa Ufaransa ambaye hakuwapo kwenye kikosi kilichocheza mchezo wa kufuzu wa Euro 2020 mwezi uliopita, ana matumaini mapumziko ya wiki mbili kabla ya mchezo ujao wa Arsenal utawafanya wajiamini zaidi.

"Tumekosa ujasiri na kujiamini na tunahitaji mechi za kimataifa ili kurudisha makali yetu," alisema Lacazette akinukuliwa na Gazeti la Mirror.

Distributed via ippmedia

# Messi ndani Rojo, Pereyra wakitemwa

**BUENOS AIRES,** Argentina

NYOTA wa Argentina, Marcos Rojo na Roberto Pereyra wameachwa kwenye kikosi cha timu hiyo kinachojiandaa kwa mechi za kirafiki za kimataifa dhidi ya Brazil na Uruguay.

Lionel Messi anajiandaa kurudi kuichezea nchi yake kwa mara ya kwanza baada ya kumaliza kifungo cha miezi mitatu, lakini beki Rojo na kiungo Pereyra wameachwa katika kikosi hicho cha kocha, Lionel Scaloni.

Rojo aliachwa kwenye kikosi cha Manchester United kilichoibuka na ushindi wa mabao 3-1 kwenye Ligi Kuu dhidi ya Brighton na Hove Albion Jumapili na Pereyra anayekipiga pale Watford anasumbuliwa na maumivu ya misuli ya nyama za paja.

Argentina pia imemwita nyota wa Boca Juniors, Alexis Mac Allister kwa ajili ya mchezo huo wa Ijumaa dhidi ya Brazil utakaopigwa nchini Saudi Arabia na mchezo wa Novemba 18 dhidi ya Uruguay utakaopigwa jijini Tel Aviv nchini Israel.

Messi amerudi kwenye kikosi hicho, baada ya nahodha huyo wa Barcelona na Argentina kulishutumu Shirikisho la Soka la Amerika Kusini kujihusisha na rushwa na kutozwa faini ya euro 50,000 Agosti mwaka huu.

Messi alilishutumu shirikisho hilo kujihusisha na rushwa baada ya kikosi chake kufungwa na Brazil kwenye nusu fainali ya Copa America.





# Guardiola akataa kutia neno mwamuzi mechi na Liverpool

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesisitiza kwamba kusalimiana na mwamuzi Michael Oliver haikuwa na maana ya kuwalaumu maofisa wa mchezo huo, baada ya Manchester City kukumbana na kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Liverpool kwenye Uwanja wa Anfield juzi, Jumapili.

City iliambulia kichapo hicho skukrani kwa mabao kutoka kwa Fabinho, Mohamed Salah na Sadio Mane.

Liverpool inaongoza msimamo wa ligi hiyo kwa pointi nane dhidi ya Leicester City waliopo nafasi ya pili na Chelsea na kuwazidi pointi tisa vijana hao wa Guardiola.

City walidai Trent Alexander-Arnold kuunawa mpira ndani ya eneo la hatari la Liverpool na hakuadhibiwa kabla ya kufanya shambulio la kushtukiza na Fabinho akafunga bao la kwanza.

Huku pia Raheem Sterling alionekana kudondoshwa kabla ya Sadio Mane kuudokoa mpira uliopiga mkono wa Alexander-Arnold.

Baada ya mchezo huo, Guardiola alionekana akisema "asante sana" Oliver na wasaidizi wake kwa mchezo huo ambao kwao walionekana kama walinyimwa penalti.

"Halikuwa jambo zuri kuzungumzia mwamuzi baada ya sisi kufungwa," alisema Guardiola.

"Muulize Mike Riley (Mkurugenzi wa Bodi ya Waamuzi wa Uingereza) ndiye anayejua zaidi na si mimi.

"Sikuwa na maana mbaya, nilisema 'asante sana'. Na nilisema hivyo kwenye mchezo dhidi ya Tottenham.

"Mara zote huwa nawachukulia waamuzi kama watu wa kawaida, huwa nasema 'asante sana, kila la heri'.

"Hii siipendi, kwa sababu inaonekana kama vile mimi nalalamika, ukweli ni kwamba kila baada ya mchezo huwa napenda kuwashukuru waamuzi na si kwamba nawalalamikia.

"Watu wanaitafsiri vibaya, lakini ukweli huwa napenda kusema asante sana na hongera na pia nawapongeza kwa Liverpool kwa ushindi wa 3-1."

HABARI MICHEZO

# Solskjaer amsogezea unahodha Maguire

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema Harry Maguire anafaa kuwa nahodha wa muda mrefu baada ya kuvaa kitambaa hicho Jumapili wakati wakiibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Brighton and Hove Albion.

United ilipata ushindi huo mnono pale kwenye Uwanja wa Old Trafford dhidi ya Brighton, huku Maguire akiiongoza timu hiyo kwa mara ya kwanza tangu aliponunuliwa kwa pauni milioni 80 akitokea kule Leicester City.


Beki huyo wa kati alivaa kitambaa hicho cha unahodha kutokana na kutokuwapo kwa Ashley Young, ingawa Solskjaer amebainisha kwamba Maguire anaweza kuendelea kukivaa kitambaa hicho kwa miaka mingi ijayo.

"Harry amekuwa kiongozi mzuri kwenye vyumba vya kubadilishia nguo na dimbani," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Anaweza kuwa nahodha wa muda mrefu."

Nyota wa United ambaye alifunga bao la uongozi, Scott McTominay alionekana kuchechemea mguu wake wa kushoto wakati akitoka uwanjani, lakini Solskjaer hakuweza kubainisha wazi kwamba mchezaji wake huyo ameumia kwa kiasi gani.

"Aliumia enka, lakini siwezi kusema kwa kiasi gani kwa sasa," alisema Solskjaer.






Distributed via ippmedia

# LAMPARD ATAKA WILLIAN APEWE MKATABA MPYA

**LONDON,** England

FRANK Lampard ameweka majaliwa ya baadaye ya Willian mikononi mwa viongozi wa Chelsea, lakini ana matumaini kwamba winga huyo ambaye kwa sasa yupo kwenye kiwango bora anaweza kuongezewa mkataba mpya.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na bado majaliwa yake hayajajulikana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alitoa pasi ya mwisho kwa bao la ufunguzi la Tammy Abraham mwishoni mwa wiki wakati wakiibuka na ushindi dhidi ya Crystal Palace.

Kiwango chake kimezimwa na wachezaji vijana ambao Lampard ameamua kuwaamini na bosi huyo wa Blues alibainisha matarajio yake kwa winga huyo baada ya ushindi wa Jumamosi wa 2-0 pale kwenye dimba la Stamford Bridge.

Lakini akaweka wazi maamuzi ya mwisho juu ya kupewa mkataba mpya wa winga huyo kuwa hayapo mikononi mwake.

"Suala la kupewa mkataba mpya si langu kwa sababu mimi sihusiki na fedha," alisema Lampard.

"Lakini kila mmoja anaona namna gani ninavyompa nafasi ya kucheza uwanjani, na anaonyesha kiwango cha kuvutia, nampenda na hata staili yake ya uchezaji.

# Klopp: Nataka pointi Liver kila mechi EPL

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema Liverpool inatakiwa kupata pointi katika kila mchezo wa Ligi Kuu ili kuisaidia timu hiyo wakati ikikabiliwa na "wakati mgumu zaidi" ndani ya wiki sita zijazo.

Ushindi wa Liverpool wa mabao 3-1 dhidi ya Manchester City Jumapili kuliifanya iongoze msimamo wa Ligi Kuu kwa tofauti ya pointi nane na ikiwapita pointi tisa mabingwa hao watetezi.

Lakini sasa 'Wekundu' hao wanakabiliwa na wakati mgumu zaidi, wakitakiwa kucheza mechi kila baada ya siku chake baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa hadi mwaka mpya, na Klopp amesema wanatakiwa kupata pointi katika kila mchezo wa Ligi Kuu, ili kuweza kupita salama kwenye wakati huo.

"Sijui nini kitatokea ingawa kwa sasa tunaongoza kwa pointi tisa dhidi ya City, hasa baada ya mchezo dhidi yao," Klopp aliiambia Sky Sports.

"Kila mchezo lazima tupate pointi ili tuweze kupita kwenye wakati mgumu unaotukabili.

"Unaona jinsi Chelsea na Leicester wanavyocheza kwa sasa, kama tungepoteza mchezo wa Jumapili, maana yake ingekuwa tunaongoza kwa pointi tano.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




Distributed via pressreader/ppmedia

# SARRI AJITETEA RONALDO AKIONDOKA UWANJANI

## Wachezaji wote ambao wanajaribu kuonyesha ubora na kisha kutolewa, hukasirika angalau...

**TURIN,** Italia

MAURIZIO Sarri hasumbuliwi na kufadhaika kwa Cristiano Ronaldo kufuata kumfanyia mabadiliko ('sub') na ameeleza Juventus lazima imshukuru nyota huyo kwa kucheza huku akipitia kipindi cha majeraha.

**Macho yalitupiwa kwa Ronaldo Jumapili baada ya kutolewa dakika ya 55, wakati wakishinda kwa bao 1-0 dhidi ya AC Milan kwenye mechi ya Serie A na nafasi yake kuchukuliwa na Paulo Dybala ayeifungia Juve bao hilo pekee wakiwa Turin.**

Hali hiyo imekuja siku tano tu baada ya Ronaldo kufanyiwa mabadiliko zikiwa zimebaki dakika nane dhidi ya Lokomotiv Moscow na wakiwa katika uhitaji wa bao, ambalo hatimaye lilipatikana dakika za majeruhi kupitia kwa Douglas Costa kwenye mechi hiyo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, juzi Ronaldo alijibu kwa kuonyesha hasira katika tukio hilo ambapo alitoka moja kwa moja kupitia lango kubwa uwanjani hapo wakati alipofanyiwa mabadiliko kwenye mechi dhidi ya mahasimu wao, AC Milan.

Lakini Kocha Mkuu wa Juve, Sarri kwa mara nyingine amesisitiza kuwa Ronaldo ambaye aliripotiwa kutoka katika Uwanja wa Allianz kabla ya kipenga cha mwisho, anasumbuliwa na jeraha la goti ambalo limekiathiri kiwango chake na anaamini majibu ya mfadhaiko wake umetokana na hilo.

"Lazima tumshukuru Ronaldo, kwa sababu amejitolea kuwa pale usiku wote wa leo [juzi] katika hali ngumu," Sarri aliiambia Sky Sport Italia.

"Amefanya kila liwezekano kucheza, lakini niliona hakuwa sawa na nikafikiri ilikuwa vema kumtoa nje.

"Ni kawaida mchezaji kupatwa na hasira akiondoka uwanjani, haswa anapofanya bidii ili awepo pale.

"Zaidi ya mwezi uliopita, alikuwa na tatizo la goti, aliligonga katika mazoezi na liliumia kwa ndani.

"Wakati anapofanya mazoezi kwa kiwango cha juu ama kucheza, kunamkosesha uwiano, hivyo anaishia kuzidi kusababisha matatizo ndani ya kigimbi cha mguu na misuli ya paja.

"Inaathiri kiwango chake na hayupo katika ubora wake kwa sasa. Wachezaji wote ambao wanajaribu kuonyesha ubora wanakuwa na kukasirika angalau kwa dakika tano ama wakati wanapofanyiwa mabadiliko, lakini kocha kwa ujumla atakuwa na wasiwasi zaidi ikiwa hakuonekana kukasirika."

## ZISIKUPITE

### IBRAHIMOVIC KURUDISHWA UTD

Manchester United inaweza kujitia majaribuni kumsajili mshambuliaji Zlatan Ibrahimovic na kumrudisha hapo Old Trafford. Nyota huyo wa zamani wa kimataifa wa Sweden atakuwa mchezaji huru wakati huu mkataba wake na miamba ya MLS, LA Galaxy ukielekea ukingoni. ***(TuttoMercatoWeb, via Mail)***

### EMERY AHAKIKISHIWA ARSENAL

UONGOZI wa Arsenal upo nyuma ya kocha Unai Emery kwa "asilimia 100" na unapanga kusubiri hadi majira ya joto kabla ya kufanya uamuzi huhusu mustakabali wa baadaye wa Mhispania huyo. ***(The Athletic)***

### ZIYECH KUMRITHI ERIKSEN

Tottenham itamfuata winga wa Ajax na Morocco, Hakim Ziyech, 26, kama na wakati nyota wa kimataifa wa Denmark, Christian Eriksen, 27, ataondoka klabuni hapo. ***(90min)***

### NEYMAR BADO PSG- BABA

BABA wa nyota wa kimataifa wa Brazil, Neymar Sr. amesema hatakuwa akifanya mazungumzo na Barcelona kuhusu mwanawe, Neymar Jr, 27, kurudi klabu hiyo ya Nou Camp na kwamba mshambuliaji huyo ataendelea kubaki Paris St-Germain. ***(ESPN Brazil, via Mail)***

### KANTE KUZEEKEA CHELSEA

KIUNGO wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante, 28, amejiweka mbali mwenyewe na uwezekano wa kujiunga na Real Madrid na amesema anaweza kumalizia soka lake hapo Stamford Bridge. ***(Sun)***

### ENRIQUE KUITOSA ARSENAL

KOCHA wa zamani wa Hispania, Luis Enrique, ambaye amekuwa akihusishwa na kurithi mikoba ya Unai Emery katika kikosi cha Arsenal, hafikiri kurudi katika uongozi kwa sasa. ***(ESPN)***

### INTER KWA MERTENS, MEUNIER

Inter Milan inavutiwa na huduma ya mshambuliaji wa kimataifa wa Ubelgiji, Dries Mertens, ambaye mkataba wake na Napoli utamalizika majira ya joto yajayo. Klabu hiyo ya San Siro pia ipo tayari kuisaka huduma ya mchezaji wa Paris St-Germain, Mbelgiji Thomas Meunier, 28, na beki mwenzake Mfaransa Layvin Kurzawa, 27. ***(Calciomercato)***

### 'RONALDO KAPOROMOKA'

KOCHA wa zamani wa England, Fabio Capello amesema kiwango cha uchezaji wa Ronaldo kimeshuka kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita. ***(Marca)***

### TRAORE AITWA HISPANIA, MALI

MSHAMBULIAJI wa Wolves, Adama Traore, 23, yupo katika vita kali ya kufanya uamuzi wa timu ipi ya taifa aitumikie baada ya kuitwa na zote mbili, Hispania na Mali. Traore alizaliwa nchini Hispania lakini wazazi wake wakiwa wazawa wa Mali. ***(Sun)***

### UNITED KWA PHILLIPS, WHITE

KIUNGO wa Leeds United, Muingereza Kalvin Phillips, 23, pamoja na raia mwenza, beki Ben White, 22, anayecheza kwa mkopo hapo Elland Road akitokea Brighton, wanafuatiliwa na Manchester United. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

## Mayanja: Julio ataimudu KMC

**Na Focus Nicus**

BAADA ya kuachana na Klabu ya KMC, aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mganda Jackson Mayanja amewaponda wachezaji wa timu hiyo kwa kutaka kujipangia mfumo wa kutumia huku akifunguka anayeweza kuinoa klabu hiyo ni Jamhuri Kihwelo 'Julio' pekee.

Wiki iliyopita KMC FC iliachana rasmi na Mayanga kwa kile kilichoelezwa ni matokeo mabaya tangu alipoanza kuinoa timu hiyo ya Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, akizungumza kabla ya kuondoka kurejea kwao Uganda, Mayanja alisema wachezaji walimuangusha kutokana na kutojituma huku wakitaka kutumia mfumo wanaoutaka wao.

Aidha, alisema yeye ni kocha 'Professional' hivyo hawezi kupelekeshwa na wachezaji pamoja kupangiwa timu na uongozi na kwamba timu hiyo anayeiweza ni Julio pekee ambaye anajua namna ya kudili na wachezaji waswahili.

"Mimi uswahili siuwezi, hii timu anaiweza kocha kama Julio ambaye anajua kudili na wachezaji kama hawa," alisema.

Hata hivyo, inadaiwa kwa sasa uongozi wa KMC upo kwenye mazungumzo na kocha wa zamani wa Simba, Mrundi Masoud Djuma kuja kuinoa timu hiyo iliyomaliza nafasi ya nne msimu uliopita ikiwa nchini ya Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije.

## Mwadui waipigia mahesabu Prisons

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, amesema kikosi chake kinatarajia kuanza maandalizi ya mechi yake ya Ligi Kuu Bara dhidi ya "Maafande" wa Tanzania Prisons hapo keshokutwa.

Tanzania Prisons itaikaribisha Mwadui FC Novemba 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Khalid alisema ameandaa programu maalumu ambayo itawaweka imara wachezaji wake kuhakikisha wanafanya vema katika mechi hiyo kwa sababu wamelenga kufanya vizuri zaidi msimu huu.

"Kikosi changu kitaanza tena mazoezi Alhamisi, ili kujiandaa na mechi dhidi ya Prisons ambayo itachezwa Novemba 23, jijini Mbeya, tutaenda huko na lengo moja la kuibuka na pointi tatu za ugenini," alisema Khalid.

Alisema kikosi chake hakina majeruhi na anawaandaa wachezaji wake kuamini kila mchezo ni sawa na fainali.

"Nashukuru sina majeruhi wengi, zaidi ya wale wa kawaida ambao hawashindwi kuingia uwanjani na kucheza, naamini mpaka siku hiyo kila mchezaji atakuwa sawa kwa ajili ya mchezo huo," alisema kocha huyo.

# ZAHERA AMTAJA BOCCO STRAIKA HATARI LIGI KUU

**Na Shufaa Lyimo**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema mchezaji wa Tanzania anayemkubali uwezo wake ni nahodha na mshambuliaji wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, John Bocco.

**Akizungumza na gazeti hili kabla ya kuondoka nchini, Zahera, alisema mshambuliaji huyo ana kiwango kizuri na uwezo aliokuwa nao, anastahili kucheza soka la kulipwa nje ya Tanzania.**

Zahera alisema Bocco, ambaye kwa sasa ni majeruhi, ameiva na anaweza kupata klabu ya kuitumikia nje ya Tanzania, endapo mchakato mzuri wa kumtafutia timu utafanyika.

"Mimi kwa Tanzania namkubali sana John Bocco, ni mchezaji ambaye uwezo wake umenivutia, vile vile ana kiwango kizuri anapokuwa uwanjani, kwa uwezo huo hastahili kucheza Tanzania, alitakiwa awe anacheza soka la kulipwa nje ya nchi," alisema Zahera.

Kocha huyo amemtaka mshambuliaji huyo wa zamani wa Azam FC, kuongeza juhudi ili aweze kufika mbali kwa sababu sifa za kukiendeleza mbele kipaji chake anazo.

"Bocco akijituma zaidi atafika mbali kwa sababu naamini uwezo wake ni mkubwa akipata nafasi ataileta sifa nchi yenu ya Tanzania," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, Zahera amewataka mabosi wake wa zamani wa Yanga kubadilika na kuachana na tabia ya kusajili wachezaji na jukumu hilo wanatakiwa kuliacha kwa kocha ambaye anakiongoza kikosi chao.

Yanga iliamua kuachana na Zahera, muda mfupi baada ya timu yao kuondolewa na Pyramids ya Misri kwenye mechi ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya



Wachezaji wa kikosi cha timu ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania Bara 'Kilimanjaro Queens' wakiendelea na mazoezi katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam, chini ya kocha wao Bakari Shime (kulia), kujiandaa na michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge) kwa wanawake inayotarajiwa kuanza Novemba 16 hadi 24, mwaka huu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *TFF, ZFF wakutana kumaliza 'utata'*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa Shirikisho na Soka Zanzibar (ZFF), pamoja na wenzao wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wamekutana katika kikao kilichofanyia visiwani hapa kwa ajili ya kujadili changamoto mbalimbali zinazoendelea baina ya vyama hivyo, imefahamika.

Kikao hicho kiliwakutanisha wajumbe sita, watatu kutoka kila upande, na kilifanyika katika ukumbi wa mikutano wa ZFF, ulioko kwenye Uwanja wa Amaan, Mjini Unguja.

Katika kikao hicho, TFF iliwakilishwa na Katibu Mkuu, Wilfred Kidao, Mkurugenzi wa Mashindano, Salum Madadi na Mkurugenzi wa Ufundi, Oscar Mirambo, wakati Katibu Mkuu wa ZFF, Mohammed Ali Hilal (Tedy), Mkurugenzi wa Mashindano, Ali Muhamad na Meneja wa Leseni za Klabu, Mbarouk Othman, waliwakilisha Zanzibar.

Ajenda tano zilizojadiliwa katika kikao hicho ilikuwa ni mgawo wa fedha kutoka Fifa, timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), mahusiano kati ya ZFF na TFF na hatima ya fedha za uhamisho za wachezaji wanaotoka kwenye Ligi Kuu Zanzibar na kuhamia Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Leseni za klabu, Othman, alisema wamefikia hatua nzuri ya majadiliano katika kikao hicho cha kwanza na wanaamini baada ya kufanyika kikao cha pili huko jijini Dar es Salaam watapata muafaka.

Othman alikataa kuweka wazi kilichojadiliwa zaidi katika kikao hicho, hadi pale watakapomaliza kikao kinachofuata ambacho malengo yake ni kuendeleza soka la hapa Tanzinia.

Naye Kidao alisema kikao hicho ni cha kawaida na kimefanyika katika kuendelea kujenga ushirikiano baina ya pande hizi mbili.

Kidao alisema wanaamini kupitia vikao hivyo, malalamiko yatamalizika na kitakachofuata ni kuendeleza programu za maendeleo.

# Michezo

Jumanne Novemba 12, 2019

Nipashe




Sarri ajitetea Ronaldo akiondoka uwanjani UKURASA 30

LA TATU HILO...



Distributed via ippmedia

Sadio Mane akiitendea haki krosi ya Jordan Henderson kutoka winga wa kulia kwa kuuzamisha mpira kimyani kwa kichwa na kuifanya Liverpool kuwa mbele kwa mabao 3-0 wakati ikishinda 3-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Manchester City iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi, Jumapili. **HABARI UK.28**

# FIFA YAMFUNGIA MALINZI MIAKA 10

## ●●● Ni kwa matumizi mabaya ya fedha za shirikisho hilo, pia atakiwa kulipa faini Sh. bilioni moja huku...

**ZURICH, Uswisi**

SHIRIKISHO la Soka Duniani (Fifa), limemfungia kwa miaka 10, Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Jamal Malinzi kwa matumizi mabaya ya fedha za shirikisho hilo.

**Aidha, kifungo hicho pia kinakwenda sambamba na Malinzi kulipa faini ya dola 503,000 sawa na Sh. bilioni 1.1 za Tanzania kwa Fifa.**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Fifa, imeeleza Malinzi alipokea dola 528,000 (Sh. bilioni 1.2) kwa zaidi ya miaka minne kwa madai ya kulipia mikopo ambayo "ilikosa uthibitisho ama maelezo sahihi"

Pia ilieleza Malinzi alipokea dola 55,000 (Sh. milioni 126. 3) fedha ambazo zilikuwa zawadi kwa timu ya Taifa ya Vijana ya Tanzania chini ya miaka 17 (Tanzania U-17) kwa kushiriki fainali za Mataifa ya Afrika iliyofanyika Gabon 2017.

FIFA imesema Malinzi alikuwa mjumbe wa Kamati yake ya Maendeleo ya kutenga pesa za miradi yote duniani kipindi akiwa katika jukumu hilo la mchezo wa haki na kamati ya uwajibikaji kijamii kuanzia mwaka 2013-17 wakati akichukua fedha hizo.

**ALIPO MALINZI**

Kwa sasa Malinzi na wenzake, aliyekuwa Katibu Mkuu wa TFF, Selestine Mwesigwa na Mhasibu wa TFF, Nsiande Isawayo Mwanga (27) wapo rumande wakikabiliwa na mashtaka ya utakatishaji wa fedha.

Katika kesi hiyo ya jinai namba 213 ya mwaka 2017, washtakiwa Malinzi, Mwesigwa na Nsiande walikosa dhamana kutokana na kesi inayowakabili kutokuwa na dhamana.

Kesi hiyo ilikuwa na mashtaka 30, lakini ilipofikia katika uamuzi wa kama washtakiwa wana kesi ya kujibu ama la walipunguziwa mashtaka 10 kati ya 30 yaliyokuwa yakiwakabili baada ya Jamhuri kushindwa kuonyesha kama washtakiwa wana kesi katika makosa hayo.

Mahakama hiyo iliwakuta wana kesi ya kujibu washtakiwa hao kwa mashtaka 20 yaliyobakia baada ya Jamhuri kuonyesha kwamba wana kesi, hivyo walijitetea wenyewe bila kuita na mashahidi. Upande wa Jamhuri katika kesi hiyo iliyokuwa na mashahidi 15 na vielelezo tisa.

Aidha, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, Novemba 7, mwaka huu ilipiga kalenda kutoa hukumu ya kesi hiyo ya Malinzi na wenzake mpaka Novemba 21, mwaka huu.

# Aussems afurahia ugumu Ligi Kuu

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi chake kikiwa kinaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema anafurahia kuona ushindani uliopo katika ligi hiyo msimu huu umeongezeka na kueleza kuwa hali hiyo inaongeza umakini kwenye timu yake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems alisema ushindani pia unasaidia kuimarisha viwango vya wachezaji kwa sababu kila mmoja anajiimarisha ili apate namba katika kikosi cha kwanza.

Aussems alisema ushindani unapokuwa mkubwa, kila timu inalazimika kuongeza mbinu za kusaka ushindi kwa sababu hakuna anayeamini atapata matokeo mazuri kabla ya kuingia uwanjani.

"Ushindani ni mzuri, utafanya kila mmoja afahamu hayuko mahali salama, hakuna jambo jepesi, tunajiimarisha kila siku, kwa sababu tunataka kupata matokeo mazuri, hakuna mechi nyepesi, hakuna mwenye uhakika wa kushinda nyumbani au ugenini," alisema Aussems.

Mbelgiji huyo aliongeza kuwa mbali na ushindani katika ligi, pia katika kila timu kuna ushindani na hali hii inasaidia kuwafanya wachezaji "waamke" na kujipanga kupambana.

"Mechi ni ngumu, timu zimeimarika, kila upande sasa unafanya vizuri, tayari wachezaji wameimarika tofauti na tulivyoanza msimu, ili tufikie malengo, tunatakiwa kujituma zaidi," alisema kocha huyo.

Alisema kuwa baada ya kuwapa mapumziko wa siku mbili, kikosi chake kilianza mazoezi ya kujiandaa na mechi dhidi ya Ruvu Shooting, na anaamini ataendelea kuwatumia wachezaji wote waliosajiliwa kulingana na aina mpinzani wanayekutana naye.

9 770856 541002 >